

# **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

## **BUNGE LA TANZANIA**

---

## **MAJADILIANO YA BUNGE**

---

## **MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Tano – Tarehe 12 Aprili, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## **D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## **HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

### **NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):**

Taarifa ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioisha tarehe 30 Juni, 2010 (*The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Financial Statements of Local Government Authorities for the Financial Year ended 30<sup>th</sup> June, 2010*).

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE.GREGORY G. TEU):** Taarifa ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2010 (*The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of the Financial Statement of the Central Government for the Year ended 30<sup>th</sup> June, 2010*).

Taarifa ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma kwa Mwaka 2009/2010 (*The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Financial Statement of Public Authorities and other Bodies for the Financial Year 2009/2010*).

Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Ukaguzi wa Ufanisi na Upembuzi kwa kipindi kilichoishia tarehe 31 Machi, 2011 (*The General Report of the Controller and Auditor General on the Performance and Forensic Audit Report for the Period ended 31<sup>st</sup> March, 2011*).

Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi wa ufuatiliaji na Tathmini ya Mgawanyo wa Bajeti kwa Shughuli za Huduma za

Kijamii kwa Akina Mama na Watoto Tanzania (*The General Report of the Controller and Auditor General on Performance Audit on the Monitoring, Evaluations and Budget All action for Maternal Health care activities in Tanzania*).

## **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 61

### **Wabunge wa Viti Maalum wa Upinzani Kubaguliwa**

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI** aliuliza:-

Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa inaeleza kuwa Baraza la Madiwani linaundwa na Madiwani wa Kata, Wabunge wa Majimbo, Wabunge wa Viti Maalum na wale wa Kuteuliwa wanaotoka katika Halmashauri ikiwa ni pamoja na Kamati ya Fedha, Uchumi na Mipango. Aidha, kumekuwepo na Wabunge wa Viti Maalum wa Upinzani kuzuiliwa kuhudhuria Vikao vya Kamati ya Fedha, Uchumi na Mipango katika Halmashauri zao:-

- (a) Je, ni sheria ipi inayoruhusu ubaguzi kwa Wabunge hao?
- (b) Je, Wabunge hao watatekeleza vipi wajibu wao kwa Wananchi kwa kuwa wanazuiwa kuhudhuria vikao hivyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika Sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hakuna Sheria yoyote inayoruhusu ubaguzi wa aina yoyote.

(b) Mheshimiwa Spika, Kamati za Kudumu zote za Halmashauri, isipokuwa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango, zinapaswa kuwa na Wajumbe wasiozidi theluthi moja ya Wajumbe wote wa Baraza. Kwa upande wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango, Kanuni za Kudumu za Halmashauri zinaelekeza kuwa, Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango ni wale tu wanaoingia kwa nyadhifa zao ambao ni Mwenyekiti au Meya; Makamu Mwenyekiti au Naibu Meya; Mbunge wa kuchaguliwa anayewakilisha Jimbo; Wenyeviti wa Kamati za kudumu za Halmashauri; na Wajumbe wawili miongoni mwa Madiwani wote wanaoteuliwa na Mwenyekiti wa Halmashauri na kuthibitishwa na Baraza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kila Jimbo lina Mbunge wa kuchaguliwa, Mbunge huyo ndiye anayewajibika kwa Wananchi wote wa makundi yote yaliyomo kwenye Jimbo hilo na anayepaswa kujua kinachoendelea katika Jimbo husika na endapo Mbunge wa Viti Maalum atakuwa na jambo la kuliwasilisha kwenye Vikao vya Halmashauri, atawasilisha hoja hiyo kwenye Baraza la Madiwani, ambalo linawajumuisha Wajumbe wote au atawasilisha kwa Mbunge wa Jimbo ambaye atawasilisha kwenye Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ambayo nayo hayakuniridhisha sana, nina maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Ikiwa Kanuni za Halmashauri zinaelekeza kuwa Wabunge wa Viti Maalum si Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Halmshauri ama Manispaa; jambo ambalo linashangaza kwa kuwa Wabunge wa Viti Maalum wanaruhusiwa kuwa Wajumbe wa Bunge wa Kamati ya Fedha nikimaanisha Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na LAAC; je, Waziri haoni kwamba, Kanuni hizi za Halmashuri zimepitwa na wakati na zinahitaji kubadilishwa ili kuongeza nguvu katika usimamiaji wa fedha za umma tukizingatia kwamba ubadhirifu mkubwa wa fedha hizi unatokea katika Halmashauri zetu?

(b) Mheshimiwa Spika, katika Kikao cha Kamati ya Uongozi na Mipango cha Halmashuri ya Wilaya ya Singida kilichofanyika tarehe 10 Februari, 2011, Wabunge wa Viti Maalum tulipata barua za mwaliko kutoka kwa Wakurugenzi kuhudhuria kikao hicho. Cha kushangaza, tulipofika Mkurugenzi huyo baada ya kutukabidhi makabrasha, alittoa nje tena bila staha kwa kutueleza kuwa, sisi hatukuwa Wajumbe wa Kikao hicho. Je, Waziri anasema nini juu ya udhalilishaji huo uliofanywa na Mkurugenzi mbele ya Watumishi wa Halmshauri na Madiwani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninachokizungumza hapa, ninazungumzia Sheria na Kanuni zinazotawala mpango huu. Ninajua kabisa kwamba, jambo hili lina *sensitivity* yake, Wabunge wote wa Viti Maalum wanajisikia kwamba wamebaguliwa, Sheria aninayoisoma hapa ndivyo inavyotamka na Kanuni zetu ndivyo zinavyosema.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba, kama Mheshimiwa anafikiri hii Sheria imepitwa na wakati, basi sasa ni wakati wa kufukiria tufanye nini; mimi sikuja hapa kuleta la kwangu, ninaleta kile kilichopo hapa. Kwa hiyo, kama kuna mawazo hapa ya kubadili, mimi sina *objection*; kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninasema hili tutalijadili na ndiyo maana liko tamko hapa lilitolewa na Mheshimiwa Celina Kombani, linalofafanua jambo hili ninalolizungumza. Ninakubali kwamba, sasa ni wakati muafaka

wa kutafakari jambo hili sote kwa pamoja, tuone tufanye nini ili na wao waweze kuingia. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, hili sasa linalozungumzwa la Mkurugenzi anayesemekana kwamba, ameandika barua akawaalika, ina maana wao siyo Wajumbe wa Kamati ile; lakini sasa tunasema kwamba, kuna barua imeandikwa hapa. Mimi nakuomba nikimaliza kujibu maswali, nitapiga simu sasa hivi ninataka aniambie ni kwa nini aliandika barua halafu watu wanafika mlangoni anawaambia tokeni. Kama amewaita, ina maana aliona umuhimu wa wao kukaribishwa kwenye ile Kamati. Sasa hili ni jambo ambalo siwezi kulijibu hapa, lakini ninataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba, nitatoa majibu baadaye kuelezea kilichotokea na barua hizo kama mnazo ninaomba mnipatie ili nishuke naye huyo. (*Makofi*)

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa katika Halmashauri za Wilaya siyo mahali pekee ambapo Wabunge wa Viti Maalum wamekuwa wanatengwa; na kwa kuwa katika Bodi za Barabara za Mikoa, Wabunge Wanawake wa Viti Maalum nao wamekuwa wanatengwa na siyo Wajumbe wa Bodi za Barabara za Mikoa; na kwa sababu Mheshimiwa Waziri amesema yuko tayari kusikiliza na kufikiria uwezekano wa kufanya mabadiliko ya msingi katika Sheria ili kutokuwabagua Wanawake katika uwakilishi wao; je, Mheshimiwa Waziri haoni kuwa hili jambo ni vizuri likaingizwa katika mpango huo?

**SPIKA:** Sisi kwetu huwa wanahudhuria; sijui wapi huko? Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Freeman Mbowe, jirani yangu, Mbunge wa Hai na pia Kiongozi wa Upinzani hapa Bungeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, unajua katika ulimwengu wa leo, kusimama hapa halafu ukasema kwamba, Wanawake wabaguliwe, utapata mgogoro ambao haujawahi kuuona hapa duniani. (*Kicheko*)

Nikisema ninajibu kwa niaba ya Serikali hapa kwamba, unajua Wanawake wawekeni pembeni msiwachukue na nini nitakuwa sieleweki. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anasifika kwa kuwapa Wanawake nafasi nyingi katika Serikali hii, ndiyo sifa yake kubwa sana na sote tunafahamu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi niseme hapa kwamba, kwa kuwa hili ni jambo la kutafakari na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani anasema kubaguliwa, wapo wengine ambao wanawaingiza. Sasa tutakwenda kuangalia hiyo busara ambayo inaruhusu hao wengine waingie kule na wengine wabaguliwe, yote kwa pamoja tutayatafakari kama nilivyosema, tutaangalia kwa pamoja.

**SPIKA:** Ninaona Waziri anataka kuongea, maana hayo matatizo yako chini yake.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri. Bodi za Barabara za Mikoani zinatawaliwa na Sheria Na. 13 ya Mwaka 2007, ambayo ndiyo inazungumzia juu ya *Road Act*. Wajumbe wote wa Bodi ya Barabara huwa wanateuliwa na Waziri wa Ujenzi. Ninataka kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge aliyeuliza swali kwamba, Wajumbe wote wanaoleta majina wakiwemo Wabunge Wanawake, huwa ninawateua kwa ajili ya kuwa Wajumbe wa Bodi ya Barabara. Kwa hiyo, hiyo Sheria haibagui na tutaendelea kuwateua Wabunge wote wanaopendekezwa kutoka Mikoani kwa ajili ya kuhudhuria katika Bodi za Barabara kwa mujibu wa Sheria Na. 13 ya Mwaka 2007. (*Makofi*)

Na. 62

### **Muda wa Taratibu za Kusajili Vijiji Hadi Kukamilika**

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU** aliuliza:-

- (a) Je, utaratibu wa kusajili vijiji huchukua muda gani hadi kukamilika?
- (b) Je, ni sababu zipi zinazosababisha kuchelewa kwa usajili wa Vijiji vya Kinyumbi, Chumo B, Ndende na Nandembo ambavyo viliombewa usajili kwa zaidi ya miaka ishirini iliyopita?
- (c) Ni nini ahadi ya Serikali juu ya utekelezaji wa usajili wa vijiji hivyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ninapenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, hakuna muda maalum uliowekwa wa kukamilisha kusajili vijiji, bali hutegemea kukamilika kwa taratibu za kisheria zinazohitajika ili vijiji viweze kusajiliwa. Taratibu zinazopaswa kufuatwa katika kusajili kijiji ni kama ifuatavyo:-

- (i) Pendekezo la kusajili kijiji/vijiji hujadiliwa na kupata ridhaa ya vikao vya kisheria (Mkutano Mkuu wa Kijiji, Baraza la Madiwani la Halmashauri na Kamati ya Ushauri ya Wilaya – *DCC*).
- (ii) Maombi ya kusajili vijiji huwasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na Mkurugenzi wa Halmashauri, ambaye ni Msajili wa Vijiji Msaidizi. Maombi huchambuliwa ili kuona kama

taratibu na vigezo vimezingatiwa. Baada ya hapo, mapendekezo yaliyoidhinishwa hutangazwa na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa katika Gazeti la Serikali (*Government Notice*).

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Namba 205 la tarehe 26 Juni, 2009, Chumo B ni Kitongoji katika Kijiji cha Chumo kilichosajiliwa tarehe 10 Septemba, 1975 kwa Namba LD/KIJ/67, Ndende ni Kitongoji katika kijiji cha Mitole Kata ya Mitole kilichosajiliwa kwa Namba LD/KIJ/34 tarehe 10 Septemba, 1975. Aidha, hakuna Kijiji cha Kinyumbi bali kuna Kijiji cha Kinjumbi Kihema kilichopo Kata ya Kinyumbi na ambacho kimesajiliwa kwa Namba LD/KIJ/29 tarehe 20 Septemba, 1975. Kijiji cha Nandembe kilichopo katika Kata ya Kipatimu kimesajiliwa tarehe 18 Aprili, 1979 kwa namba ya usajili LD/KIJ/318.

(c) Mheshimiwa Spika, kimsingi, Serikali ilikwishatekeleza wajibu wake wa kusajili Vijiji vya Kinjumbi, Kihema na Nandembo kama ilivyoelezwa kwenye sehemu (b) ya jibu la msingi.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Inawezekana ikawa majibu ya Waziri yanaridhisha, lakini ninaomba numwulize maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Takwimu ambazo amezitoa hapa, anazungumzia ya juu kabisa ni ya mwaka 1979 na ni kweli kabisa sehemu alizozitaja zilikuwa na hadhi ya vitongoji kwa wakati huo. Ningependa Waziri aniambie kama yuko tayari kuweza kusimamia maombi hayo ambayo yameletwa na watu wa vitongoji kwa taratibu ambazo zimeelekezwa na wamefuata majibu mpaka leo majibu hayajapatikana kwa kipindi cha miaka zaidi ya 20?

Mheshimiwa Spika, ningependa pia Mheshimiwa Waziri anihakikishie kama yuko tayari; aidha yeye au wataalamu wake; kufika katika maeneo ambapo anazungumzia takwimu za miaka ya sabini kipindi ambacho hata idadi ya watu Tanzania nzima ilikuwa chini ya milioni kumi na sasa tuna zaidi ya milioni 40? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Murtaza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Vitongoji hivi vinavyotajwa hapa kama kuna maombi yake yameletwa, mimi ninazungumza hapa habari ya *records*, nimeitisha majina ya vijiji vyote vya Tanzania, nikaangalia mle ndani tukaona kwamba, hicho kinachozungumzwa hapa ni vitongoji na vitongoji hivyo vimetamkwa katika vijiji nilivyovisema hapa. Sasa kama Mheshimiwa Mbunge anasema kwamba, vitongoji hivyo vilifika mahali vikaombewa vijiji, *no problem*; mimi ninasema kwamba, tuko tayari sisi kwenda kuangalia hilo ili tuweze kusajili. Hizo ndiyo kazi zetu.

Mheshimiwa Spika, pili, ananiambia kwamba, ninazungumza habari ya miaka ya 70; mimi ninaangalia mambo kihistoria. *When you look at things in a sort of perspective, you are trying to be scientific* na ndicho ninachofanya hapa. Mimi ninasema *records* zetu zilivyo, hivyo vijiji nilivyovitaja kama vilianzishwa mwaka 1979, nikasema mwaka 1990 si mtanishangaa humu ndani! Kwa hiyo, ninachosema hapa; kama Mheshimiwa Mbunge ana *records* ambazo ni tofauti na hizi tulizonazo, ofisi hii ipo kwa ajili ya kazi hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Murtaza aje wakati nitakapokwenda kupiga ile simu ninayosema huko huko twende tukamalizane pia na hii habari anayoizungumza hapa. *(Makofi)*

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza. Mimi ninaitwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini. Kwa vile swali Na. 62 linafanana kabisa na mambo yaliyoko kwenye Jimbo langu la Nkasi Kusini ambapo Vijiji vya Nkata, Kijiji cha Nkata kilichoko Kata ya Kate, Kitongoji cha Kasapa kilichoko Kata ya Simtali na Kitongoji cha Lolesha pamoja na Kasanga vilivyopo Mwambao wa Ziwa Tanganyika pia havijapata usajili licha ya maombi ya muda mrefu. Je, Serikali inatoa matumaini gani kwa Wananchi hawa ambao wamekuwa wakisubiri ili kuendeleza maendeleo yanayohusu vijiji vyao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza, niseme tu kwamba, siyo kila wakati utakapokuwa umeomba vijiji visajiliwe vitasajiliwa. Ukiomba vijiji visajiliwe tutatuma watu kutoka hapa Dodoma watakwenda mpaka kule kwenda kuangalia kama vile vijiji kweli vinafaa kusajiliwa au havifai na tutaangalia vigezo vilivyopo pale ndivyo tunavyoangalia.

Mheshimiwa Spika, ninataka niseme mbele ya Baraza hili kwamba, kama kuna kitu ambacho kimefanyika kwa uangalifu mkubwa sana kwa kipindi kilichopita, ilikuwa ni usajili wa Kata hizi pamoja na vijiji vinavyozungumzwa hapa. Usajili ulifanyika na orodha ikaletwa hapa Bungeni, Wabunge wakapewa wakaambiwa wa-*cross check*, waangalie mle ndani kama kuna mahali popote ambapo kuna kitu kimedondoka wafanye hivyo. Baadaye tukatengeneza orodha nyingine ya vijiji ambavyo tumesema kwamba, hii itakuja na watafanya *by-election* kwa ajili ya kuchagua Wenyeviti wa hivyo vijiji.

Kwa hiyo, mimi ninamkaribisha Mheshimiwa Mbunge, aje pale Ofisini, kama kuna vijiji ambavyo vimedondoka na ambavyo kweli vinaonekana kwamba vinakidhi haya masharti ambayo tunayazungumza hapa, Ofisi ya Waziri Mkuu haina tatizo na hilo. Kupeleka vijiji kule maana yake ni kupeleka huduma zaidi kwa Wananchi, maana yake ni kuleta maendeleo kwa haraka zaidi, ambayo ndiyo *objective* ya kuwepo kwa Serikali yetu hii. Kwa hiyo, hatuwezi kuzuia kabisa kusajiliwa kwa vijiji kama vinakidhi haja hiyo. *(Makofi)*

Na. 63

**Hitaji la Kulinusuru Ziwa Tanganyika Lisitoweke**

**MHE. ALLY K. MOHAMED** aliuliza:-

Ziwa Tanganyika linapungua kwa kasi kubwa sana:-

- (a) Ni sababu zipi zilizosababisha hali hiyo?
- (b) Je, Serikali itachukua hatua gani za haraka za kulinusuru Ziwa hilo lisitoweke?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdul Mteketa, Mbunge wa Kilombero, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Abdul Mteketa kuwa, katika maeneo mengi nchini, kumekuwepo na kasi kubwa ya uharibifu wa mazingira hususan vyanzo vya maji na hivyo kusababisha upotevu.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, taarifa; Mheshimiwa Waziri anajibu swali ambalo hajaulizwa.

**SPIKA:** Hata mimi ninashangaa Mheshimiwa Mteketa ni nani hapa. Hili ni swali Na. 63 la Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Swali namba ngapi?

**SPIKA:** Na. 63 linaulizwa na Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, Mbunge wa Nkasi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Samahani, Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Nikawa ninashangaa Mteketa tena; amebadilisha wapi sasa! (*Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Ninaona kuna matatizo, sikupangiwa sawasawa maswali.

**SPIKA:** Wewe jibu tu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-



(a) Mheshimiwa Spika, utafiti kuhusu kushuka na kupanda kwa kina cha maji cha Ziwa Tanganyika sehemu ya Kigoma uliofanyika kati ya mwaka 1995 hadi 2010 na kwenye Bandari ya Bujumbura huko Burundi kuanzia mwaka 1929 hadi 1999, matokeo yanaonesha kuwa, Ziwa Tanganyika hupungua kiasi cha mita moja katika kipindi cha miaka kumi. Sababu za kupungua kwa kina cha maji ni pamoja na hizi zifuazo:-

- (i) Kupungua kwa mvua: Takwimu za mvua kuanzia mwaka 1929 zimeonesha kuwa, zimekuwa zikipungua na kuongezeka hususan mwaka 1962 zilipoongezeka sana hadi kufikia mm 3,000 kwa mwaka na wakati wa *El-Nino* mwaka 1998 zikafikia kiasi kama hicho. Wingi wa mvua huongeza kina cha maji. Miaka mingine mvua zimekuwa kidogo zikiwa kwenye wastani wa mm 1,200.
- (ii) Mabadiliko ya tabianchi: Tafiti pia zimeonesha kuwa, Ziwa Tanganyika limeongezeka joto kwa kiasi cha nyuzi joto *1.0 centigrade* katika kipindi cha miaka 40 iliyopita na hivyo kuongeza kasi ya myeyuko wa maji (*evaporation rates*). Hata hivyo, tafiti zaidi za kikanda zinatakiwa kufanyika ili kuthibitisha jambo hili.
- (iii) Kuongezeka kwa tope ziwani: Utafiti uliofanyika mwaka 1997 umeonesha kuwa, Mto Malagarasi pekee uliingiza tabaki Ziwani kiasi cha tani mbili hadi tatu kwa sekunde kutegemea kiasi cha mvua kutokana na mmomonyoko wa udongo. Hivyo, wingi wa tabaki hizo unaendelea kupunguza kina cha Ziwa pia na kusababisha mazalia ya samaki kuharibika na pia kupunguza ubora wa maji na kuathiri meli zisiweze kutia nanga katika Bandari ya Kigoma.

- (b) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua tatizo hilo, imechukua hatua mbalimbali ambazo ni pamoja na uanzishwaji wa Programu Endelevu ya Kuhifadhi Mazingira ya Bonde la Ziwa Tanganyika. Programu hii ni ya Kikanda, inayoshirikisha Nchi ya Tanzania, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Zambia. Chini ya Programu hii, kwa upande wa Tanzania, Miradi mitatu inatekelezwa ambayo ni Mradi wa Usimamizi wa Bonde (*Catchment Management*); Mradi wa Usimamizi wa Majitaka katika Manispaa ya Kigoma/Ujiji; na Mradi wa Uendelezaji wa Uvuvi na Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Tanganyika.

Programu hii ni ya miaka minne na utekelezaji wake umeanza Septemba 2008 katika Mikoa ya Kigoma na Rukwa katika Wilaya za Kigoma Vijijini, Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Kasulu, Mpanda, Nkasi na Sumbawanga Vijijini. Programu hii inatekelezwa na kushirikisha Watendaji wa Hlamshauri pamoja na Wananchi, ili muda wa Mradi utakapoisha, Halmashauri ziendeele kutekeleza

shughuli za hifadhi ya mazingira katika Bonde la Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2008, Serikali iliandaa mkakati wa hatua za haraka za kuhifadhi mazingira ya bahari, maziwa, mabwawa na mito, kwa lengo la kuboresha na kuhifadhi maeneo hayo na hatimaye kuinua hali ya kipato na maisha ya Wananchi kwa ujumla kupitia bioanuai na rasilimali zake. Mkakati huu umeanza kutekelezwa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, sasa hivi Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu kwamba, maji yanayoingia Ziwa Tanganyika kupitia Mto Malagarasi yote yanatoka Mto Kongo na kwenda Bahari ya Atlantic. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuzungumza na Serikali ya DRC Kongo maana nayo inahusika na upunguaji wa Ziwa Tanganyika ili Mto Malagarasi kwa upande wa Kongo upunguze maji kwenda *Atlantic Ocean*?

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi ...

**SPIKA:** Kwa niaba ya Serikali.

**WAZIRI WA MAJI:** Kwa niaba ya Serikali, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, kama ifuatavyo:-

Upande wa Kongo kama ilivyo Maziwa ya Bonde la Ufa ni Mto mmoja tu unaotoa maji kutoka Ziwa Tanganyika na Mto huo unaitwa Mto Lukuga, ambao unaingiza maji katika Bonde la Mto Kongo. Kwa bahati mbaya, kutokana na matatizo ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo hasa upande huu wa Mashariki, kidhibiti maji yanayotoka katika Ziwa Tanganyika ambacho kiliwekwa na Wabelgiji enzi za Wakoloni, hakifanyi kazi tena kimeharibika. Kwa hiyo, maji yanatoka katika Ziwa Tanganyika kwenda katika Bonde la Kongo Mto Kongo bila udhibiti wowote na ni maji mengi na inasemekana huenda hali hii ikachangia pia katika kupungua kwa kina cha Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Rais alinituma kwenda Kongo mwaka jana kupeleka ujumbe kwa Mheshimiwa Kabila kuhusu suala hili na suala zima la kushuka kwa kina cha Ziwa Tanganyika na matokeo yake ni kwamba; tumekubaliana kwamba, kwa maana ya kudhibiti maji yanayotoka Ziwa Tanganyika kupitia Mto Lukuba, basi tufanye ushirikiano sisi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, kutengeneza kile kidhibiti maji ili kudhibiti maji yanayotoka Ziwa Tanganyika kwenda Kongo. Ahsante.

Na. 64

### **Uharibifu wa Vyanzo vya Maji**

**MHE. ABDUL R. MTEKETA** aliuliza:-

Jimbo la Kilombero lilikuwa na mito sabini na tisa, lakini hivi sasa mito hiyo imeharibiwa na kubakia thelathini na tisa tu:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuchukua hatua za haraka za kutunza vyanzo vya maji na vivutio mbalimbali vya asili katika Jimbo la Kilombero?
- (b) Je, Serikali ilichukua hatua gani za makusudi za kuzuia uharibifu huo, pamoja na utoaji wa elimu ya mazingira?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA)**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba, mimi siyo Naibu Waziri, mimi ni Waziri kamili wa Nchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, fanya hiyo kazi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):**  
Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdul Mteketa, Mbunge wa Kilombero, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Abdul Mteketa kuwa, katika maeneo mengi nchini, kumekuwepo na kasi kubwa ya uharibifu wa mazingira hususan vyanzo vya maji na hivyo kusababisha upotevu wa mabwawa, mito na chemchemi. Ili kudhibiti uharibifu huu, Serikali iliamua kuchukua hatua za haraka ambapo mwezi Machi, 2006 ilipitisha mkakati wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji.

Mkakati uliwataka wafugaji na wakulima waliovamia maeneo yasiyoruhusiwa kisheria ikiwa ni pamoja na maeneo ya ardhi oevu ya Kilombero, waondoke katika maeneo hayo. Ninapenda kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa, katika kutekeleza azma hii, kufikia mwaka 2010, jumla ya ng'ombe 16,241, mbuzi 1,432 na kondoo 1,445 waliokuwa wamevamia Bonde la Kilombero waliondolewa. Aidha, mwaka 2008, Serikali iliandaa mkakati na hatua za haraka za kuhifadhi mazingira ya bahari, maziwa, mabwawa na mito, kwa lengo la kuboresha mazingira katika sehemu hizo ambazo ni chepechepe, pia ni muhimu kwa kuongeza uzalishaji wa umeme utokanao na maji na kulinda au kuhifadhi bioanuai na rasilimali zake na hatimaye kuinua hali ya kipato na maisha ya Wananchi kwa ujumla. Mkakati huu umeanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa uharibifu wa mazingira unaotokana pia na uelewa mdogo katika masuala ya usimamizi wa mazingira, mkakati wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji ulielekeza kuandaliwa kwa Programu ya Taifa ya Elimu kwa Umma na tayari Programu hii imeshaandaliwa na imeanza kutekelezwa. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais na wadau wengine, wameendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu kuhifadhi mazingira kwa kupitia njia mbalimbali, kwa mfano, vipindi vya redio, televisheni, magazeti, majarida, vipeperushi, machapisho na Maonesho mbalimbali

ya Kitaifa kama Nanenane na Sabasaba, Siku za Mazingira Duniani, Siku za Mazingira Afrika na kadhalika. Vilevile, Wilaya mbalimbali ikiwemo Wilaya ya Kilombero, zimeandaa Sheria ndogo ambazo pamoja na mambo mengine, suala la usimamizi wa mazingira limezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza hamasa kwa jamii katika utunzaji wa mazingira, Ofisi ya Makamu wa Rais, imeanza kutoa Tuzo ya Rais ya Kutunza Vyanzo vya Maji, kupanda na kutunza miti. Tuzo inatarajiwa kuongeza ufahamu wa Wananchi katika umuhimu wa utunzaji wa mazingira, ikiwa ni pamoja na Wananchi wanaoishi katika Bonde la Mto Kilombero. Tuzo hii imetolewa kwa mara ya kwanza mwaka 2010 katika Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, tarehe 5 mwezi Juni. Tuzo hii itakuwa inatolewa mara moja kila baada ya miaka miwili.

Mheshimiwa Mbunge akiwa ni mdau wa usimamizi wa mazingira, ninapenda kuchukua nafasi hii, kumwomba aendelee kuihamasisha jamii kushiriki kikamilifu katika mashindano haya. Aidha, kwa kuwa usimamizi wa mazingira ni jukumu la kila mmoja katika jamii, ninapenda kumwomba Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote mliopo hapa ndani, mshirikiane na Waheshimiwa Madiwani pamoja na Uongozi wa Wilaya ya Kilombero katika ngazi zote nchini, kuhamasisha na kuelimisha Wananchi wote kwa ujumla kuhusu faida za kiuchumi na kijamii zitokanazo na utunzaji wa mazingira hususan upandaji wa miti inayofaa katika mazingira husika kwa faida yetu na ya vizazi vijavyo.

**MHE. ABDUL R. MTEKETA:** Ahsante sana Mheshimiwa ...

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Mtekela.

**MHE. ABDUL R. MTEKETA:** Jina langu kamili ni Abdul Rajab Mteketa, siyo Mtekela.

**SPIKA:** Mteketa.

**MHE. ABDUL R. MTEKETA:** Ninashukuru kwa majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri; nina swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Pamoja na Serikali kuchukua hatua ya pamoja na Halmashauri kutunga Sheria za Kuhifadhi Mazingira; je, hawaoni hali imebaki pale pale haijabadilika?

(ii) Kwa nini Serikali isitenge fedha ili kudhibiti suala hili?

**SPIKA:** Kudhibiti suala gani tena?

**MHE. ABDUL R. MTEKETA:** Basi, maswali mawili tu.

**SPIKA:** Haya ahsante. Kama huna swali la nyongeza siyo lazima usimame. Haya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali imetunga Sheria na Halmashauri pia imetunga Sheria ndogo ndogo ili kuhifadhi mazingira. Kama nilivyojibu kwenye jibu langu la awali kwamba, uelewa wa Wananchi ni mdogo. Mimi ninaamini kuwa, kama sisi Wabunge wote hapa ndani tutashirikiana kwa pamoja na Madiwani na Halmashauri tulizonazo kule kwa sababu majimbo yote yapo hapa ndani, jambo hili litatekelezeka. Siamini kama Ofisi ya Makamu wa Rais tu ndiyo yenye wajibu wa kusimamia Sheria. Sheria hizi tunazitunga sisi hapa Bungeni; kwa hiyo, sisi sote hapa tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba, zinatekelezeka. *(Makofi)*

Swali la pili, ni kwa nini Serikali isitenge fedha; Serikali mara zote inatenga fedha. Mimi ninaamini kuwa, utunzaji wa mazingira ni ari ya mtu binafsi toka rohani; ni kama vile mtu anajenga nyumba lakini hasafishi, hafagii, anangoja Serikali ikamsafishie. Kwa hiyo, ninaomba sote kwa pamoja tusaaidiane kuwaelimisha Wananchi wawe na ari na moyo wa kutunza mazingira katika sehemu tunazoishi. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii nami niulize swali la nyongeza. Nikiwa mdau wa Wilaya ya Kilombero, ninaomba kumwuliza swali la nyongeza Mheshimiwa Waziri kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa katika Jimbo la Kilombero pamoja na suala zima la uharibifu wa mazingira, tatizo kubwa sana lililopo katika Kata ya Mgeta ni kwamba mwekezaji kanyunyizia dawa katika mashamba yake; na kwa kuwa dawa hizo zinaathiri sana wakulima walioko katika Kata hiyo; na kwa kuwa matokeo yake mpaka hivi sasa mazao waliyolima yote yamekauka; na kwa kuwa Wananchi wakiwemo Watoto wanaathirika sana kutokana na yale madawa; na kwa kuwa iliundwa Kamati kufuatilia Wananchi pale na walipeleka malalamiko yao mpaka Wilayani, Mkoani na Ofisi ya Waziri Mkuu; na kwa kuwa ilikwenda Kamati Maalum ya Wizara ya Kilimo lakini mpaka sasa hakuna suala lolote lililochukuliwa hatua; je, Waziri haoni kwamba sasa ni wakati wa kwenda Mgeta kuangalia suala hili ili kuwanusuru Wananchi wa Wilaya ya Kilombero hususan Kata ya Mgeta?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, ...

**SPIKA:** Sema kwa kifupi kwa sababu ni swali la nyongeza hilo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, swali ulilouliza lina mwingiliano kwa sababu kuna suala la uwekezaji wakati huo huo kuna suala la kutunza mazingira; lakini ninapenda kusema hivi, wewe unapowekeza usipende kuudhi watu wengine hasa wanyonge, kwa sababu unapowekeza inabidi mtu achukue tahadhari kwa watu wanaomzunguka. Ninaahidi kwamba, nitakuja Mgeta niangalie huo uharibifu wa mazingira uko kiasi gani ili tujue njia gani tutachukua za kumshauri huyo mwekezaji asiharibu afya za watu wengine.

**Askari wa TANAPA – Serengeti kunyanyasa Wananchi**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza:-

Askari wa TANAPA katika Mbuga ya Serengeti wamekuwa wakiwanyanyasa Wananchi wa Vijiji vya Mangucha, Masanga na Gibaso kwa kuwaua na mifugo yao kuchukuliwa na familia za wahusika kutakiwa kulipa fidia ya mifugo hiyo tofauti na ilivyo kwenye maeneo mengine yanayopakana na Hifadhi za Taifa kama Manyara na Arusha:-

(a) Je, kwa nini wafugaji wa vijiji hivyo wananyanyaswa na Askari wa TANAPA; na Sheria inasema nini juu ya hali hiyo?

(b) Je, ni nini hatma ya wakazi sita wa Kijiji cha Gibaso waliopotea mwaka jana katika mazingira ya kutatanisha?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu haijapata taarifa zenye ushahidi kuwa, Wananchi kwenye Vijiji vya Mangucha, Masanga na Gibaso wananyanyaswa. Kwa kawaida, inapotokea kuwa mtu mmoja au baadhi ya Wananchi kukutwa ndani ya hifadhi kwa shughuli zao binafsi, ikiwa ni pamoja na ujangili, uchungaji wa mifugo au shughuli nyingine yoyote, hatua mbalimbali za kisheria zimekuwa zikichukuliwa juu yao ikiwa ni pamoja na utozaji wa faini kwa mujibu wa Sheria ya Hifadhi ya Taifa, Sura ya 282, Toleo la Mwaka 2002, Kifungu cha 28, kikisomwa kwa pamoja na Sheria Namba 11 ya Mwaka 2003, ambayo inarekebisha Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura ya 412. Aidha, Sheria ya Hifadhi za Taifa, inaruhusu kumtoza faini isiyozidi shilingi 100,000 mtu anayefanya kosa dogo, kwa kila kosa analokiri.

Mheshimiwa Spika, kila mfugo unaokutwa ndani ya Hifadhi unachukuliwa kwamba ni kosa moja. Hata hivyo, kwa sasa Hifadhi za Taifa, Serengeti, imekuwa ikitoza 5,000 kwa mfugo.

(b) Mheshimiwa Spika, taarifa kuhusu wakazi sita wa Kijiji cha Gibaso, wanaoripotiwa kupotea katika mazingira ya kutatanisha katika Hifadhi ya Serengeti, zilitufikia mapema mwezi Novemba mwaka jana na taarifa hizo zikawa zimeripotiwa Jeshi la Polisi, Kanda Maalum ya Rorya. Shughuli za kuwatafuta watu wale zimekuwa zikiendelea toka wakati huo, zikifanywa na Jeshi la Polisi. Kwa upande wetu, tumekuwa tukitoa ushirikiano, lakini mpaka sasa hivi hatujapata taarifa zozote za kuonekana kwao.

**MHE. ESTHER NICHOLAS MATIKO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza hasa katika kipengele (b) kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa kila Raia wa Tanzania ana haki ya kuishi; na kwa kuwa upoteaji wa Vijana Ng'eng'e Magarya, Maro Sila, Chacha Marwa Mwita Marwa Museti na Tore Chiwala, uliotokea tarehe 31 Oktoba, 2010 ulitokana na Askari wa *TANAPA* waliokuwa katika doria kuwafukuza na kulisikika milio ya bunduki: Je, Serikali inaweza kuwaambia Watanzania na hasa wazazi wa vijana hawa nini hatma ya vijana hao ambao mpaka sasa wazazi wao wapo *desperate* hawajui hatma ya watoto wao kwa sababu majibu wa Mheshimiwa Waziri yanaeleza kwamba upelelezi bado unaendelea na sasa ni takriban miezi sita?

(ii) Kwa kuwa katika siku ya tukio kuna vijana wawili walinusurika na wakabahatika kurudi majumbani kwao na inasemekana Askari wa *TANAPA* wakiitishwa *parade* wanaweza wakawatambua baadhi ya askari waliokuwepo; na kwa kuwa inasemekana pia kwamba gari lililokuwa doria lilitokea katika Kituo cha Kenyanganga na Namahiya; je, Wizara ya Mambo ya Ndani haioni kwamba itakuwa ni busara katika kuharakisha upelelezi huu kuitisha *parade* kwa kushirikiana na hao vijana walionusurika ili tuweze kujua hatma ya hawa vijana wetu sita?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, niseme kwamba, katika miaka ya karibuni, kumekuwepo na matukio mengi ya watu wema na wabaya, kuingia hifadhini bila utaratibu. Matukio haya inakuwa siyo rahisi kwa Wizara yangu kuweza kuchukua dhamana. Mwezi wa kwanza mwaka huu, kulitokea tukio la wawindaji wa kitalii kushambuliwa kwenye Hifadhi ya *Maswa Game Reserve* na watu ambao waliua mtu mmoja na kukimbia. Watu ambao haikufahamika kama ni majangili au laah.

Mheshimiwa Spika, kwa mazingira kama haya, inakuwa ni vigumu kuweza kusema kwamba, anapoingia mtu kwenye hifadhi bila kujua ameingia saa ngapi na anakutana na nani, siyo rahisi kuweza kujua na kuchukua dhamana kwamba, Askari wa Wanyamapori au Askari wa Mamlaka wanaweza wakaeleza. Kwa hiyo, niseme tu kwamba, kwa sasa hivi Jeshi la Polisi baada ya kuwa limetaarifiwa, linafanya kazi yake.

Mheshimiwa Spika, jibu hili linajibu pia swali la pili ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliuliza; ni kwamba, Polisi wana taratibu zao; waliwaita Askari wa *TANAPA* tarehe 23 Novemba, wakawahoji kwa utaratibu ambao wao taratibu zao za kazi zinawataka wafanye na mpaka sasa hivi uchunguzi bado unaendelea.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninamwomba Mheshimiwa Mbunge kwamba, tuwaache Polisi wafanye kazi yao na sisi kwa upande wetu kama Wizara,

nimeshawaelekeza *TANAPA* watoe ushirikiano kwa Polisi, wasimwogope mtu yeyote ambaye anaonekana au anahisiwa kwamba anaweza kusaidia ahojiwe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Max, swali la nyongeza; ni Max wewe? Siyo Max? Hivi mnakaa mahali penu maana mnachanganya; wewe uliyesimama nyuma kabisa unaitwa nani?

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, mimi naitwa Dokta Kebwe Stephen Kebwe, Mbunge wa Jimbo la Serengeti.

**SPIKA:** Watu hawakai mahali pao, sasa inakuwa ni kazi kwa Spika.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, nipo sehemu hii siku zote. Kwa kuwa swali namba 65 la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, linafanana kabisa na mazingira ya Wilaya ya Serengeti; na ukitilia maanani Wilaya ya Serengeti yenye mbuga kubwa kuliko zote Duniani, 70% ni Hifadhi ya Serengeti katika Wilaya ya Serengeti na mapori mawili ya akiba jumla inakuwa 94%. Adha hizi na migororo ya namna hii ni mikubwa Serengeti kuliko sehemu zote katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, katika Kata tisa ambazo zipo jirani zikiwemo Nyasurura, Machochwe, Baribari, Sedeko, Ikoma na hata Isenye, Manchira na Kyambahi, upo mgogoro mkubwa wa ardhi kati ya hifadhi na wanavijiji; ni lini Wizara ya Maliasili wataangalia upya mipaka kupunguza migogoro hii?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dokta Kebwe, Mbunge wa Serengeti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba, maeneo yaliyo mengi ambayo yapo nje ya hifadhi kwa hivi sasa yamekaliwa na watu na kwa maana hiyo, hakuna *buffer zone*, yaani eneo la wazi linalotenga au kuinga hifadhi; na hii imesababisha migogoro mingi.

Kupitia Sheria Namba 5 ya Mwaka 2009, tumeelekeza kwamba, Wizara itapitia upya mipaka ya hifadhi, lakini mipaka ya hifadhi inayozunguka Hifadhi za Taifa ambazo zinatawaliwa na Sheria nyingine, tumekwihawaelekeza *TANAPA* kwamba, wapitie upya mipaka yao, waweke alama zinazoonekana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, zoezi hili linakuwa halina mafanikio sana kwa sababu kuna maeneo mengine ambayo mipaka ipo wazi, isipokuwa hakuna eneo la wazi kati ya mpaka wa hifadhi na makazi ya watu. Kwa hiyo, kwenye mazingira kama hayo, tunatafuta namna nyingine ambayo inaweza ikasaidia kupunguza migogoro lakini mipaka inapitiwa upya.



## Utaratibu Mpya wa Ugawaji wa Vitalu

**MHE. ALI KHAMISI SEIF** aliuliza:-

Serikali iliahidi kuanzisha utaratibu mpya wa ugawaji wa vitalu. Je, utaratibu huo umefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mchakato wa ugawaji wa vitalu katika kipindi cha mwaka 2013 hadi 2018 umeanza na Wizara yangu imetangaza vitalu 156 vilivyo wazi kwenye Magazeti ya Uhuru, Majira, Habari Leo, *The Guardian* na *Daily News* ya tarehe 10 Februari 2011. Katika tangazo hilo, waombaji walifahamishwa utaratibu unaotakiwa kuzingatiwa katika kuwasilisha maombi yao. Aidha, tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ya vitalu ilikuwa ni tarehe 12 Machi, 2011 ikiwa ni siku 30 tangu tangazo lilipotolewa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maombi hayo kupokelewa, Wizara yangu inaendelea na kufanya tathmini ya waombaji, kubaini uwezo wao wa kuendesha biashara ya uwindaji wa kitalii. Hivyo, matokeo rasmi ya shughuli hii, yataweza kutangazwa baada ya siku 60 kwa mujibu wa Kanuni za Sheria ya Uwindaji wa Kitalii.

**MHE. ALI KHAMISI SEIF:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, lengo moja la MKUKUTA ni kuwawezesha Wananchi katika suala zima la uchumi. Je, Serikali ina mpango gani kwa Watanzania ambao watahitaji vitalu hivyo wapewe upendeleo maalum?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ali Khamis Seif, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kupitia Sheria Namba 5 ya Mwaka 2009, Sheria iliweka vigezo ambavyo vinatakiwa vizingatiwe na makampuni yanayofanya biashara hii. Mojawapo ni kuzungumzia suala la umiliki wa hisa kwamba, makampuni ya uwindaji wa kitalii yawe na hisa kwa Tanzania isiyopungua 25%, hiyo ni mojawapo. La pili ni kwamba, kwenye vigezo ambavyo tumeviweka kwa ajili ya kuwafanyia tathmini waombaji, vigezo kwa ajili ya waombaji wenyeji ni tofauti na vile vya waombaji wageni.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kama nilivyosema kwamba, kwa sasa hivi zoezi limeshakamilika kwa maana ya kutangaza, muda wa kupokea maombi ulikuwa ni tarehe 12 Machi, 2011 na umeshapita.

Kwa hiyo, sasa hivi tunaendelea na zoezi la kugawa kwa wale walioomba na maombi ya Watanzania wanyonge yatazingatiwa kwa mujibu wa Kanuni na taratibu ambazo tuliziweka kwenye Tangazo pia.

Na. 67

### **Askari wa Jeshi la Polisi**

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA** aliuliza:-

- (a) Je, ni Askari wangapi wa Jeshi la Polisi wamestaafu kuanzia mwaka 2007 – 2010?
- (b) Je, kati ya hao ni wangapi wameshalipwa mafao yao kutoka Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa *Al-Khabibi* Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Askari wa Jeshi la Polisi waliostaafu katika kipindi hicho cha miaka minne ni 1,857 katika mchanganuo ufuatao:-

2007	–	Askari	–	493
2008	–	Askari	–	428
2009	–	Askari	–	480
2010	–	Askari	–	456

(b) Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2011 askari 1,805 kati ya 1,857 waliostaafu, walishalipwa mafao yao Tanzania nzima. Kati ya idadi hiyo, Askari 1,562 wanatoka Tanzania Bara na 243 ni kutoka Zanzibar. Askari 52 bado hawajalipwa mafao yao, kati yao 34 ni wa Tanzania Bara na 18 ni wa Zanzibar.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimwia Naibu Waziri, *Al-Muhtaram*, nina maswali mawili madogo ya kumwuliza:-

(i) Kwa kuwa sababu zinazofanya malipo ya Askari kuchelewa ni ndogo ndogo sana kama vile *NSSF* na mambo mengine; haoni sasa ni wakati muafaka kama alivyosema Mheshimiwa Waziri hapa wakati akijibu swali katika Bunge lililopita kuwa wanaohusika katika makato haya madogo madogo wayaharakishe ili kupunguza usumbufu kama huu?

(ii) Je, hawa wachache waliobakia ni lini watakuwa wameshalipwa mafao yao ambapo mara nyingi kila wakibakia wachache inakuwa ni ngumu sana kulipwa kwa sababu lile kundi kubwa limeondoka?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Khalifa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni sahihi kwamba, yapo haya mambo madogo madogo ambayo yamekuwa yakileta ucheleweshaji katika malipo. Ninaomba nimhakikishie kwamba, *IGP* Mwema, amefanya mabadiliko ndani ya utawala wao na tuna uhakika kabisa kwamba, tangu mwaka jana malipo haya yamekuwa yanakwenda kwa uharaka na ninadhani kasi hiyo ikiendelea, tutakuwa tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, ninaomba nimwambie kwamba, tatizo tulilokuwanalo katika Wizara ni kwamba, wakati hizi fomu au karatasi za madai zinapojazwa, unakuta mara nyingi katika hii idadi ya watu wachache, kunakuwa na makosa. Sasa ni katika kujaribu kusahihisha na ule utaratibu wa nenda rudi, sahihisha hili, tunataka karatasi hii, hapo ndiyo kumekuwepo na matatizo makubwa. Vilevile na hilo tunalitazama na tunajaribu kuliondoa kwa sababu tunajua ni muhimu sana kwa mtu aliyestaafu aweze kupata mafao yake yaweze kumsaidia yeye na hali yake.

Na. 68

### **Ukosefu wa Afisa Ardhi Manispaa ya Kigoma Ujiji**

**MHE. SABREENA H. SUNGURA** aliuliza:-

Manispaa ya Kigoma Ujiji ni moja ya Manispaa maskini nchini yenye wastani wa pato la 360,000 kwa kila mwaka. Ardhi ni mali pekee tegemezi iliyobaki inayoweza kumkomboa Mwananchi huyu na sasa ni zaidi ya miaka miwili Wananchi hawa duni wamekosa Afisa Ardhi:-

(a) Je, Serikali haioni ni vema Manispaa hiyo kupata Afisa Ardhi wa kudumu ili Wananchi waweze kupata haki zao za msingi kama hati miliki na kadhalika?

(b) Je, ni sababu zipi za msingi zinazosababisha tatizo hilo lisipate ufumbuzi kwa muda mrefu sasa?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua kuwa, Manispaa ya Kigoma Ujiji haikuwa na Afisa Ardhi Mteule kwa takriban miaka miwili, kufuatia kuhamishwa kwa aliyekuwa Afisa Ardhi Mteule wa Manispaa hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, sababu za msingi za kutokuwepo kwa Afisa Ardhi kwenye Halmashauri hiyo kwa muda huo ni pamoja na Uongozi wa Halmashauri ya Manispaa kutokuajiri mtumishi mwingine kumbadili yule aliyehamishwa.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mashauriano baina ya Uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji na Wizara yangu, uteuzi wa Afisa Ardhi Mteule, ulifanyika kuanzia tarehe 1 Aprili, 2011.

Mheshimiwa Spika, nafasi ya Afisa Ardhi Mteule katika usimamizi wa matumizi ya ardhi kwenye Halmashauri zetu ni muhimu sana. Kukosekana kwa mtaalamu wa fani hiyo, husababisha usumbufu kwa Wananchi wanaohitaji huduma, hususan za kumilikishwa ardhi. Ili kuepusha usumbufu kwa Wananchi kwa siku zijazo, Serikali inaaagiza Wakurugenzi wa Halmashauri za Miji na Wilaya, wawe wakiwasilisha mapendekezo ya uteuzi Wizarani kwangu, kabla ya Afisa aliyekasimiwa madaraka ya Afisa Ardhi Mteule, Afisa Mipango Miji na Afisa Mpima, kustaafu, kuachishwa kazi au kuhamishwa ili Mamlaka ya Uteuzi ipate muda wa kutosha kufanya uamuzi kwa mujibu wa sheria.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Manispaa ya Halmashauri ya Mji wa Kigoma Ujiji imetenga hekta takribani 3,000 kwa ajili ya *Special Economic Zone*; na kwa kuwa Manispaa hiyo ni moja ya Manispaa zinazofaidika na Mradi wa *World Bank* ujulikanao kama *Tanzania Strategic City Project* ambao umeahidi kujenga dampo, stendi na barabara; je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuiimarisha kada ya Wathamini wa Ardhi katika Manispaa hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Mheshimiwa Mbunge, tumeyapata na tutayazingatia na kuyafanyia kazi ipasavyo. Ahsante.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa tatizo la uhaba wa wataalamu lililopo katika Manispaa ya Kigoma lipo pia katika Wilaya ya Ngala; na kwa kuwa Wananchi wa Ngala wanangojea kwa hamu sana utekelezaji wa Mradi wa MKURABITA, Mradi wa Kurasimisha Mali na Biashara za Wanyonge, lakini Mradi huo hauwezi kutekelezwa kabla ya kupima vijiji; tunavyo vijiji 72 ili Wananchi wapate hati waweze kuomba mikopo ninamwomba Waziri wa Ardhi atoe kauli ni lini Wizara ya Ardhi itapima vijijini hivyo na mashamba ya Wananchi ili waweze kufaidika na Mradi wa MKURABITA?

**SPIKA:** Mbona swali ni jipya; Naibu Waziri sijui unaweza kujibu?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ninaomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina, Mbunge wa Ngala, kama ifuatavyo:-

Serikali imekwishapima karibu asilimia 99 ya vijiji vyote nchini na hapa nilipo, sina takwimu sahihi lakini kwa Wilaya ya Ngala, nina uhakika kwamba, sehemu kubwa ya vijiji vimeshapimwa. Suala la upimaji wa mashamba na kutoa hati miliki za kimila kwa Wananchi wanaomiliki maeneo katika Wilaya hiyo, unafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya Mwaka 1999.

Utaratibu ni baada ya kijiji kupimwa na kupata hati, wanapaswa kuanzisha masjala na daftari la ardhi, wakishatimiza masharti hayo, vijiji sasa vinaweza kuleta mapendekezo ili upimaji wa mashamba yanayomilikiwa na Wananchi kihalali yaweze kufanyika na Wananchi kupatiwa hati.

Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge ashirikiane nasi, kufanya tathmini ya vijiji vingapi vimesajiliwa katika wilaya yake na kama vina hati na kisha awasiliane nasi ili tuweze kutekeleza jukumu hilo la kuwapimia ardhi Wananchi na kuwamilikisha rasmi.

Na. 69

### **Ujenzi wa Barabara ya Tukuyu - Mbambo - Lwangwa - Katumba**

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA** aliuliza:-

Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2010 - 2015 imeainisha kwamba, Barabara ya Tukuyu - Mbambo - Lwangwa - Katumba itajengwa kwa kiwango cha lami:-

(a) Je, Wananchi na Wadau wengine watakaonufaika na barabara hiyo wategeme mpango gani wa utekelezaji wa Mradi huo mwaka hadi mwaka?

(b) Je, Mradi huo umepangwa kukamilika lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. David Homel Mwakyusa, Mbunge wa Jimbo la Rungwe Magharibi, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Barabara ya Tukuyu - Mbambo - Lwangwa - Katumba yenye urefu wa jumla ya km 79.4, inahudumiwa na Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*),

Mkoa wa Mbeya. Mchakato wa kujenga Barabara hii kwa kiwango cha lami, ulianza katika Mwaka wa Fedha wa 2008/2009, kwa kuanzia na usanifu wa kina uliokamilika Mwaka wa Fedha wa 2009/2010.

Baada ya kukamilika usanifu, Serikali imepanga kutekeleza Mradi huu kwa awamu. Katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi milioni 600 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa madaraja mawili, ambayo ni Mwalisi na Mbaka.

Kwa sasa mchakato wa kumpata mkandarasi wa kufanya kazi hiyo unaendelea. Ili kukamilisha ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami, jumla ya shilingi bilioni 83 zinahitajika. Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa barabara hii kutoka vyanzo mbalimbali ili kutekeleza Mradi huu. Tarehe ya kukamilika Mradi huu, itategemea upatikanaji wa fedha.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi niweze kumshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana. Nina swali dogo la nyongeza:-

Hapo barabara niliyouliza kwenye swali la msingi itakapokamilika na kwa kutambua kwamba ujenzi wa barabara ya kutoka Kyela kwenda ufukwe wa Matema kupitia Ipinda unaendelea vizuri; hizi barabara mbili zitakapokamilika zitabaki kilomita kama 20 za barabara kutoka Mbambo kwenda Ipinda. Ninaamini kwamba, Naibu Waziri anaifahamu vizuri. Nilitaka kujua; je, Serikali ina mpango gani wa kuiwekea lami hiyo barabara niliyoitaja ili iwe rahisi kwa watu kusafiri kutoka Tukuyu kwenda *Matema Beach*; ambapo ni kivutio cha utalii?

**SPIKA:** Ahsante. Naibu Waziri majibu na wewe si wa huko huko? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Prof. David Homel Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimeshakwikagua Barabara ya Tukuyu – Mbambo – Lwangwa – Katumba na vilevile kipande kifupi anachokiongelea cha Barabara ya Mbambo kwenda Ipinda, nikiwa nimeongozana na Wahandisi wa *TANROADS* Mkoa wa Mbeya. Ninaomba nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaanza kukihangaikia kipande hiki mara tu baada ya ujenzi wa Barabara ya Tukuyu – Mbambo – Lwangwa – Katumba na Barabara kutoka Kikusya hadi Matema kukamilika kwa kiwango cha lami.

Na. 70

### **Ujenzi wa Barabara za Tabora**

**MHE. SELEMANI J. ZEDI (K.N.Y. MHE. SAID J. NKUMBA)** aliuliza:-

Barabara za Sikonge - Tanga - Ipole - Koga - Mpanda na Ipole - Rungwa zinaunganisha Mkoa wa Tabora na Mikoa ya Kusini kuelekea Kaskazini:-

(a) Je, hatua za upembuzi yakinifu zilizochukua muda mrefu zitaisha lini?

(b) Ni maandalizi gani yanayoandaliwa ya kujenga barabara hizo kwa kiwango cha lami ili kuinua uchumi wa Wananchi wa Sikonge, Mpanda na Tarafa ya Kiwere?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE)**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, unahitaji maandalizi makubwa ambayo ni pamoja na kufanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina, tathmini ya athari kwa mazingira na kutafuta fedha za ujenzi.

Kazi za upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na tathmini ya athari kwa mazingira kwa Barabara ya Tabora - Sikonge - Ipole - Koga – Mpanda, yenye urefu wa km 359, zimeanza mwezi Juni mwaka 2009 na zimepangwa kukamilika mwezi Juni mwaka 2011. Aidha, mchakato wa kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na tathmini ya athari kwa mazingira kwa Barabara ya Ipole – Rungwa, yenye urefu wa kilometa 172 inaendelea na inategemewa kuwa, ifikapo mwezi Juni, 2011, Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi hizi atakuwa amepatikana.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya kazi hizo kukamilika, Serikali itaanza kutafuta fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali la nyongeza. Kwa kuwa kazi hii ya upembuzi yakinifu ya Barabara ya kutoka Sikonge - Tabora inafanana kabisa na kazi ya upembuzi yakinifu ya barabara inayoanzia Tabora kupitia Vijiji vya Mambali, Bukene, Itobo, Mwamala, Igusule na Kahama. Je, Wizara ya Ujenzi inaweza kulihakikishia Bunge hili kwamba katika bajeti ijayo itatenga pesa ili kazi ya upembuzi yakinifu katika barabara hii ya kuanzia Tabora kupitia Mwambali – Bukene – Itobo – Mwamla – Igusule iweze kufanyiwa kazi?

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu watu wasikie.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Barabara na Viwanja vya Ndege, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Selemani Zedi, Mbunge wa Bukene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara kwa sasa iko katika zoezi la utekelezaji wa barabara zote zilizo kwenye Ilani na Ahadi za Rais kwa mpangilio kufuatana na upatikanaji wa fedha na umuhimu wa barabara moja moja kulinganisha na zingine; ninaomba nimshauri Mheshimiwa Zedi, atulee swali rasmi kama alivyofanya Mheshimiwa Nkumba, Mbunge wa Sikonge, kuhusu Barabara hii ya Tabora – Mambali – Bukene – Itobo na Kahama ili tuangalie tuipe kipaumbele gani kati ya Miradi zaidi ya 100 ambayo inasubiri tuitekeleze.

Mheshimiwa Zeddy, akifanya hivyo, atakuwa amewatendea haki zaidi Wananchi wa Bukene.

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa barabara iliyolizwa katika swali la msingi inafanana kabisa na Barabara ya Dumila – Turiani – Mzia na kwa sasa matengenezo ya barabara hii yamesimama; Waziri anaweza kutuambia nini hasa tatizo?

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu maana mnatakiwa mjue barabara zote bila kuulizwa; ni maswali mapya hayo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, ninapenda kumjibu Mheshimiwa Makalla, Mbunge wa Mvomero, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tuseme tu ukweli kwamba, barabara zote nchini zinafanana lakini ingekuwa vema kama Waheshimiwa Wabunge, kwa kila barabara wangeweza kuleta maswali. Kwa barabara hii ya Dumila – Turiani, mimi nimeikagua, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kazi ya ujenzi wa barabara hiyo ilikuwa inasuasua kutokana na uhaba wa fedha uliokuwa umeikumba Serikali kulipa madai ya makandarasi. Nimefurahi leo kumweleza Mheshimiwa Makalla, Mbunge wa Mvomero kuwa, Serikali imeshaipatia fedha Wizara ya Ujenzi na tumeshawasilisha kwa makandarasi. Ninamwomba apitie tena aangalie kazi inayofanyika pale hivi sasa.

Na. 71

### **Gharama za Vifaa vya Ujenzi**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.N.Y. MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAAY)** aliuliza:-

(a) Je, kwa nini Serikali isipunguze kodi kwenye vifaa vya ujenzi ili Wananchi waweze kujenga nyumba za kisasa?

(b) Je, Serikali ina mpango gani kuwawezesha Wananchi wa kipato cha chini kujenga nyumba za kisasa?



**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, Mbunge wa Jimbo la Mbulu, lenye vipengele (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, taratibu za utoaji wa misamaha ya kodi zinasimamiwa na kuongozwa na Sheria za Kodi zinazotoa misamaha. Sheria hizo zinajumuisha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148, Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147.

Mheshimiwa Spika, kimsingi, misamaha ya kodi iliyotolewa imekuwa ikihusu makundi ya jamii, sekta za kiuchumi na kijamii, ambazo huwagusa wananchi waishio mijini na vijijini; mfano, misamaha ya kodi hutolewa kwa zana za kilimo ili kumwezesha mkulima kupata mahitaji hayo kwa bei nafuu na kuongeza uzalishaji wa mazao. Aidha, unafuu wa kodi hutolewa kwa mashirika ya dini na yasiyo ya kiserikali ili yaweze kutoa huduma za afya, elimu, maji na kadhalika katika maeneo waishio Wananchi na hasa yale ya vijijini. Kwa mantiki hiyo, makundi mbalimbali ya jamii na sekta za uchumi na kijamii, zimekuwa zikinufaika na misamaha hii.

Mheshimiwa Spika, kodi inayotowza kwenye vifaa vya ujenzi inazingatia Sheria za Kodi na hivyo hutozwa kwa misingi ya utozaji kodi ya kutobagua makundi ya jamii kwa mantiki kuwa, vifaa hivyo hutumiwa na Watanzania wote. Nia ya Serikali ni kuona kwamba, Wananchi wa Vijijini wanaishi kwenye makazi bora na hivyo ndiyo maana hutoa unafuu wa kodi kwa upande wa afya, elimu, vifaa na pembejo za kilimo na kadhalika. Serikali itaendelea kuimarisha huduma mbalimbali kama vile barabara za vijijini na masoko ili kuwawezesha Wananchi waishio katika maeneo hayo, kuongeza kipato na kuweza kupata vifaa vya ujenzi kwa gharama nafuu, kwa kuwa unafuu wa kodi peke yake, hautoshi kuondoa umaskini vijijini.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiendelea na utekelezaji wa mikakati mbalimbali ya kuwawezesha Wananchi kuongeza kipato na kuboresha maisha yao, ambapo ni pamoja na kuwawezesha kujenga nyumba za kisasa.

Hatua zinazochukuliwa ni pamoja na kusambaza teknolojia rahisi ya ujenzi wa nyumba bora na zenye gharama nafuu; kuhamasisha uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika wa Nyumba (*Housing Cooperatives*) na vikosi vya ujenzi wa nyumba katika ngazi za Wilaya na Kata; na kuanzishwa kwa *Tanzania Mortgage Refinancing Company*.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yangu kwamba, tutashirikiana kwa pamoja katika kuhimiza utekelezaji wa mikakati hiyo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa ya maisha bora kwa kila Mtanzania.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri hajaweka wazi kwamba Serikali inatafakari kuondoa kodi katika vifaa vya ujenzi ili kuwawezesha Wananchi kujenga nyumba bora na kuondokana na nyumba za tembe ambazo zinawadhalilisha katika karne hii. Je, Serikali iko tayari kujifunza kutoka kwa wenzetu nchi jirani ambao wameweka ruzuku katika vifaa vya ujenzi kama bati na *cement* ambayo inatokana na viwanda vyetu hapa Tanzania matokeo yake kufanya bidhaa hizo kuwa bei nafuu kuliko hata hapa nchini kwetu?

(ii) Kwa kuwa Benki ya Nyumba Tanzania ambayo ilifilisiwa mwaka 1995 ndiyo iliyokuwa na dhamana ya kujenga nyumba na kuwakopesha Wananchi; na kwa kuwa majibu ya Mheshimiwa Waziri yanafanana tangu mwaka 1995 mpaka leo; je, Serikali itatuambia utaratibu huu unaanza mwaka gani au unaanza lini? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Selasini, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba, Serikali iko mbioni na inafahamu kwamba, tozo za kodi kwenye vifaa vya ujenzi, inazingatia Sheria ya Kodi. Pamoja na ukweli kwamba, Serikali ingependa kuona Wananchi wote wanamudu gharama za ujenzi wa nyumba nafuu na wanaishi katika mazingira mazuri au makazi ambayo ni bora; hata hivyo, imekuwa ni vigumu sana kusamehe kodi na kuweka unafuu mkubwa wa kodi kwa kila bidhaa ambayo inahusu maisha ya kila siku. Kama nilivyosema, kwa swali la pili ni kwamba, kwenye mabenki, Serikali imeona ni vema iwasaidie Wananchi wake ili waweze kupata unafuu kupitia vyombo vya ujenzi na kujenga nyumba ambazo zina unafuu. Kwa hiyo, imeanzisha *Tanzania Mortgage Refinancing Company*, ambayo nimesema kwamba, itatoa mikopo kwa mabenki na kisha mabenki hayo yataweza kutoa mikopo kwa Wananchi kwa riba nafuu.

Na. 72

### **Kuwezesha Wachimbaji Madini Wadogo**

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE** aliuliza:-

Wachimbaji wakubwa wa madini wanaomiliki migodi mikubwa hupata misamaha ya kodi (*grace period*), lakini wachimbaji wadogo hawapati fursa hiyo wanayopata wenzao, hivyo kupata manufaa kidogo ikilinganishwa na manufaa makubwa wanayopata wachimbaji wakubwa.

Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kuwawezesha na kuwapa motisha wachimbaji wadogo ili nao waweze kufaidika na raslimali hizo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Catherine V. Magige, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi kwenye vifaa vya uchimbaji na utafutaji wa madini hutolewa kwa wachimbaji wote wakubwa na wadogo, ambao wanamiliki leseni halali za utafutaji na uchimbaji. Hata hivyo, misamaha hiyo hutolewa kwa mmiliki wa leseni baada ya kuwasilisha maombi yake kwa Kamishna wa Forodha kupitia kwa Kamishna wa Madini kwa ajili ya tathmini ya maombi hayo, yaani kuona kama vifaa vinavyoombewa msamaha ni sahihi kulingana na aina ya leseni na mahitaji halisi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekuwa ikishughulikia maombi ya wachimbaji wakubwa na wadogo kwa kuyachambua na kuyaandikia mapendekezo stahiki kabla ya kuyapeleka katika ngazi husika. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, hakuna mchimbaji mdogo ambaye ameomba msamaha wa kodi kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato na *Financial Law (Miscellaneous Amendments) Act 1997* akanyimwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa mchango wa wachimbaji wadogo, tangu mwaka 2009/2010 imeanzisha mfuko wa kuwasaidia wachimbaji wadogo kwa ajili ya kuwakopesha vifaa na mitaji na mfuko huo unaitwa *Small Scale Mining Development Revolving Fund*. Hadi sasa Kampuni tano za *STAMICO, Tan Discovery Mineral Consultancy Ltd, Kilimo G. and General Supplies Co. Ltd, C.E Holdings (T) Ltd, na Gemstyles Co. Ltd* zimepatiwa mikopo yenye riba nafuu kutoka katika Mfuko huo kwa ajili ya kuanzisha vituo vya kukodisha na kuuza vifaa vya uchimbaji (*hire-purchase scheme*) na uongezaji wa thamani ya madini kwa bei nafuu. Kampuni hizo hadi sasa zimekopesha jumla ya shilingi milioni 345.

Mheshimiwa Spika, vituo hivyo vimeanzishwa katika maeneo ya Rwamugasa Wilayani Geita - Busanda, Londoni Wilayani Singida na Pongwa Msungora Wilayani Bagamoyo kwa upande wa kukodisha na kuuza vifaa vya uchimbaji (*Hire-purchase scheme*). Vituo kwa ajili ya kuongeza thamani ya Madini vipo katika maeneo ya Mikocheni na Kijitonyama Jijini Dar es Salaam.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, ninapenda kumwuliza maswali mawili ya nyongeza.

Ninapenda kujua ni vigezo gani vilitumika katika kupata hizo kampuni tano zilizokopesha kama ulivyonielea katika jibu lako la msingi.

Je, Serikali ina mpango gani kusogeza vituo vya kukopesha vifaa vya uchimbaji wa madini hasa kwa maeneo ya wachimbaji wadogo kama vile Mererani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Catherine V. Magige kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, makampuni haya matano yaliyochaguliwa yamezingatia uwezo wa kampuni yenyewe, lakini pia na malengo ya mfuko wenyewe. Mfuko huu ulikuwa na malengo kama matano, lakini kuna makampuni ambayo yanatoa huduma kwa wachimbaji wadogo, tunataka tuyazingatie makampuni hayo. Halafu kuna wachimbaji wenyewe wadogo kuwawezesha katika vikundi vyao ambavyo sasa hiyo inakidhi mahitaji au maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, tulikuwa na mpango wa kuelekeza uwezeshaji wa wachimbaji wadogo kupitia vikundi vyao vya uzalishaji.

Kwa hiyo, kwa sasa hivi kwa sababu pesa zenyewe zilizokusudiwa kuanzisha mfuko ni shilingi bilioni tano, tumeanza na pesa ndogo, lakini tumesema tuanze na hizi kampuni ambazo zinajikita kutoa huduma, yaani *Service providers* kwa wachimbaji wadogo. Kwa hiyo, hicho ndicho kigezo kilichotumika. Ndiyo maana nikasema katika awamu ya kwanza ya shilingi bilioni 1.2 zimeshatolewa shilingi milioni 430, wamepatiwa shilingi milioni 300 na tunatarajia tutaendelea kuwaongezea wachimbaji wadogo wenyewe moja kwa moja katika uzalishaji na pia *service providers* wa makampuni haya kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, hili la pili la kusogeza vituo kwa wachimbaji wadogo ndiyo lengo, kwa hiyo, sasa hivi nimesema tumekwenda Rwamgasa kula Busanda na Londoni, Singida na Bagamoyo kwa wachimbaji wa kokoto, lakini lengo ni kwenda Mererani kama alivyoomba Mheshimiwa Catherine V. Magige, lengo ni kwenda Ikungu kule Nachingwea kwa Mheshimiwa Chikawe na Mungo, Rwanda kwa Mheshimiwa Majaliwa na maeneo mengine kama hayo ambayo tunakusudia kwamba huduma au mfuko wenyewe uwe palepale *site* na siyo wachimbaji wadogo kuja mbali, Dar es Salaam kupata huduma hizo.

Na. 73

### **Tatizo Sugu la Maji Korogwe**

**MHE. MARY PIUS CHATANDA** aliuliza:-

Halmashauri ya Mji wa Korogwe ina tatizo sugu la ukosefu wa maji hali inayosababisha magonjwa ya milipuko kama kipindupindu cha mara kwa mara na wanawake na watoto kwenda kuchoma maji ya Mto Pangani na kukamatwa na mamba.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wananchi hao maji, hata kwa kuwachimia visima virefu/vifupi wakati wakiendelea na mpango wa *World Bank*?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inakiri kuwa na Halmashauri ya Mji wa Korogwe ambayo inajumuisha eneo linalohudumiwa na Mamlaka ya Maji Mjini Korogwe na eneo la vijiji vilivyopo pembezoni mwa Mji na ina upungufu wa huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa kero hiyo ya maji katika meneo husika, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji wa Korogwe inatekeleza Program ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji tangu mwaka 2007. Mchakato wa utekelezaji wa Programu hii ulianza na ukarabati/ujenzi wa miradi ya kuleta matokeo ya haraka ujulikano kama *Quick win projects*, lengo likiwa ni kupunguza kero ya huduma ya maji kwa wananchi sambamba na utekelezaji wa miradi ya vijiji kumi kwa kila Halmashauri nchini.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007 Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji wa Korogwe, ilitokeleza miradi ya kuleta matokeo ya haraka kwa kuchimba visima vifupi katika vijiji vya Chang'ombe (Kisima kimoja), Kwakombo (Kisima kimoja), Mahenge (Kisima kimoja), Msambazi (Kisima kimoja), Kwamsisi (Kisima kimoja) na Mgombezi (Visima viwili). Jumla ya shilingi miliomi 33.2 zilitumika kwa kazi hiyo na jumla ya wakazi 13,541 wanapatiwa huduma ya maji safi.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali ya Wilaya ya Mji wa Korogwe ilimwajiri mtaalamu mshauri *COWI Tanzania Consulting Engineers and Planners Ltd* tarehe 20 Mei, 2009 ambaye anafanya kazi ya kutafuta vyanzo vya maji, kusanifu miradi na kuandaa makabrasha ya zabuni na kusimamia ujenzi wa miradi katika vijiji vya Kwasisi, Kwakombo, Kwamndolwa, Kwameta, Mahenge, Kwasemangube, Lwengera Relini, Mgombezi, Mgambo na Msambazi. Baada ya mtaalamu mshauri kutafuta vyanzo vya maji, mchakato wa kumtafuta mkandarasi wa uchimbaji wa visima vya majaribio ulifanyika na kukamilika. Halmashauri ya Mji wa Korogwe itasaini mkataba na Mkandarasi mwezi wa Aprili, 2011 na kuanza kazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imeanza kuchukua hatua za kuboresha huduma za maji katika Mji wa Korogwe. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 Serikali imetenga shilingi milioni 750 kupitia Programu ya maendeleo ya Sekta ya Maji (*WSDP*) kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa hali ya maji na kuchimba visima virefu viwili kwenye maeneo ya Kilole Juu na Mlimafundi na kufunga pampu kwenye visima vitakavyochimbwa, kukarabati chanzo cha maji cha mto Mbeza, kukarabati mtandao wa kusambaza maji ili kupunguza maji yanayopotea, kupanua mtandao wa kusambaza maji kwa kilomita mbili ili kuongeza huduma na kukarabati tenki la maji la chuma Kwamkole.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutekeleza miradi hiyo, uzalishaji wa maji katika Halmashauri ya Mji wa Korogwe utaimarika na hivyo kupunguza tatizo la maji.

**MHE. MARY PIUS CHATANDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa tayari kuna miundombinu katika chanzo cha maji cha mto Mbeza na tayari wananchi wa Korogwe wanaendelea kuteseka na upatikanaji wa maji

safi na salama: Je, Waziri haoni upo umuhimu wa kukarabati kwa dharura chanzo cha mto Mbeza ili wananchi hawa waweze kupata maji kwa uhakika?

(b) Kwa kuwa Mji wa Korogwe unapitiwa na Mto Pangani katikati: Je, Serikali haioni upo umuhimu wa kujenga matenki makubwa na kusambaza miundombinu ili wananchi wa Korogwe ambao wanapata tatizo kubwa la maji waweze kupata maji safi na salama?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoieleza kwenye jibu langu la msingi kwamba Serikali imetenga shilingi milioni 750 hii ni pamoja na kuweza kukarabati chanzo cha maji cha mto Mbeza. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo tutapata maji zaidi nakuweza kuongeza upatikanaji wa maji katika Mji wa Kwamkole.

Katika sehemu (b) labda nimjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba Mji wa Korogwe uko chini ya mpango maalum tunaaita *Clustering*, Mamlaka ya Jiji la Tanga litashughulikia kusimamia hii Miji midogo ya Muheza, Pangani na Korogwe ili kuweza kuongezea ufanisi zaidi na kuhakikisha kwamba wananchi watapata maji zaidi ya uhakika.

**MHE. ABDUL – AZIZ MOHAMED ABOUD:** Mheshimiwa Spika, tatizo la Halmashauri ya Korogwe linafanana na tatizo la Halmashauri ya Morogoro Mjini.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya Kata katika Halmashauri ya Morogoro Mjini, yaani Kata ya Kihonda, Mkundi, Lukobe, Kasanga A, Kasanga B, Nane Nane, Kingorwila na Mindu, kuna tatizo kubwa na sugu la maji: Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia maji wananchi katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na tatizo la maji Morogoro mjini kama ifuatavyo:-

Morogoro tuna mradi mkubwa wa kukarabati miundimbinu ya maji katika mji wa Morogoro, kwa hiyo maeneo hayo Mbunge aliyoyataja yatahusishwa na wataweza kupata maji ya uhakika.

Na. 74

### **Tatizo la Maji – Tarafa ya Mlalo**

**MHE. HENRY D. SHEKIFU** aliuliza:-

Tarafa ya Mlalo Jimboni Lushoto inakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani ya kusaidia juhudi za wananchi wa Tarafa hiyo ambao wamechanga fedha ili kupata mtaalamu wa kufanya uchambuzi wa kupata maji toka mlima Mtumbi?

(b) Baada ya uchambuzi huo kukamilika, Serikali inawaahidi nini wananchi katika utekelezaji wa mradi huo ambao utahudumia Vijiji vya Kata za Kwekanga, Malimbwi na Kikole?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Henry D. Shekifu, Mbunge wa Lushoto kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inapogeza juhudi za wananchi wa Tarafa ya Mlalo, Jimbo la Lushoto kwa jitihada zao za kuchanga fedha na kuweza kumpata mtalaamu wa maji (Bwana Abdul Mbwambo) ambaye amefanya upembuzi wa awali wa kuweza kupata maji toka mlima Mtumbi. Serikali kupitia Halmashauri ya Lushoto katika mipango yake ya maendeleo itaweka mradi huo na kuendeleza katika hatua za usanifu na hatimaye kuujenga.

(b) Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi huo kukamilika, Serikali kupitia Halmashauri ya Lushoto itauweka mradi wa maji Mtumbi katika vijiji vyenye kipaumbele vitakavyowekwa katika awamu ya pili ya Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini itakayoanza kutelezwa mwezi Julai, 2012.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, namshukuru sana kwa kutoa majibu ya matumaini. Wananchi hawa walichanga fedha zao kuanzia mwaka 2004, ndiyo wamemaliza upembuzi wa msingi, yaani mwanzo. Sasa kwa sababu wananchi hawa wamepoteza matumaini na leo Serikali inatamka kwamba itasaidia kwa mwaka 2012: Je, kwa sasa Serikali inatamka nini kuwahakikishia kwamba mradi huu unawekwa katika mipango ya Halmashauri mwaka 2011/2012?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, tunaposema kwamba Serikali itaweka katika awamu ya pili, maana yake hili tayari ni ahadi ya Serikali. Kwa hiyo, Halmashauri ni lazima ifanye hivyo, yaani iweke katika mpango wa kutekeleza mradi huu. Kwa hiyo, hili ni agizo.

**MHE. MANSOOR SHANIF MIRAN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana umenipa nafasi ya kuuliza swali. Kwa kuwa tatizo la Jimbo la Kwimba hususan mji mdogo wa Ngudu unafanana na matatizo yaliyoelezwa katika maeneo yaliyotajwa kwenye swali lililo mbele yetu, naomba kujua ni lini Wizara itatusaidia Jimbo la Kwimba hususan Mji mdogo wa Ngudu wenye matatizo ya maji, visima vipo vitano lakini viwili havina pampu ya kusukuma maji na pia pampu kubwa ya kusukuma maji kutoka tenki kubwa kupeleka kwa wananchi ni mbovu, mara kwa mara hiyo pampu inaharibika, wananchi wanakosa maji kwa karibuni takribani hata wiki moja?

Naomba kujua ni lini Serikali itatusaidia kutuletea mitambo mipya ili maji yaweze kupatikana kwa uhakika zaidi kwenye mji mdogo wa Ngudu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, tatizo la maji katika Mji wa Ngudu tumeshalielewa na sasa hivi tunafanya tathmini ili tuone ni namna gani tutaweza kusaidia na kulitatua kwa haraka tatizo hilo.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyoona, muda wa maswali umekwisha na maswali pia yamekwisha. Lakini tunajifunza tena kwamba mkitaka kujibiwa vizuri maswali yenu yawe yanayofanana na lile swali la msingi. Maswali ya nyongeza ni juu ya lile la msingi. Sasa inaonekana watu wanauliza maswali mengine kabisa, matokeo yake Waziri hawezi kujua majibu ya maeneo mbalimbali, haiwezekani. Kwa hiyo, swali la nyongeza liwe linafanana na liwe la kisera siyo kila kitu kinafanana na kwetu. Haiwezekani kufanana kila mahali. Kwa hiyo, mnakosa fursa ya kujibiwa vizuri kwa sababu ya kuuliza maswali ambayo Waziri hawezi kujua na kuuliza maswali marefu yanatupotezea muda wa kuuliza maswali mengi ya nyongeza.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni kwenye *Speakers Gallery* nao ni wataalamu wanaoongozana na Ndugu Ludovick Utoh - Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali. (*Makofi*)

Zaidi ya hayo ni kwamba katika kuwasilisha hati mbalimbali za Serikali ambazo zimewasilishwa asubuhi hii, kuna hati moja inaitwa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi wa ufanisi wa ufuatiliaji na tathmini ya mgawanyo wa bajeti kwa shughuli za huduma za kijamii kwa akina mama na watoto Tanzania.

Inasema: *The General Report of the Control and Auditor General on Performance Audit on the Monitoring Evaluation and Budget, all action for Maternal Health Care Activities in Tanzania.* Hawa jamaa walishindanishwa na Wakaguzi wengine wa kimataifa wa Sweeden *SNAO Prize*, kwa hiyo, Wakaguzi wa Tanzania wameshinda *first prize* na ndiyo *report* hii mtaiona katika vitabu vyenu, wameshinda vizuri sana. Wameshinda kama Taasisi ya Ukaguzi, lakini na waliohusika wa tatu pia wameshinda tuzo ya juu zaidi kutokana na eneo lake. Kwa hiyo, tunampongeza Mheshimiwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kuendelea kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa ndani ya nchi na nje ya nchi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge pia kuna matangazo ya kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo - Mheshimiwa George B. Simbachawene, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo kwamba kutakuwa na kikao cha kujadili Muswada wa Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama, 2011 (*The Judicial Administration Bill*) leo hii saa 5.00 asubuhi katika ukumbi wa Msekwa 'C', kwa hiyo, ile Kamati ya Sheria Ndogo wakutane huko leo saa 5.00 asubuhi kujadili huu Muswada.

Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala - Mheshimiwa Pindi Chana, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo hii saa 7.00 mchana wakutane katika Ukumbi wa Msekwa 'B'.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama - Mheshimiwa Edward Lowasa anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba kutakuwa na kikao leo hii saa 5.00 asubuhi katika ukumbi Na. 231. Kwa hiyo, Wajumbe wa Kamati hiyo wanatakiwa kuhudhuria kikao hicho.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Katibu wa Kamati ya Wabunge wa CCM anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM kwamba leo baada ya kuahirisha kikao cha Bunge jioni kutakuweko na kikao cha Kambi ya Chama hicho katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Tangazo lingine, Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Uongozi pamoja na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kuwa kutakuwa na kikao leo saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Spika. Ni wale Wenyeviti wote wa Kamati zetu za kudumu pamoja na Makamu wao.

Pia ofisi ya Bunge inawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeleta nyaraka zifuatazo na zimewekwa kwenye *pigeon holes* zenu. Waraka wa kwanza ni Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 (*The Land Act No. 4, 1999*), kuna Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999, halafu kuna *The Land Registrations Act of 2001*, Kanuni za Ardhi ya Vijiji ya mwaka 2002, halafu kuna *Morgage Financing Special Provisions Act, 2008* na ya mwisho ni *The Unity Titles Act, 2008*. Wamewaletea hizi zote ili kuweza kuzifahamu kwa sababu nyie wote mnashughulika na wananchi na matatizo ya ardhi yapo mengi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mzechukue zile, msiziache kwenye *pigeon holes*, ni documents muhimu sana kwenu kwa hiyo hakikisheni kila mtu anachukua. Hata ukichukua ukaweka ofisini kwako kule itakusaidia zaidi.

Halafu, ofisi tena inaomba niwatangazie wafuatao wafike Chumba Na. 311 Idara ya Utawala na Raslimali Watu kabla ya saa 7.00 mchana, kuna maelezo muhimu. Hawa ni Mheshimiwa Mary M. Nagu, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Deogratias Ntukumazima, Mheshimiwa Jeremiah Sumari, Mheshimiwa Gerude Rwakatare, Mheshimiwa Lolencia Bukwimba na Mheshimiwa Susan A. Lyimo. Hawa watakwenda kujua huko wanachoitwa, mimi sifahamu, Chumba Na. 311 naona kuna shughuli zinazowahusu wao binafsi.

Hawa wa *Sports Club* mnapenda kuandika kwa mkono tu, hii ni dalili inayoonesha kwamba hamjajipanga vizuri. Matangazo yenu myalete yakiwa yamechapishwa. Sasa sijui ni nani huyu anayatengaza, ni Mheshimiwa Kassim Majaliwa - Kocha wa timu ya *Football Club* ya Bunge, anasema mazoezi yanaendelea rasmi leo kwa maandalizi ya mchezo wa kirafiki kati ya Bunge na *LAPF* siku ya Jumamosi katika Uwanja wa Jamhuri.

Wachezaji wote wanaombwa kufika kwenye mazoezi kila siku saa 12.00 asubuhi. Wabunge wote mnaombwa mhudhurie mazoezi ya viungo kila siku sasa 12.00 asubuhi Jamhuri Stadium. Naomba mjifunze kuandaa matangazo yenu na kuyachapisha na sio kuandikia hapa hapa. Hii itaendelea kuonesha kwamba hamwendi na wakati.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani matangazo yametosha, sasa tunaendelea na shughuli inayofuata.

## **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

### **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Maeneo ya Maendeleo ya Kiuchumi wa Mwaka 2011 (*The Economic Zones Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2011*)**

*(Kusomwa mara ya Pili)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuaminiwa na Watanzania kuiongoza nchi yetu kwa kipindi cha miaka mingine mitano. Aidha, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kunitewa tena katika Baraza lake la Mawaziri na kunipandisha ngazi kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara.

Nampongeza pia Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda - Waziri Mkuu, kwa kuteuliwa kushika wadhifa huo tena kwa kipindi cha miaka mitano. Namshukuru pia kwa maelekezo yake ya mara kwa mara ambayo yameniwezesha kutekeleza majukumu yangu ipasavyo. Nawapongeza pia Mawaziri wote walioteuliwa kushika nyadhifa hizo na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuaminiwa na Watanzania waliowachagua kuwa wawakilishi wao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii pia, kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwako kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi cha miaka mitano ya uhai wa Bunge hili ukiwa Spika wa kwanza Mwanamke. Nimpongeze pia Naibu Spika Mheshimiwa Job Ndugai kwa kuchaguliwa kushika nafasi ya Naibu Spika.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati wapigakura wangu wa Jimbo la Moshi Vijijini kwa imani kubwa walioionesha kwangu kwa kunichagua tena kuwa Mbunge wao kwa kipindi cha pili. Nawashukuru sana na ninawaahidi kuwatumikia kwa moyo wangu wote.

Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Maeneo Maalum ya Kukuza Uchumi (*The Economic Development Zones Laws (Miscellaneous Amendments) Act 2011*, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2007. Wizara yangu inaleta katika Bunge lako Tukufu Muswada huu unaolenga kufanya marekebisho madogo kwenye Sheria za *Export Processing Zones (EPZ)* na *Special Economic Zones (SEZ)* kama njia mojawapo ya kuboresha utekelezaji wa Sheria hizo na hivyo kuchochea uwekezaji katika Maeneo Maalum ya Uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha Muswada huu, napenda kuwashukuru wadau wa Sekta ya Viwanda na Biashara ambao walichambua na kutoa michango yao kwa njia ya maandishi na kauli. Aidha, naishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara ambayo kwa jitihada kubwa imechambua na kutoa maoni juu ya Muswada huu. Kwa namna ya pekee nampongeza Mheshimiwa Mahmoud Mгимwa - Mbunge wa Mufindi Kaskazini na Mwenyekiti wa Kamati hii, pia Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum na Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa michango yao na ushirikiano wao mzuri katika kukamilisha Muswada huu. Maoni ya Wadau wa Sekta ya Viwanda na Biashara pamoja na ya Kamati ya Viwanda na Biashara yaliboresha kwa kiasi kikubwa Muswada ninaouwasilisha mbele ya Bunge lako leo hii.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Muswada huu kama nilivyoeleza hapo juu, ni kufanya marekebisho ya Sheria za Mifumo ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje (*EPZ Act*) na ya Maeneo Maalum ya Kiuchumi (*SEZ Act*) ili kuipa nguvu Mamlaka ya *EPZ (Export Processing Zones Authority - EPZA)* kusimamia pia Sheria ya *SEZ*. Aidha, marekebisho hayo pia yanalenga kubadilisha mfumo wa usimamizi wa Mamlaka ya *EPZ* kwa kuweka Bodi badala ya Baraza.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002 Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara ilianzisha maeneo ya *EPZ* kupitia Sheria ya *EPZ* ya mwaka 2002. Lengo la kuanzishwa kwa *EPZ* lilikuwa kuinua uchumi na hasa mauzo nje ikiwa ni mojawapo ya utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda (1996-2020).

Sheria ya *EPZ* ilifanyiwa marekebisho mwaka 2006 na matokeo yake yakawa kuanzishwa kwa Mamlaka ya *EPZ*. Mwaka 2006 pia Serikali ilianzisha Mfumo wa *SEZ* kupitia Sheria ya *SEZ* ya mwaka 2006 ikiwa ni mfumo wa kutekeleza *Tanzania Mini-Tiger Plan, 2020* chini ya iliyokuwa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezesaji. Mwaka 2008, majukumu ya *SEZ* yaliamishwa iliyokuwa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko baada ya iliyokuwa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezesaji kuvunjwa.

Mheshimiwa Spika, tofauti ya mifumo hii ni kwamba wakati mfumo wa *EPZ* unalenga sekta moja ya uzalishaji viwandani ambapo zaidi ya asilimia 80 ya bidhaa huuzwa nje ya nchi, mfumo wa *SEZ* unalenga sekta mbalimbali kama vile viwanda, kilimo, biashara, utalii, na kadhalika. Pia, mfumo wa *SEZ* hauna masharti ya kiasi cha kuuza nje ya nchi ambapo mwekezaji anaweza kuuza sehemu kubwa ya bidhaa au bidhaa zote katika soko la ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, uzoefu wa utekelezaji wa majukumu ya *EPZ* na *SEZ* chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, umeonesha kuwa sheria zinazotumika kusimamia *EPZ* na *SEZ* zinaingiliana katika maeneo mengi hususan utengaji wa maeneo ya uwekezaji, mifumo ya usimamizi, vivutio vya uwekezaji na masoko na hivyo kusababisha migongano katika utekelezaji kwa vile mahitaji yake yanafanana. Aidha, mamlaka ya *EPZ* ambayo imepewa pia jukumu la kusimamia utekelezaji wa *SEZ*, haina nguvu ya kisheria ya kusimamia mfumo huo kwa vile Sheria ya *SEZ* imeainisha kuanzishwa kwa mamlaka ya *SEZ* ambayo ndio ingesimamia mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, ili kuepuka migongano iliyojitokeza katika usimamizi, kuipa nguvu *EPZA* kusimamia mfumo wa *SEZ* na kwa kuzingatia uzoefu kutoka nchi nyingine ambazo zinatekeleza mfumo ya aina hii, tarehe 15 Julai, 2010 Wizara iliwasilisha Waraka wa Baraza la Mawaziri wa mapendekezo ya kuunganisha mfumo ya *EPZ* na *SEZ* ili kuwa na mfumo mmoja utakaoitwa Maeneo ya Kukuza Uchumi (*The Economic Development Zones - EDZs*). Maamuzi yaliyotolewa na Baraza la Mawaziri ni haya yafuatayo:-

- (a) Sheria ya *Export Processing Zone (EPZ)* ifanyiwe marekebisho ipasavyo ili mamlaka ya *EPZ (EPZA)* sasa isimamie pia Maeneo Maalum ya Uchumi (*Special Economic Zones - SEZs*);
- (b) Sheria ya *SEZ* ifanyiwe marekebisho na kuwianishwa na ya *EPZ* ili:-
  - (i) Mamlaka ya Usimamizi wa *SEZ* iwe *EPZA*; na
  - (ii) Waziri wa Kusimamia Sheria ya *SEZ* awe Waziri mwenye dhamana ya Viwanda badala ya Uwekezaji.
- (c) *EPZA* sasa isimamiwe na Bodi badala ya Baraza.

Hivyo, Muswada ulioko mbele yetu una nia ya kutekeleza maamuzi ya Baraza la Mawaziri ya kurekebisha na kuwianisha sheria za *EPZ* na *SEZ*.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unazingatia kuondoa baadhi ya vifungu vya sheria, kuingiza vifungu vipya, kufuta baadhi ya vifungu na maneno na kuingiza maneno mapya pamoja na kuongeza masharti yanayoambatana na kufutwa kwa Baraza na kuanzishwa kwa Bodi ya kiutendaji ili kuboresha utekelezaji wa Mamlaka ya *EPZ*.

Sehemu ya Kwanza ya Muswada inatoa utangulizi ambao unaeleza jina la Muswada na maudhui ya mapendekezo ya kurekebisha na kuwianisha Sheria za *EPZ* na *SEZ* na kuainisha majukumu ya Mamlaka ya *EPZ*.

Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho ya Sheria ya *EPZ* Sura ya 373 kwa kuondoa neno Baraza kokote linakotokea kwenye Sheria na kubadilisha na neno Bodi inayopendekezwa kuanzishwa katika Ibara ya 14. Aidha, sehemu hii inaipa Bodi mamlaka ya kuridhia sera za uendeshaji na maslahi ya wafanyakazi.

Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho ya Sheria ya *SEZ* Sura ya 420. Sehemu hii inaongeza tafsiri za maneno “Waziri, Mamlaka, Mkurugenzi Mkuu na Mipango ya Maendeleo” ili kuoanisha marekebisho yaliyofanyika katika Sheria hizi. Aidha, Sehemu hii inampa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya Ardhi kutwaa ardhi kwa madhumuni ya kutekeleza sheria hizi na kutoa mamlaka zaidi kwa Mamlaka ya *EPZ* kuridhia na kutoa vibali vya ujenzi chini ya Sheria ya Mipango Miji, Sura ya 355.

Sehemu hii pia inafuta vifungu vya 4 - 7 na 21, 23 hadi 27 na 38 baada ya mtiririko wa namba kurejewa kufuatia kufutwa kwa namba 4 - 7.

Kiambatisho cha Marekebisho (*Schedule of Amendment*) kinapendekeza Mwenyekiti wa Bodi ya EPZA kuwa Waziri mwenye dhamana ya Viwanda. Aidha, kimebadilisha mjumbe wa Bodi kutoka Wizara yenye dhamana ya Madini kuwa Wizara yenye dhamana ya Nishati. Kiambatisho hiki pia kimeainisha masuala yote ya SEZ yanayohusiana na kufuta, kusitisha na kurekebisha leseni. Rufaa dhidi ya maamuzi yanayofanywa na Mamlaka ya EPZ na Shughuli nyingine zisizoruhusiwa yatashughulikiwa kama ilivyoainishwa kwa mujibu wa Vifungu Na. 7, 8, 9 na 10 vya Sheria ya EPZ. Vilevile, Kiambatisho hicho kinafuta Kifungu Na. 38 cha Sheria ya SEZ kama namba zilivyorekebisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Kabla sijamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Muswada huu, unajua tena kuna vikaratasi vya matangazo vinakuja haraka haraka, sasa mtu ukishasimama huwezi kuviona. Kwa hiyo, Mheshimiwa John Mnyika - Katibu wa Wabunge wa CHADEMA hapa Bungeni anaomba niwatangazie Wabunge wa CHADEMA kwamba leo watakutana katika chumba Na. 219 saa 7.00 mchana.

Sasa ninamuita Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Muswada huu, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA NA BIAHARA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Maeneo Maalum ya Kukuza Uchumi (*The Economic Development Zones Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2011*, kwa mujibu wa kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2007.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuwasilisha maoni ya Kamati, napenda nichukue fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwako kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nampongeza Naibu Spika - Mheshimiwa Job Ndugai kwa kuchaguliwa kushika nafasi hii ya Naibu Spika.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Wajumbe wa Tume ya Bunge kwa kuchaguliwa kwao kushika wadhifa huo. Aidha, nawapongeza Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuchaguliwa kwao kuziongoza Kamati za Bunge ambazo ndiyo mhimili wa Bunge letu. Kwa namna ya pekee nampongeza na kumshukuru Makamu Mwenyekiti wangu Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya kwa ushirikiano mkubwa anaotoa wakati wote wa kutekeleza

majukumu ya Kamati. Pongezi pia kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa kuliwakilisha Bunge letu katika nafasi mbalimbali za ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuaminiwa na Watanzania kuiongoza nchi yetu kwa kipindi cha miaka mitano tena. Nampongeza Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda kwa kuteuliwa kushika wadhifa huo tena kwa kipindi cha miaka mitano na nawapongeza pia Mawaziri wote walioteuliwa kushika wadhifa huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya Kamati kutoa salaam za rambirambi kwa wakazi wote wa Gongolo la Mboto kwa maafa yaliyotokea. Aidha, natoa pole kwa familia za wanamuziki wa *Five Stars Modern Taarabu* na wale wote waliopata ajali kwa kipindi hiki. Tunatoa pole pia kwa Waheshimiwa Wabunge waliofiwa na ndugu na jamaa zao, Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu wa Sheria ya Maeneo Maalum ya kukuza Uchumi (*The Economic Development Zones Laws*) wa Mwaka 2011, unalenga kufanya marekebisho ya Sheria za Mifumo ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje (*Export Processing Zone Act*) na ya Maeneo Maalum ya Kiuchumi (*Special Economic Zone Act*). Marekebisho haya yanalenga kuipa nguvu Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje (*Export Processing Zones Authority – EPZA*) kusimamia Sheria ya Maeneo Maalum ya Kiuchumi (*Special Economic Zone - SEZ*) kufuatia Sheria hiyo kuwekwa chini ya Mamlaka ya *EPZ*. Aidha, marekebisho haya yataondoa migongano ambayo ingejitokeza katika usimamizi na utekelezaji wa sheria hizi mbili katika utengaji wa maeneo ya uwekezaji, utoaji wa vivutio vya uwekezaji, usimamizi wa miradi iliyoanzishwa na masoko.

Pia, imeonekana kwamba utekelezaji wa mifumo hii miwili chini ya Taasisi mbili tofauti zinazofanya shughuli zinazofanana kama ilivyokuwa ifanyike hapo awali ni upotevu wa rasilimali.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, Kamati yangu ilikutana Dar es Salam kwa siku mbili kuchambua na kujadili Muswada wa Maeneo Maalum ya Kukuza Uchumi. Kwa kuzingatia Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, Kamati yangu iliwakaribisha wadau tarehe 29 Machi, 2011 ili waweze kujadili na kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu.

Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wadau wote waliohudhuria na kutoa mawazo yao kwa lengo la kuboresha Muswada. Ushiriki wa wadau ulikuwa wa kuridhisha kwani wadau wote muhimu walioalikwa walifika. Baadhi ya wadau hao ni Kituo cha Sheria cha Haki za Binadamu, (*Legal Human Rights Centre - LHRC*), wawakilishi wa wawekezaji katika Maeneo Maalumu kutoka Arusha na Mabibo DSM; *TCCIA*, Kituo cha Uwekezaji (*CTI*) na Chama cha Wataalamu wa Biashara (*TTIA*).

Mheshimiwa Spika, tarehe 30 Machi, 2011 Kamati yangu ilikutana na Waziri ambaye aliwasilisha Muswada wa Sheria ya Maeneo Maalum ya Kukuza Uchumi na Kamati ilipata fursa ya kutoa maoni na ushauri wa kuzingatiwa katika utekelezaji wa Sheria hii. Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi wa kuirekebisha Mifumo ya EPZ na SEZ kwani itapunguza usumbufu kwa wawekezaji na kuondoa matumizi mabaya ya rasilimali. Hata hivyo, Kamati imeona kuwa Muswada huu umechelewa kuletwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa kina wa Maudhui ya Muswada huu, Kamati yangu inaomba Bunge lako Tukufu liridhie Muswada huu wa kurekebisha Sheria za Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje (*Export Processing Zone Act*) na ya Maeneo Maalum ya Kiuchumi (*Special Economic Zone Act*).

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imeridhishwa na Muswada huu kwani una lengo la kuondoa mwingiliano ambao ungejitokeza katika maeneo mengi hususan utengaji wa maeneo ya uwekezaji, mfumo wa usimamizi, vivutio vya uwekezaji na masoko na pia kuipa Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo nje (*EPZA*) nguvu ya kusimamia mfumo wa SEZ. Aidha, marekebisho haya yataondoa upotevu wa rasilimali ambazo zingepotea kwa kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Mfumo wa SEZ.

Mheshimiwa Spika, pamoja na dhamira nzuri ya Serikali ya kufanyia marekebisho Sheria ya EPZ na SEZ, Kamati ilitegemea kuwa Serikali ingeunganisha moja kwa moja hizi mbili ili zisimamiwe na Sheria moja ya Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Kukuza Uchumi (*Economic Development Zones Authority – EDZAs*) . Kamati inashauri Serikali kufanya juhudi za makusudi kuunganisha Sheria za EPZ na SEZ ili kuwe na sheria moja itakayotekelezwa chini ya Mfumo wa Maeneo Maalum ya Kukuza Uchumi (*Economic Development Zones (EDZs)*) utakaosimamiwa na Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Kukuza Uchumi (*Economic Development Zones Authority - EDZAs*).

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri neno *acquire* litolewe tafsiri kama litakavyotumika katika Muswada huu. Kamati inashauri kuwa baada ya Muswada huu kupitishwa na kuwa Sheria, Serikali iharakishe kutengeneza kanuni ili kuondoa mianya ya kutokuwajibika vizuri na rushwa, kutokana na baadhi ya majukumu kupangwa na kuainishwa kwenye kanuni.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua Muswada, Kamati ilibaini kuwepo kwa maeneo ambayo yalitengwa kwa ajili ya EPZ na SEZ mfano Bagamoyo, Bunda na Songea ambayo yalipaswa kulipwa fidia kwa wananchi, lakini kwa muda mrefu maeneo hayo hajalipwa fidia. Hali hii inawafanya wananchi kushindwa kuendeleza maeneo yao ambayo wanatakiwa kuhamia. Jambo hili limedumaza juhudi za wananchi na kuwafanya waichukie Serikali yao ambayo kimsingi ina dhamira njema. Ili kuondoa migogoro inayoweza kujitokeza katika maeneo maalum ambayo yatatengwa kwa ajili ya uwekezaji na ambayo tayari yalikuwa yakimilikiwa na watu, Kamati inashauri, fidia inayopaswa kulipwa kwa wahusika wa maeneo hayo ilipwe mapema kabla ya mradi kuanza. Aidha,

wanakijiji wa maeneo husika washirikishwe kikamilifu tangu hatua za awali za mchakato wa umilikaji wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa maeneo ya *EPZ* na *SEZ* hayafahamiki kwa wananchi walio wengi na ili kukidhi dhamira ya Sera ya Viwanda Vidogo na vya Kati ya Mwaka 2003 pamoja na utekelezaji wa azma ya Kilimo Kwanza, Kamati inashauri Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Mauzo Nje (*EPZAs*) ifanye jitihada za makusudi za kujitangaza na kuelimisha jamii juu ya fursa za uwekezaji katika maeneo *EPZ* na *SEZ* zilizopo kwa wawekezaji wa ndani wakiwemo wajasiriamali wadogo, kwani kwa sasa wananchi wengi hawajui kama kuna fursa hizo katika maeneo ya *EPZ* na *SEZ* kwa ajili ya wawekezaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokutana na SIDO, ilijifunza matatizo yanayokwamisha viwanda vidogo Tanzania kuwa ni pamoja na ukosefu wa maeneo ya kufanyia kazi yenye miundombinu na hivyo kusababisha kuwepo na viwanda vidogo kiholela na visivyo na tija. Hali kadhalika, tulijifunza kuwa viwanda vikubwa hutegemeana sana na viwanda vidogo, hivyo kwa kuviweka katika ukanda mmoja kutaleta tija. Kwa misingi hiyo, Kamati inashauri kuwa kifungu cha 5(a) kinachofanyia marekebisho ya kifungu cha 13 (2)(a) yaongezeke maneno: *“And to Small and Medium Entrepreneurs”* hivyo kifungu kisomeke, *“In consultation with the Minister responsible for Lands and Minister responsible for Local Government Authorities, or issue derivative rights to Investors or erect thereon Industrial and Commercial building and lease such buildings to Investors for Undertakings thereon the Export Processing Zones licensed businesses and to Small and Medium Entrepreneurs”*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kifungu cha 5(2) (a) chenye marekebisho ya kifungu cha 13 cha Sheria kusigana na Sheria ya Uwekezaji kifungu cha 15 na 16, Sheria ya Umiliki wa Ardhi kifungu cha (3), Sheria ya Ardhi kifungu cha 25(1) (h) na (i) na Sheria ya Vijiji kifungu cha (8). Kamati inashauri kuwa masuala yote yanayohusu ardhi na uwekezaji yafanyike kwa kufuata Sheria ya Ardhi (*Land Act*), Sheria ya Umiliki wa Ardhi (*Land Acquisition Act*) na Sheria ya Vijiji (*Village Land Act*).

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inaipongeza na kukubaliana na Serikali kuondoa neno Baraza popote linapojitokeza katika Muswada huu pamoja na kazi zake kuzihamishia kwenye Bodi inayopendekezwa kuanzishwa katika Ibara ya (4). Kamati yangu inaamini kuwa uanzishwaji wa Bodi utaipa nguvu Bodi kuridhia na kusimamia utekelezaji wa Sera na usimamiaji wa maslahi ya Wafanyakazi. Hata hivyo, Kamati yangu imebaini mapungufu katika muundo wa Bodi mpya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokuwepo kwa uwakilishi wa Taasisi muhimu katika Bodi mfano, Katibu Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (*TUCTA*), ambaye katika Sheria inayorekebishwa alikuwepo na sasa ameondolewa, Mkurugenzi Mtendaji wa *EPZA*. Kutokana na mapungufu haya, Kamati inashauri kifungu cha 14 kifanyiwe marekebisho kwa kuongeza uwakilishi katika Bodi wa Katibu Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (*TUCTA*), na Mkurugenzi Mtendaji wa *EPZA* ambaye inapendekezwa awe Katibu wa Bodi.



Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri pia kuwa kifungu cha (6) kinachofuta maneno ya kifungu cha 14 na kubadilisha maneno mengine, kifungu 14 (2)(a) yaongezwe maneno “*who shall be the Chairperson of the Board.*” Hivyo kifungu hicho sasa kisomeke *The Minister responsible for Industries* “*who shall be the Chairperson of the Board.*”

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa kifungu cha (6) kinachofuta maneno ya kifungu cha 14 na kubadilisha maneno mengine, kifungu 14 (2)(e) liondolewe neno “*Minerals*” liandikwe neno “*Energy*”, hivyo kifungu hicho kisomeke “*The Permanent Secretary of the Ministry responsible for Energy*”.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa kifungu cha (6) kinachofuta maneno ya kifungu cha 14 na kubadilisha maneno mengine, kifungu 14 (2)(h) kinachosomeka, “*The Commissioner General of the Tanzania Revenue Authority*”, kiondolewe kwa sababu tayari upo uwakilishi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha katika Bodi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kifungu cha (6) marekebisho ya kifungu cha 14(3) kifanyiwe marekebisho na kuongeza maneno “*if required*”, hivyo kisomeke, “*The Board may Co-opt any other person to attend Meetings of the Board* “*if required.*”

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 9(a) kinachofanyiwa marekebisho ya kifungu cha (3), kuna neno “*industries*” limekosewa na kuandikwa “*industries*”. Kamati inashauri neno hilo lirekebishwe, hivyo lisomeke “*Industries*”.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inaipongeza Serikali kwa kuweka karibu vitengo vyote vinavyohitajika katika Mamlaka kwa lengo la kurahisisha huduma kwa wawekezaji. Hata hivyo kumekuwepo na malalamiko mengi kuhusu urasimu usio wa lazima katika kitengo cha *TRA*, na hivyo kusababisha mali ghafi zinazolingia na kutoka bandarini kucheleweshwa sana. Ili kuondokana na tatizo hili, Kamati inashauri kwamba Afisa wa *TRA* atakayekuwepo katika eneo la uwekezaji, apewe mamlaka kamili ya maamuzi yahasuyo kodi. Aidha, kuwepo pia na Afisa kutoka Mamlaka ya Bandari atakayeshughulikia masuala yanayohusu Bandari.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara kwa kutoa maoni yao katika kuboresha Muswada huu. Naomba niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mahmoud H. Mgimwa - Mwenyekiti, Mhe. Eng. Stella M. Manyanya – Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mheshimiwa Khatibu Said Haji, Mheshimiwa Shawana Bukheti Hassan, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Haji Khatibu Kai, Mheshimiwa Naomi A. Mwakyoma Kaihula, Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mheshimiwa Godbless Johnathan Lema, Mheshimiwa Chiku Aflah Abwao, Mheshimiwa Conchesta Leons Rwamlaza, Mheshimiwa Ester Lukago Minza Midimu, Mheshimiwa Margaret Agnes Mkanga,

Mheshimiwa Said Mussa Zuberi, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Ezekia Dibogo Wenje, Mheshimiwa Salim Abdallah Turkey Hassan, Mheshimiwa Jumaa Hamoud Abuu, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga na Mheshimiwa Mohamed Gulam Dewji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru Waziri wa Viwanda na Biashara - Mheshimiwa Dr. Cyril Chami, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara - Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Katibu Mkuu wa Viwanda na Biashara - Ndg. Joyce Mapunjo, Naibu Katibu Mkuu Dr. Shaban Mwinjaka - Mkurugenzi Mtendaji wa EPZA Dr. Edelhelm Meru na Watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa Muswada huu. Vile vile nawashukuru Wadau wote waliofika mbele ya Kamati na kutoa Maoni na Mapendekezo yao kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda nimshukuru Katibu wa Bunge Dr. Thomas D. Kasilillah kwa umakini wake katika kuiongoza Ofisi ya Bunge katika kutekeleza majukumu yake. Aidha, namshukuru Katibu wa Kamati hii, Ndugu Angelina Sanga na Msaidizi wake Paulina Mavunde kwa kuihudumia Kamati vizuri pamoja na kukamilisha Taarifa ya Maoni haya kwa wakati. Baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuridhia hoja hii ya Serikali kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Msemaji kutoka Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada huu, Mheshimiwa Lucy Owenya.

**MHE. LUCY F. OWENYA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA BIASHARA NA VIWANDA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa pumzi na kuendelea kunilinda na mabaya yote hata leo hii kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusiana na Muswada wa Sheria ulio mbele yetu. Aidha, nachukua fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwako na kwa Naibu Spika kwa kuliongoza Bunge hili la kumi, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote waliobahatika kuwemo katika Bunge hili la kumi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Mbowe kwa imani yake kwangu na hivyo kunipa jukumu la kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika Wizara hii ya Viwanda na Biashara. Shukrani zangu pia nazitoa kwa Naibu wake Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto kwa uongozi wao thabiti wa Kambi yetu na miongozo mbalimbali wanayoitoa kwa Mawaziri Vivuli.

Sambamba na hilo, natoa shukrani kwa Chama changu cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa kunitaua kuwa Mbunge. Naahidi kuwa nitaifanya kazi hii

kwa uaminifu mkubwa kwa manufaa ya Watanzania wote. Hakuna kulala mpaka kieleweke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa, ni kwa Mheshimiwa Mahmoud Mгимwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge Wajumbe wote wa Kamati ya Viwanda na Biashara kwa ushirikiano wao mkubwa walionipatia katika mchakato mzima wa maandalizi ya maoni haya ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa shukrani hizo, naomba kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria wa “*The economic zones Laws*” wa mwaka 2011 kwa mujibu wa kanuni za Bunge kanuni ya 53(6) (c) toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, Wakati Bunge lako Tukufu linatafakari mabadiliko haya ya sheria za *SEZ* na *EPZ*, ni vema kuangalia haja ya kuwa na mipango na namna ya kuona kama uwekezaji tunaofanya kwenye mipango hii ya *EPZ* na *SEZ* unashabihiana na tunachokipata kama nchi. Tafiti nyingi zimefanyika duniani toka mipango ya namna hii kuanza huko Ireland mwaka 1959 (*Irish Shanon Export Free Zone*) na zimeonyesha mashaka makubwa ya faida zipatikanazo na mipango ya namna hii. Kankesu Jayanthakumaran - mtafiti kutoka Idara ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha *Wollongong* huko Australia, katika makala yake aliyoiita *Benefit-Cost Appraisals of Export Processing Zones: Review of Literature*, aliyoitoa mwaka 2003 katika *Development Policy Review*, 2003, 21 (1):51-65 ameonyesha dhahiri kwamba nchi nyingi zinazoendelea bado hazifaidiki na mipango ya namna hii. Sababu kubwa aliyoitoa ni kutokuwepo kwa mahusiano (*linkages*) katika ya *EPZs/SEZs* na uchumi mpana wa nchi. Hapa Tanzania hatujapata tafiti ambazo zimefanywa na watafiti huru na kuona namna gani nchi inafaidika au kutofaidika na *EPZs/SEZs*.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ilieleze Bunge ni namna gani Muswada huu utasaidia malengo ya mipango ya *SEZ* na *EPZ* kufanikiwa kwa maslahi ya Taifa. Vinginevyo, tunatengeneza sheria ili kuendelea kufaidisha wawekezaji wachache ambao hawana faida kubwa kwa uchumi wetu badala ya kuelekeza nguvu kwenye kusaidia ukuaji wa uchumi vijijini ambako ndio kutaongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na Biashara. Kimsingi tunatengeneza ‘*enclaves*’ kwa kutarajia tu kuwa Watanzania watapata ajira na kuongeza mauzo nje, vipimo ambavyo havitoshi kuona nchi inavyofaidika na mipango hii. Kuna haja na ulazima wa kufanya ‘*impact study*’ ya *EPZs/SEZs* katika uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani baada ya kuupitia Muswada huu kwa makini, imebaini baadhi ya mapungufu ambayo yamekuwa yakipigiwa kelele na wananchi wengi na hasa jinsi tunavyopoteza raslimali nyingi kwa kuwathamini watu toka nje na hivyo kupelekea upendeleo wa dhahiri katika uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasema hivyo kwa kuangalia kifungu cha 5(a) na (b) cha Muswada kinachokifanyia marekebisho kifungu cha 13 cha sheria mama ya “*Export Processing zone.*”

Mheshimiwa Spika, katika *EPZ* na *SEZ* wawekezaji hupewa vivutio mbalimbali kama vile msamaha wa kodi ya mapato kwa miaka 10, msamaha wa kodi ya mapato kwenye gawio, riba na pango kwa miaka 10, msamaha wa ushuru wa forodha, *VAT* na kodi nyingine kwenye malighafi na mitambo ya uzalishaji ndani ya *EPZ*. Vivutio vingine ni kama msamaha wa ushuru unaotowwa na Serikali za Mitaa kwa miaka 10, kupewa dhamana ya Benki Kuu kwenye mikopo (*Export Credit Guarantee Scheme*). Kwa upande wa *SEZ* msamaha wa ushuru wa forodha, *VAT* na kodi nyingine kwenye malighafi na mitambo ya uzalishaji ndani ya *SEZ*, msamaha wa kodi ya zuio (*Withholding Tax*) kwenye riba ya mikopo na ukaguzi wa mizigo unaofanywa na *TRA* kufanyika katika *SEZ*.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kawaida, vivutio hivi vingetusaidia kupata faida kama watu wetu kupata ajira, viwanda vya ndani vilivyo nje ya *EPZs/SEZs* kupata soko la bidhaa (*raw materials*), malipo ya huduma kama Umeme, simu na kadhalika, baadhi ya kodi na hata mapato ya kigeni (urari wa biashara ya kimataifa). Kwa kuwa hakuna mahusiano au mahusiano ni madogo (*linkages*), faida tunayopata ni kidogo sana ukilinganisha na uwekezaji wetu kwenye kuendeleza maeneo haya na ruzuku tunayowapa kama vivutio vya kikodi.

Mheshimiwa Spika, wakati lengo la Muswada huu ni kuunganisha miradi miwili, yaani *EPZA* iliyoungwa mwaka 2002 na *SEZ* iliyoungwa mwaka 2006, tathmini inaonyesha kuwa miradi hii haijakidhi madhumuni ya kuanzishwa kwake. Malengo ya *EPZ* ya kukuza viwanda, kukuza mauzo nje, kuongeza teknolojia, kuunganisha bidhaa za Tanzania na masoko ya Kimataifa na kuhamasisha usindikaji wa mazao bado hayajafikiwa kwa kiwango kinachostahili na hailingani kabisa na nguvu kubwa iliyowekwa na Serikali katika mpango huu wa *EPZ*.

Mheshimiwa Spika, wakati *EPZ* imeanzishwa mwaka 2002 na sasa ni mwaka 2011, mchango wake kwa uchumi bado ni mdogo sana. Mpaka mwaka 2010 Mauzo nje yanayotokana na *EPZ* yalifikia thamani ya shilingi bilioni 700 ukilinganisha na jumla ya mauzo ya nje ya nchi ya ujumla ya shilingi trilioni nne katika kipindi cha mwaka 2009 pekee. Hii inaonyesha kuwa licha ya vivutio vinavyotolewa kwenye uwekezaji ndani ya *EPZ*, bado zaidi ya asilimia 85 ya mauzo yote ya nje Tanzania hayatokani na uwekezaji nje ya *EPZ*. Vivutio vinavyotolewa kwa *EPZ* ni kama vile msamaha wa kodi ya Mapato kwa miaka 10, msamaha wa *Withholding tax* kwenye gawio, riba na pango kwa miaka 10, msamaha wa kodi ya Forodha, *VAT* na kodi nyingine kwa miaka kumi na zaidi ya yote kupewa dhamana ya Benki Kuu kwenye mikopo (*Export Credit Guarantee Scheme*).

Mheshimiwa Spika, vilevile miradi ya *EPZ* na *SEZ* imekuwa ikisuasua. Kumekuwa na mazungumzo mengi ya miradi kuliko utendaji au hata Taifa kupata Taarifa kuhusu utendaji. Kwa mfano, mwezi Aprili, 2008, Rais wa China - Mheshimiwa Hu Jintao na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania – Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete walikutana na kujadiliana kuhusu miradi miwili ya *SEZ*. Mradi wa Mbegani - Bagamoyo *SEZ* ambao ungegharimu dola za Kimarekani bilioni mbili na mradi wa Kigoma *SEZ*. Mwezi Agosti, 2008, miradi hii iliwasilishwa kwa Benki ya Maendeleo ya

China (CDB). Hata hivyo, hakuna taarifa yeyote ambayo imetolewa kwa Taifa kuhusiana na miradi hii.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kwa miaka yote toka tuanzishe Sera ya Uwekezaji tumekuwa tukifanywa shamba la bibi na baadhi ya wawekezaji kutokana na vivutio hivyo ambavyo Kambi ya Upinzani inaviona kuwa ni mbinu ya kuiuza nchi yetu kwa wageni na kuwaacha Watanzania kuendelea kuwa masikini wa kutupwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maelezo hayo hapo juu yanaungwa mkono na mamlaka na kazi (*Functions and powers of Agent*) zitakazofanywa na Wakala ambaye katika Muswada huu ni *National Development Corporation – NDC*, imeainishwa katika marekebisho ya kifungu cha 5(2)(a) “... *acquire land in its name and lease or issue derivative rights to investors or erect thereon industrial and commercial buildings and lease such buildings to investors for undertaking thereon the Export Processing Zones licensed businesses.*” Aidha, kifungu cha 5(b) kinasema kuwa mamlaka itakuwa na uwezo, nanukuu: “...*to subcontract any person to execute any duty or perform any function provided for under subsection (2), and in particular, may license or enter into joint venture with private investors to develop Export Processing Zones Infrastructure.*”

Mheshimiwa Spika, vifungu hivi vinaitaka Mamlaka kutayarisha huduma zote zinazohitajika miundombinu yote hiyo ni kama maji, umeme na barabara ili mwekezaji aje na kuweka mitambo yake na aweze kuanza uzalishaji (*stand alone facilities*).

Mheshimiwa Spika, kwa maana ya kawaida ni kwamba Serikali itatengeneza mazingira yote yanayotakiwa ili mwekezaji aje kuweka mitambo yake na aanze uzalishaji. Japokuwa Serikali inakuwa imeingia gharama za kuhakikisha miundombinu yote inayohitajika kwa ajili ya mitambo ya uzalishaji kufungwa katika eneo husika, lakini bado mwekezaji huyo atapewa vivutio vya kutokulipa kodi kwa miaka 10 na vivutio vingine vingi vinavyolikosesha Taifa mapato.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inauliza: Je, gharama zote ambazo Serikali inazitumia katika kutayarisha miundombinu zinafidiwa vipi? Je, kama mwekezaji ataamua kufunga biashara kama ambavyo imeshatokea akiwa katika kipindi cha kutokulipa kodi hasara inarudi kwa Watanzania au inakuwaje? Ni kwanini gharama hizo zisiwe ndio mchango wa Serikali katika kutengeneza ubia na mwekezaji? Yaani Serikali kuwa na hisa sawa kwa sawa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona lingekuwa jambo la busara kama huduma hizi au vivutio hivi vingekuwa vinatolewa kwa wajasiriamali ambao wanapata mafunzo toka Shirika la Viwanda vidogo vidogo (*SIDO*). Kwa njia hii ungekuwa ndio mwanzo wa Watanzania kuanzisha viwanda vya kati na vikubwa na hivyo nchi yetu kuwa na mafanikio makubwa kwa kuwa na viwanda vya kati na vikubwa na hivyo kufikia lengo la Muasisi wa nchi yetu, hayati Mwalimu Julius K. Nyerere kutimia.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha (6) cha muswada kinachofuta kifungu cha 14 na kuweka kifungu kipya kinachounda Bodi, Wajumbe wa bodi inayoundwa na sheria hizi

mbili kifungu kipya cha 14(2) (j) na (k), Kambi ya Upinzani inauliza: Ni kwanini atajwe Mwenyekiti na Rais kwa asasi hizo badala ya kutajwa kwa mwakilishi kutoka katika asasi hizo? Aidha, Kambi inauliza kuwa asasi hizo zimeundwa kwa hiari na wahusika hivyo siku ushirika huo wa hiari ukivunjika sheria hii inasimama wapi?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa itakuwa vyema kama Muswada huu utatambua uwakilishi wa asasi za kiraia na Vyama vya Wafanyakazi na wao wawe ndio watakaolewa ni kundi lipi miongoni mwao linatakiwa liwakilishe wapi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inategemea ushauri tulioutoa utazingatiwa katika Muswada huu ili kukidhi haja ya kukuza uchumi kwa kusaidia wajasiriamali wadogo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, nashukuru kwa kunisikiliza na Mungu awabariki. kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupewa nafasi hii niweze nami kuchangia Muswada wa Sheria. Awali ya yote namshukuru Waziri mwenye dhamana ambaye ametoa Muswada huu na kuuwasilisha ndani ya Bunge lako Tukufu. Pili, nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara kwa maoni yake aliyotoa. Pia namshukuru Mwakilishi wa Kambi ya Upinzani ambaye ametoa mchango wake.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwa ujumla katika maeneo ya Muswada huu ili kuweza kutoa tija kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda tuangalie maeneo ya wananchi wanaotoka katika maeneo husika yatakayokuwa yamewekezwa. Daima wawekezaji wamekuwa wakilinda maslahi yao binafsi kuliko wale wananchi wanaokutwa katika maeneo hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge hakuna kusoma.

**MHE. MOSHI S. KAKOSA:** Mheshimiwa Spika, ni vizuri sheria ikaweka malengo ya kuandaa mazingira ambayo yatajenga nia halisi ya kumsaidia mwananchi husika.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ni vyema tukaliangalia kwa kina, tunapoandaa mazingira ya uwekezaji, lazima tujenge mikakati ya kuwalipa fidia wananchi ambao wataguswa katika maeneo husika. Wananchi wengi wanapofika wawekezaji, Serikali imekuwa ikiwatoa na kuwafukuza katika maeneo husika na wala hawatafutiwi maeneo ambayo wataendeleza shughuli zao za kiuchumi. Jambo ambalo ni hatari kubwa sana kwa wananchi wetu. Ni vizuri eneo hili likaangaliwa kwa kina. Kuna maeneo mengi sana yamejitokeza na bahati nzuri Mwasilishaji na Mwenyekiti wa Kamati hii ameeleza katika maeneo ya Mkoa wa Ruvuma maeneo ambayo yamejitokeza kwa wananchi kiasi kwamba kunatokea kutokuwa na imani na Serikali.

Sambamba na hayo yaliyojitokeza katika maeneo ya Mkoa wa Rukwa sasa hivi kuna vurugu kubwa sana kati ya wawekezaji na wananchi. Ni vyema maeneo haya tukayaangalia kwa kina ili tuepoke migogoro isiyokuwa na ulazima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunapounga mkono Muswada huu, ni lazima napo tuangalie vyombo vya Serikali ili viweze kushughulikia haraka urasimu usiokuwa wa lazima kama vile *TRA*. *TRA* wamekuwa wasumbufu sana hasa kwa Sheria wanazozitumia kuwabana hawa wawekezaji. Kupewa tu kibali inachukua muda mrefu sana. Kwa hiyo, ule urasimu nao ni lazima tuangalie kuutoa ili kuwajengea mazingira mazuri ya uwekezaji waweze kuwa na fursa hasa hawa wanaokuja kuwekeza katika kipindi hiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningependa zaidi ni kuwapa fursa wananchi ambao nao wana haki ya kuwekeza. Serikali inaweza kuelekeza mawazo kwa watu wa nje ili waweze kuwekeza. Lakini bahati mbaya hawa wananchi ambao wanahitaji kukuza uchumi wake wakapewa mgongo. Mimi nilikuwa naomba Serikali ijenge mazingira mazuri kwa wananchi ambao nao wanaweza wakawekeza. Leo hii uwekezaji mkubwa tunauonesha kwenye ardhi na ardhi ndiyo ambayo wanaitumia wananchi na kuitegemea wananchi wote.

Ni vyema Serikali ikajenga mazingira ya kuwapa nguvu hawa wananchi wa kawaida nao wakawa sehemu ya uwekezaji. Wapewe upendeleo maalum ili wawe na maeneo ambayo yatawasaidia wananchi wa Kawaida kukuza uchumi wao.

Mheshimiwa Spika, naomba niwasilishe na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi, nami nichangie hoja iliyoko Mezani. Awali ya yote, niwapongeze wale wote ambao kwa njia moja wameweza kuhakikisha kwamba hoja hii imetufikia Mezani siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, napenda nichangie mambo machache kulingana na suala zima la kuiongezea nguvu *SEZ* ili iweze kuleta ufanisi. Pamoja na kwamba leo tunafanya marekebisho ya Sheria hii ya *EPZ* ili kuweza kuipa nguvu *SEZ*, lakini kuna mambo kadhaa ya msingi ambayo yangefanyiwa kazi, tungeweza ku-*revisit* hii Sheria nzima ya *EPZ* ili kuweza kuongeza tija katika Taifa letu la Tanzania.

Marekebisho haya ambayo tunayafanya leo kwa mtazamo wangu mengi yao naona ni madogo sana ambayo sidhani kama yanaongezea tija kubwa sana katika kuleta ufanisi. Suala la kuweka Bodi kuondoa Baraza, suala zima la Mamlaka ya Usimamizi wa *SEZ* badala yake isimamiwe na *EPZ* bado kwangu mimi naona ni madogo, lakini kuna yale ya msingi ambayo ni vyema pia tukayapitia upya ili kujitathimini kama Taifa tangu tumeanza mpaka leo hii tumefaidika kwa kiwango gani na huu uwekezaji katika *EPZ* na mapungufu yako wapi ili kuweza kuongezea tija Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano tunaona kabisa tumeweka vivutio mbalimbali kwa wawekezaji hasa wa nje ili waweze kuwekeza, lakini vivutio hivi vimekuwa vinawa-

*favour* zaidi na kusababisha Taifa letu kukosa mapato mengi ya msingi. Tunaambiwa kwamba *EPZ* inatoa vivutio kwa mfano kuna misamaha ya kodi ya mapato, kuna misamaha ya mapato katika gawio, kuna misamaha ya pango wasiweze kulipa riba halafu wanapewa muda mrefu miaka kumi kitu ambacho kwa kweli kinalikosesha Taifa letu pato kubwa ambalo lingesaidia katika ukuaji wa uchumi katika Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nadhani kama tungewekeza kwenye kuandaa mazingira mazuri, miundombinu ya kuhakikisha kwamba wawekezaji hawa wanaweza kuwekeza katika Taifa letu, basi hakuna sababu ya kuwasamehe kodi hizi kwa muda wote huu wa miaka kumi na badala yake wawekezaji wa ndani ndiyo wangepewa misamaha hii ili kuweza kuwapa motisha waweze kuwekeza na tuweze kuwa na wawekezaji wengi wa ndani kuliko wawekezaji wa nje.

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa kwamba kama tukiweka mazingira mazuri, mwekezaji yeyote atawekeza tu ndani kwetu, hatashindwa kulipa kodi ya pango, hatashindwa kulipa kodi ya mapato. Nchi za wenzetu wapo ambao wanafanya hivyo, kukiwa na mazingira mazuri, *automatically* atakwenda kuwekeza kwa sababu mazingira yaliyoko katika nchi ile yanafanya akawekeze. Kunakuwa kuna ushindani wa biashara, kuna soko zuri, kunakuwa na suala zima la mahitaji ya umeme kama yapo ya kutosha, kama kuna maji ya kutosha, miundombinu iko mizuri, mwekezaji atawekeza na vile vile ataweza kulipa kodi kwa kulingana na sheria ambazo zimewekwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tupitie upya Sheria hii ili tuondoe misamaha ya kodi kwa kipindi chote cha miaka kumi. Hata kivutio hiki cha kuwa dhamana, tunawadhamini kwenye Benki Kuu hawa wawekezaji na wengine wanashindwa kulipa, matokeo yake nchi inaingia hasara ya kulipa deni hilo, ni lazima pia tulipitie kwa mara nyingine tuone tunafanyaje. Katika kufanya hivyo, tukiboresha mazingira mazuri ya kazi, naamini kabisa wawekezaji watawekeza kwa wingi na hatimaye malengo ya *EPZ* yatafikiwa, kwa sababu mpaka sasa malengo yetu hayajafikiwa kwa kiwango tunachotaka. Lengo lilikuwa ni kuongeza mauzo ya nje katika Taifa letu la Tanzania, lakini bado tunaona hali iko chini. Taarifa zinaonyesha kwamba Tanzania inapata shilingi bilioni 700 peke yake ukilinganisha na shilingi trilioni nne ambazo zinatokana na mauzo ya nje. Kwa hiyo, bado ni asilimia ndogo sana kulingana na vivutio ambavyo tunawapa wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, vile vile malengo mengine ya *EPZ* ilikuwa ni kukuza viwanda vyetu, lakini bado viwanda vyetu viko katika hali duni, tumeona uzalishaji ni mdogo, hata maslahi ya wafanyakazi vile vile ni madogo. Kwa hiyo, nashauri, pamoja na kwamba leo tunafanya marekebisho ya sheria hizi, lakini kuna masuala ya muhimu tuweze kuyapitia tena ili kuweza kuleta tija katika Taifa letu la Tanzania na ili kuweza kuongeza ufanisi katika *EPZ* pamoja na *SEZ* ili Taifa letu liweze kuongeza mapato yake kupitia *EPZ* pamoja na *SEZ*.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.



**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hatari ninayoiona, wakati tunajadili mambo kama ya hotuba za bajeti, huwa tunaweza kuogelea sana. Lakini hapa ni Muswada mahsusi, kwa hiyo, msianze kwenda nje kabisa mnakokutafuta nyie. Muswada mahsusi, sasa tunajaribu kuuboresha hapa, ndicho hasa tunachotakiwa kujadiliana hapa na hii ni kwa mujibu wa Kanuni zetu.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia katika Muswada huu wa *The Economic Zones Laws* wa Mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, kwa ufahamu wangu *EPZ* na *SEZ* zote bado hazijakidhi mahitaji ya Watanzania walio wengi. Pamoja na kwamba tutakuja na *EPZA* ambayo itasaidia kuendesha mipango hii miwili ambayo ina mwingiliano, lakini mimi bado nina mashaka makubwa kuhusu maendeleo ya Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Spika, mpango huu unaegemea kuwapa misamaha ya kodi wawekezaji kutoka nje na matokeo yake Taifa letu linapoteza pato kubwa sana. Juzi juzi katika kikao cha Kamati yetu ya Fedha na Uchumi, tulibaini kwamba *TRA* imepoteza mapato makubwa sana kutokana na mipango hii ambayo inaegemea kuwakumbatia wageni.

Mheshimiwa Spika, ni kweli nakubali kwamba *EPZA* itachangia katika kukuza uchumi wa Taifa letu. Lakini, hatuwezi kuwa na uchumi unaokua lakini tukawa hatuna *sustainable human development*. Wananchi wetu wa kawaida hasa wale wa vijijini, maisha yao yanaendelea kudidimia pamoja na kwamba tunadai uchumi wetu unapanda.

Mheshimiwa Spika, itakuwa ni jambo la busara na muhimu kuangalia maeneo ambayo ni nyeti na yana manufaa katika Taifa letu. Ili tuweze kuwakwamua wananchi walio wengi, Watanzania walio wengi wakiwemo vijana, ni lazima mpango huu uelekeze nguvu katika kilimo na siyo kilimo tu, ni lazima tuzingatie kuingia katika kilimo cha *horticultural products* ambazo zinaingiza vitu kama mboga za majani, vitunguu, matunda, mazao ambayo yanachukua muda mfupi kabla ya kupatikana. Endapo mpango huu utalenga katika hizo *horticultural products*, vijana wetu watapata fursa ya kuzalisha mazao ambayo hayachukui muda mrefu, ambayo yatawasaidia katika mahitaji yao ya kila siku na vile vile yatawasaidia kujikwamua kiuchumi kwa kuuza mazao yao haya.

Mheshimiwa Spika, ni lazima tuzingatie hali halisi ya dunia. Mipango hii yote itakapolenga kwenye sekta ya kilimo, ni lazima watazame kwa umakini na undani wake kilimo cha umwagiliaji (*irrigation system*) kwa sababu hii itatuwezesha kuepuka madhara ambayo yanaweza yakajitokeza kwa sababu ya ukosefu wa mvua.

Mheshimiwa Spika, mipango hii imeletwa kwa ajili ya kutunufaisha wote kwa pamoja pande zote mbili; wawekezaji na sisi Watanzania. Lakini, jambo la kusikitisha ni kwamba mipango yote ambayo imekuja kwa mtindo huo wa *EPZ* ikiwemo *AGOA* ambayo ni kutoka Marekani, ikiwemo ya *EBA* ambayo imeletwa na *European Union*, nasikitika kusema kwamba mipango hii yote imekuwa ikiwanufaisha zaidi wageni.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika na sisi tuwe na maamuzi kama nchi ya kuchagua na kuamua wanaokuja kuwekeza nchini wawekeze maeneo gani. Nasema hivyo kwa sababu natambua kabisa na najua kuna nchi ambazo ukienda una mahitaji ya kuwekeza watakwambia moja kwa moja kwamba sisi mahitaji yetu ni kwenye kilimo na tena mahitaji yetu ni Vijijini na siyo Mjini.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, ninavyoona mipango hii haina tatizo endapo itazingatia matakwa ya Watanzania wote nchi nzima wakiwemo wananchi wangu wa Jimbo la Kwimba.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Wewe Mbunge wa Kwimba? Wewe Viti Maalum! Tunaendelea na Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto. Mheshimiwa Kabwe simuoni. Mheshimiwa Mansoor S. Hiran, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla. (*Kicheko*)

**MHE. MANSOOR S. HIRAN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa meza yako kuniruhusu mimi nichangie Muswada huu. Mheshimiwa Spika, leo ni mara yangu ya kwanza nachangia Muswada kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nishukuru wananchi wa Jimbo la Kwimba kwa kunichagua na kunituma hapa niwawakilishe. Huyu mwenzangu si Mbunge wa Kwimba, naomba hilo lirekebishwe.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, taarifa!

**SPIKA:** Taarifa! Mheshimiwa ukae.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge, akanushe kauli yake, kwani mimi ni mkazi wa Jimbo la Kwimba na vile vile ni Mbunge wa Viti Maalum.

**SPIKA:** Mheshimiwa, ahsante. Hiyo taarifa nitaijibu mimi. Wewe ni Mbunge wa Viti Maalum, siyo Mbunge wa Kwimba. (*Makofi*)

**MHE. MANSOOR S. HIRAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nichukue nafasi hii pia kipekee kushukuru familia yangu na marafiki zangu ambao walikuwa bega kwa bega kwenye mchakato wa uchaguzi na kuhakikisha kwamba ushindi unapatikana.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nichukue fursa hii kukishukuru Chama cha Mapinduzi kwa kunipa tiketi ya kugombea Ubunge Jimbo la Kwimba na ushindi umepatikana wa kishindo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara kwa kuleta Muswada huu. Muswada huu umefika muda muafaka, mimi nauunga mkono.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mchango wangu wa kuboresha Muswada huu. Nashauri Serikali iweze kufanya tafsiri ya Muswada huu kwa Kiswahili ambayo ni Lugha ya wananchi wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningeshauri pia Serikali ifanye maandalizi au Wizara ifanye maandalizi ya kuzunguka nchi nzima, wananchi wengi nchi nzima hawafahamu huu Muswada au hii Sera ya *EPZA* inawanufaisha vipi kiuchumi. Kwa hiyo, ningeeomba watangaze, wapeleke taarifa zote Mikoani ili huko nako pia wananchi waelewe.

Mheshimiwa Spika, hii Sera ikipelekwa vizuri Mikoani, vijana watapata ajira, nchi itanufaika. Kwa hiyo naomba hilo nalo waliangalie.

Mheshimiwa Spika, kwenye Muswada huu wamesema wanaunda *Board (Export Processing Zone Authority Board)*. Nashauri kwenye hiyo *Board* uwakilishi wa Mikoa uwepo kwa sababu nimeona kuwa hakuna uwakilishi wa Mikoa; ni Waziri, Makatibu Wakuu wa Wizara mbalimbali, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Kamishna wa Ardhi na *TRA*. Sijaona unawakilishi wa Mikoa, ningeshauri kwamba Mikoa ambako wanataka kuanzisha hizo *Zones* nayo iwakilishwe kwenye hizo *Board*.

Mheshimiwa Spika, pia kuna hoja hapa amesema kwamba Waziri mwenye mamlaka atatwaa ardhi ya wananchi. Kwenye suala hilo nashauri kwamba, wanapotwaa ardhi ya wananchi huwa kuna sera za kuandika barua na kumwambia mwananchi kwamba eneo hili linatwaliwa na Serikali kwa sera mbalimbali kwa hiyo asiendeleze. Naomba Serikali inapoamua kutwaa ardhi ya mwananchi ilipe fidia ili huyo mwananchi aweze kwenda sehemu nyingine akajiendeleze, asizuiliwe kuendeleza eneo na huku hajui lini Serikali itamtoa pale.

Mheshimiwa Spika, hayo machache ndio nilikuwa nataka kuyachangia katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia masuala kadhaa kuhusu Muswada ulioko mbele yetu. Kwanza, niseme kwamba Muswada huu unahusu kwa kiwango kikubwa sana wananchi wa Jimbo walionituma kuja kuwakilisha ndani ya Bunge hili Tukufu, kwa sababu kati ya maeneo ya uwekezaji wa *EPZ*, Ubungo ina maeneo mawili makubwa: Ina eneo la Benjamin Mkapa *SEZ* ambayo iko pale Mabibo Makuburi ambayo ndiyo Makao Makuu vilevile ya hii Mamlaka, lakini na eneo vile vile la Hifadhi *EPZ* ambao ni uwekezaji chini ya *NSSF*. Kwa hiyo, kati ya Wabunge ambao wanaweza kuzungumza kuhusu faida na athari za huu mfumo mzima, na mimi ni mmojawapo.

Mheshimiwa Spika, la pili, niseme tu toka mwanzo kwamba siungi mkono hoja hii. Siungi mkono siyo kwa sababu sipendi maendeleo ya wananchi wa Jimbo langu, Jimbo ninalotoka, Jimbo walilonituma, Jimbo letu la Ubungo, bali kwa sababu leo tunakwenda kufanya kazi nusunusu. Ukisikiliza maoni yaliyotolewa na Kamati, pamoja na kuwa Kamati mwishoni imekwenda kutamka kwamba inaunga mkono hoja, lakini utangulizi wa uchambuzi wa Kamati unaashiria kwamba Muswada huu ulipaswa kurejeshwa ukafanyiwe marekebisho makubwa kwa sababu msingi ambao Waziri amezungumza kwenye utangulizi wake ni maagizo ya Kikao cha Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, ukisoma katikati ya mstari maagizo ya Kikao cha Baraza la Mawaziri na hata uchambuzi wa Kamati unaashiria kwamba kulipaswa kuwa na mabadiliko makubwa sana kwenye hii sheria ambayo yangehusisha moja kwa moja kuunganisha moja kwa moja hizi sheria mbili badala ya kufanya marekebisho madogo. Sasa katika mazingira haya ya sasa, naamini katika Bunge hili, katika Kikao hiki ni vigumu sana kuweza kukamilisha yale marekebisho makubwa sana ambayo Kamati imeyapendekeza, Kambi ya Upinzani imeyapendekeza na ndiyo msingi wa mapendekezo ya Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, lakini, pamoja na kuwa siungi mkono hoja, naomba nichangie maeneo kadhaa kuhusiana na Muswada huu. La kwanza, Muswada unapendekeza kwamba kuundwe Bodi na Bodi hii iwe na Mwenyekiti ambaye ni Waziri. Kwa muundo wa namna hii, uwajibikaji wa mamlaka ambayo vile vile iko chini ya Wizara hiyo ambayo Mwenyekiti wake wa Bodi ni Waziri, kimsingi kutakuwa na tatizo sana la namna ya usimamizi na mamlaka na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama tulivyoona kwamba miaka mingi imepita toka 2002 mpaka 2011, tija ya mfumo huu haijapatikana vya kutosha, ndivyo ambavyo kwa muundo huu tunaopitisha leo, tija inaweza isipatikane muda mrefu kwa kwenda mbele. Kwa hiyo, kama Serikali inaweza kufanya marekebisho ya haraka kwenye Muswada huu kwa kuzingatia haya maoni basi inaweza ikatupa tija.

Mheshimiwa Spika, lakini, ukiangalia Wajumbe wa Bodi vile vile, kuna wadau wengine wa msingi ambao wangepaswa kuingia kwenye Bodi. Bunge lako Tukufu lilifanya hatua moja sahihi kabisa ya kuunganisha vyombo mbalimbali vya Kiserikali, *Board of External Trade* na *Board of Internal Trade* kutengeneza chombo cha kusimamia masuala ya kibiashara. Kimsingi mifumo hii yote inahusu biashara ya Kimataifa, biashara ya mauzo ya nje. Ni busara sana vyombo kama hivi ambavyo na vyenyewe vimeundwa kwa Sheria ya Bunge ikiwemo Kituo cha Uwekezaji, vikawa na uwakilishi mzuri katika Mamlaka hii inayoundwa.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo limesemwa na Kamati, lakini nimepitia *schedule* ya *amendment* ya Serikali sijaliona na ni jambo zito kidogo. Kuhusu mgongano baina ya Sheria hii tunayoitunga sasa hivi juu ya mamlaka ya Waziri wa Ardhi na kadhalika *versus* sheria nyingine ambazo Bunge lilitunga Sheria ya Ardhi ya Vijiji na Sheria za Uwekezaji. Jambo hili ni zito nilitarajia kwamba kwenye *schedule of amendment*, Serikali ingezingatia kwa ukamilifu wake hii hoja na ndiyo maana nasema siungi mkono hoja

kwa sababu nilitarajia Serikali ingeyachukua haya yote, ambayo vile vile Kamati imeyasema na kuyaingiza.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba kama tutapitisha marekebisha haya leo, bado tunahitaji kama Taifa kwenda kufanya uchambuzi kwa kina sana kuhusu mfumo huu wa *SEZ*. Kwa mujibu wa taarifa za Kiserikali, mtaji ambao umewekezwa kwenye *EPZ* na *SEZ* mpaka hivi sasa, ni dola za Kimarekani milioni takribani mia sita. Kwa thamani ya sarafu yetu inavyoporomoka sasa hivi, naweza kusema hii ni takribani trilioni moja imewekezwa kwenye masuala ya *EPZ* na *SEZ*.

Mheshimiwa Spika, lakini ukiangalia matokeo, wenzangu wamezungumzia matokeo kwa upande wa mauzo ya nje, tuangalie matokeo kwa upande wa utengenezaji wa ajira, kwa mujibu wa takwimu za Serikali yenyewe, ajira za moja kwa moja zilizotengenezwa kupitia mfumo huu, ikiwemo ajira za baadhi ya watu wachache wa Dar es Salaam ni ajira elfu kumi tu. Sasa kama umetumia trilioni moja kama mtaji ulioingia kutengeneza ajira elfu kumi ni sawasawa na wastani wa shilingi milioni mia moja kwa kila ajira moja. Sasa kama unatengeneza ajira moja kwa kutumia milioni mia moja maana yake ni kiwango kikubwa sana. Yaani hata wangeamua tu kwamba sasa hizi milioni tuwape wajasiriamali wadogo wafungue viwanda, tungeweza kufungua viwanda vingi sana na vikapeleka mauzo mengi sana nje na tungetengeneza ajira nyingi sana. Nazungumzia kwa kuangalia takwimu za Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninachoomba kwa chochote kile kitakachopitishwa lakini mwisho wa siku tunapaswa tufanye tathmini kama Taifa, kuangalia lengo letu la mfumo huu ni nini. Thailand walipoamua kuingiza mfumo wao wa namna hii *EPZ* na *SEZ* walilenga kuhamisha viwanda kutoka Bangkok kupeleka nje ya Mji, hilo ndilo lilikuwa lengo lao, watu kama Malaysia walipoanzisha mfumo kama huu walilenga kuingia kwenye soko la Kimataifa, wengine walianzisha mifumo kama hii kutafuta mitaji. Sisi kama Taifa tunaamua kuanzisha mfumo wa *SEZ* na mfumo *EPZ* kwa sababu gani hasa? Lengo letu la msingi ni lipi, ili sheria tunayotunga *i-reflect* kwamba haya ndiyo matakwa ambayo tunataka kuyafikia kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, niendeleo kusema kwamba siungi mkono hoja hii na natarajia kwamba mamlaka itakayoundwa kama sheria itaendelea kufanyiwa mabadiliko kama ilivyo, itafuatilia kwa umakini sana *SEZ* ya Benjamin Mkapa *SEZ* ya Mabibo iliyozinduliwa na Rais mwaka jana, mpaka sasa hivi ni kiwanda kimoja tu mle ndani ambacho kinafanya kazi kwa ukamilifu wake, lakini ukiangalia eneo la ekari 65 na *incentives* za kodi na kila kitu wananchi wakipita wakiona yale majengo yapo pale Ubungo, wanaona kwamba hapa kuna tija kubwa sana, lakini ukiangalia matokeo ni madogo. Kwa hiyo, mamlaka itakayoundwa ikafanye tathmini zaidi. Iangalie namna ya kuunganisha dhamira hiyo ya kuuza bidhaa nje, ya kutoa motisha ya kodi na kadhalika na uendelezaji wa wafanyakazi. Wananchi kwa mfano wa Makuburi Ubungo wanalalamika sana kwamba kuna *EPZ*, kuna viwanda mle, kuna geti kubwa pale nje hata ajira zinavyotolewa kwa namna ambayo wanaozunguka lile eneo wanaweza kunufaika na vitu kama hivyo. Ni mambo ambayo yanahitaji mjadala wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tunasema kwamba *SEZ* ya Ubungo pale, taarifa za Kiserikali na nirudi kwenye hoja za marekebisho za Muswada huu, taarifa zinaonesha kwamba moja ya tija ambayo Serikali imeifanya ni kuweka vizuri miundombinu ya barabara, maji na kadhalika. Lakini ukitoka nje ya geti la *SEZ* pale Makuburi, utakuta wananchi wa Mwongozo, Makuburi, Kibangu, majirani pale wana shida kweli ya maji mpaka wananchi wanafika hatua wanaanza kufikiria huu uwekezaji uliojengwa hapa ndiyo umefanya maji ambayo yalikuwa yanatoka kwetu sasa yanapelekwa kwenye viwanda, wananchi wanakosa maji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasema pamoja na kufanya marekebisho ya vifungu vingine ni lazima kuhakikisha kwamba *EPZ* na *SEZ* zinakuwa na vifungu ambavyo vina-*provide* mfumo wa kuwa na *corporate social responsibility* ya kiwango cha kutosha sana kwa Serikali yenyewe kama Mbia wa miundombinu hii inayowekezwa, lakini vile vile kwa makampuni ambayo yanawekezwa ndani ya mifumo hii. La sivyo nia njema ya mifumo kama hii inaweza isitimie.

Mheshimiwa Spika, nisisitize tu kwamba, pamoja na uwekezaji wa maeneo haya kwa kuwa tunalenga sasa kwenda mbele, ni vizuri Sheria hii ikaenda sambamba na kuongeza kasi ya uwekezaji wa miundombinu. Najua *SEZ* ya Benjamin Mkapa haina tatizo kubwa la maji kama ilivyo *EPZ* ya *Millenium Park*, lakini ni lazima kuyatazama haya mambo kwa upana wake ili mwisho wa siku tija stahili iweze kutimia kwa mifumo hii ambayo inapendekezwa.

Mheshimiwa Spika, niliombe Bunge lako Tukufu kwamba nashukuru kwa kazi nzuri sana ambayo Kamati imefanya. Kwa kweli Kamati imeainisha ya msingi na Kambi ya Upinzani imeainisha mambo ya msingi, sasa kwa mambo haya yaliyoainishwa sioni ni kwanini tuwe na haraka sana ya kuititisha sheria bila kufanya marekebisho haya makubwa ya msingi yaliyopendekezwa kwa sababu *schedule of amendment* ambayo imeletwa na Serikali haikuzingatia kwa ukamilifu wake hoja za msingi sana ambazo zimetolewa na Kamati na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sioni kama kuna uwezekano kwa muda tulionao na leo tuna Miswada miwili ya *miscellaneous*, sioni kama kuna uwezekano kwa leo peke yake hivi vifungu vyote vilivyoelezwa na Kambi ya Upinzani, vilivyoelezwa na Kamati vikabadilishwa haraka sana na Serikali kwa muda huu mfupi wakatuletea *schedule of amendment* nyingine yenye kuzingatia maoni haya ya msingi. Kwa sababu hiyo basi nashauri Bunge lako Tukufu kwamba mtoa hoja atakapokuja kuhitimisha hoja yake, pengine hoja hii arejee kutoa muda wa ziada ili kuweza kufanya hayo marekebisho ya msingi yanayozingatiwa.

Mheshimiwa Spika, niendeleo kuisitiza umuhimu wa kutenganisha kati ya kazi za kiseri na kazi za kiutendaji, ukiangalia hii Bodi tunayoiunda leo ni ya mamlaka, Bunge lako Tukufu limekwishapitisha sheria nyingi sana za mamlaka nyingine, ukitazama miundo ya mamlaka nyingine ambayo tumepitisha Bodi zake, hukuti sana mamlaka ambazo watendaji wa Kiserikali na Viongozi wa kiseri wa Kiserikali ndiyo wasimamizi hasa wa zile Bodi. Lakini kwa sheria hii hii ipo kwa kiwango kikubwa sana,

kuanzia Mwenyekiti na kuendelea. Sasa hii *principle* nadhani tukiipitisha inaweza ikafanya hii bodi isifanye kazi yake ipasavyo halafu mwisho wa siku tutajiuliza ni nani ataiwajibisha Bodi kama Waziri mwenye dhamana ni Mwenyekiti wa Bodi hiyo hiyo ya mamlaka hiyo hiyo. Kwa hiyo, haya mambo ni vizuri yakafanyiwa marekebisho makubwa ili vile vile kupunguza mianya.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. DR. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie mawazo kidogo kwenye Muswada huu. Kwanza, napenda kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu wakati huu. Nasema Muswada huu umechelewa zaidi kwani ulitakiwa kuja mapema kabisa. Kwa sababu nia njema ya kuwianisha utendaji wa mamlaka hizi mbili ulikuwa ni wa msingi sana kwa maana ya kupunguza gharama za uendeshaji wa shughuli za Serikali, lakini vilevile kuwianisha na kuondoa maeneo ambayo kungeweza kuwa na upinzani au mgongano katika utendaji wa shughuli ile ile iliyokusudiwa. Kwa hiyo, nawashukuru sana Serikali kwa kuuleta Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, vile vile nafikiri ni vizuri tukafahamu hali ya ushindani wa kibiashara uliopo katika dunia, lakini hata katika Kanda yetu ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, tunapokuwa tunashiriki kama nchi ni vizuri tukaelewa kwamba, tunashindana na ni lazima tuweke misingi ya kutufanya tuweze kushindana vizuri. Muswada huu unatuwekea misingi hiyo muhimu sana ili tuweze kushindana na wenzetu katika Kanda hii ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kijiografia tumekaa vizuri sana, tumezungukwa na nchi takriban nane ambazo ni masoko mazuri sana ya kibiashara, lakini wakati mwingine tunashindwa kuyatumia vizuri kwa sababu hatujaweka taratibu na miundombinu. Muswada huu unatupeleka sasa kutuwekea misingi na miongozo ya kuweza na sisi tukashindana na tukalitumia hili soko kubwa la Kanda ya Mashariki ya Afrika kwa uzuri zaidi na Taifa likanufaika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafikiri wakati hii mamlaka inatengenezwa katika sheria hii tutakayoipitisha, ni vizuri wakaangalia sana maeneo ambayo yapo *strategic* katika kutenga maeneo haya ya uwekezaji na maendeleo ya kiuchumi. Maeneo yetu ya mipaka, karibu nchi zote zinazotuzunguka zina mahitaji maalum kutoka ndani ya nchi yetu na bidhaa nyingi ambazo tumekuwa tukiuzwa kwenye nchi hizi za jirani zinakuwa hazijafanyiwa *processing*. Matokeo yake ni kwamba mapato yanakuwa ni kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafikiri kwamba, wakati mamlaka hii inaundwa ijielekeze kwa kushirikiana labda kwa karibu sana na Halmashauri za Wilaya kubainisha maeneo ambayo nchi yetu inaweza ikanufaika kwa ukubwa zaidi. Maeneo yakipimwa, viwanda stahili vikajengwa, kwa mfano, nchi jirani ya Kenya mara nyingi imekuwa ikihitaji sana nafaka kutoka kwetu lakini nafaka hizo zinakwenda kama zilivyo, sasa maeneo ya mipaka kama yangeweza kuwekezwa viwanda vinavyoendana na uboreshaji wa nafaka hizo na *packaging* ni sahihi. Nina hakika kwanza tungetengeneza ajira zaidi,

Taifa lingepata mapato kwa maana ya kodi ya ndani ya nchi lakini pia kwa fedha ya kigeni kutokana na bidhaa za namna hiyo. Bidhaa hizo zipo za aina mbalimbali, kuna mahindi mengi kule Sumbawanga ambayo yangeweza kuwa *processed*, vile vile yanahitajika Zambia.

Mheshimiwa Spika, maeneo haya yangeweza vile vile kuwa na kitu wanaita *multiplier effect* kama uwekezaji huu ungefanywa, kwa sababu unapopima kujenga viwanda katika maeneo hayo ni lazima muweke zile *supportive facilities*, kwa mfano, mahoteli, *lodges*, hospitali, shule, maduka makubwa na *supermarkets*. Kwa sababu hali ilivyo sasa hivi, vitu kama mabenki unayakuta kwenye maeneo ya mipaka yetu, huduma ziko duni sana au hazipo kabisa. Unakuta hata wageni wanaokuja ndani ya nchi yetu kununua bidhaa wanapitia kwenye mipaka tu kama njia, hakuna, pesa inayobaki pale ndani ya nchi yetu zaidi ya kununua ile bidhaa ambayo wameifuata. Sasa hili naona ni eneo ambalo tunapoteza fursa na hivyo ni vizuri sana hii mamlaka inayoundwa na hii sheria tunayoipitisha ikaweka vipaumbele.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunazungumza kwamba *EPZ* na *SEZ* hazijaleta mapato makubwa kwa sababu hatujawekeza vya kutosha. Maeneo mawili tu tunayoyazungumzia ndani ya nchi hii ni kidogo sana kwa nchi hii ukiweza kulinganisha na uwezo wa mapato ambayo tungeweza kupata. Kwa hiyo, ni lazima tuwekeze na tuwekeze kwenye maeneo makubwa zaidi ili tuweze kupata manufaa yanayostahili kutokana na kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa ujumla Muswada huu ni wa msingi na mimi nauunga mkono kabisa kwamba ni vizuri tukaupitisha na kwa sababu utakuwa na manufaa makubwa sana kwa watu wetu na hasa kama utapanua maeneo ya kupanua kazi, isiwe tu Dar es Salaam lakini na maeneo yale mengine ambayo wameshabainisha kama Kigoma, lakini nasisitiza sana maeneo ya mipakani ni maeneo ya msingi sana yanaweza kuliletea faida kubwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika ahsante, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia Muswada huu ambao upo mbele yetu na nitachangia kwa kifupi sana. Kwanza, naipongeza Kamati kwa kazi nzito ambayo wameifanya na mimi nikiwa mmojawapo kwamba Muswada huu ulikuwa umechelewa kufika.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna vitu ambavyo nataka tujaribu kuviongezea kuhusu masuala ya uwekezaji, ni vipi Watanzania wananufaika na uwekezaji huu. Hili suala wanatakiwa waliangalie kwa upana sana kwa sababu wawekezaji waliopo mpaka sasa hivi katika nchi yetu hii, hatujaona tija labda Muswada huu utakapopitishwa yawezekana tija ikaonekana. Mfano, leo wawekezaji wanakuja kwenye nchi yetu lakini wazawa hawashirikishwi. Nitatoa mfano, ukienda kama vile Dubai ukitaka kuwekeza ni lazima wewe mwekezaji ushirikiane na mzawa. (*Makofi*)



Mheshimiwa Spika, leo sisi wawekezaji wetu wanakuja wanawekeza, hawawashirikishi wazawa. Pia tukiangalia hata kwenye kusajili, usajili wa wawekezaji ama makampuni usajili wake pia ni ubabaishaji. Nasema hivyo kwa sababu unakuta kampuni inakuja kusajiliwa majina yamepangwa kama ni majina matano, sahihi zinawekwa pale, lakini ushahidi kama vile picha haupo. Nchi zingine wanaweka mpaka picha kwenye usajili wa makampuni.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na makampuni ya ubabaishaji, nasema hivyo kwa sababu gani. Kwetu Wilaya ya Geita kuna makampuni mengi ambayo yamezunguka ama yapo katika Wilaya hiyo lakini ukiangalia wazawa hali yao ni mbaya sana, kwa sababu wawekezaji hawakuwashirikisha wananchi. Hawako ndani pale hata ajira zimekuwa ni duni sana. Wananchi hawapati ajira eti kwa sababu wawekezaji wapo pale lakini wananchi hawafaidiki. Tunaomba sheria hii ipitishwe kwamba Wawekezaji lazima wanapotaka kuja kuwekeza na wazawa wawe wako ndani.

**SPIKA:** Hii ni *EPZ* siyo ile ya uwekezaji wa kawaida.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** *Okay*, basi nimesema kwamba nachangia kwa uchache kwa sababu nimeshtukizwa, pamoja na kwamba nimeomba. Lakini nasema kwamba wawekezaji tuwatengenezee mipango iliyo mizuri, tuwaandalie maandalizi kama haya ambayo yamewekwa ndani ya utaratibu wa Muswada huu. Lakini jambo la kuongezea hapo ni kwamba Wazawa na wao wapewe kipaumbele ili waweze kufaidika pamoja na huo uwekezaji. Wawekezaji wanapokuja wananchi wawepo ndani, ajira ipatikane ili tuweze kuona faida ya uwekezaji, siyo wawekezaji wanakuja, wanakamua na Watanzania hawafaidiki na huo uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo nasema kwamba hoja hii naiunga mkono, ahsante.  
(*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ndiyo maana mara nyingine wengine wakiandika vikaratasi vyao vidogo vidogo wanachana kwenye daftari wananiletea kuomba kuchangia nakataa, kwa sababu tuna fomu zetu za kuomba kuchangia, hizi zinaandikwa namba, ukishaomba tunajua ni nani aliwahi na nani akafuata, sasa mkiandika na kusema nimewashtukiza inakuwa siyo sahihi kwa sababu hakuna fomu uliyoandika. Kwa hiyo kama hujajiandaa siyo vizuri kuomba.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kidogo Muswada huu wa Mabadiliko ya Sheria za Maeneo Maalum ya Kiuchumi. Naomba radhi kwamba wakati umeniita sikuwepo nilikuwa kwenye *Press Conference* na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya hesabu zinazoishia Juni 2010.

Lakini pili, kabla ya kuchangia tumepata taarifa kwamba baadhi ya Wabunge, wenzetu katika Bunge hili wamepata fursa ya kutumikia vyama vyao. Tumepata taarifa kwamba Mheshimiwa Mwigulu, Mbunge wa Iramba amekuwa Katibu wa Fedha wa Chama cha Mapinduzi na Mheshimiwa Januari Makamba na wengine. Nimewataja hao

kwa sababu ni vijana wenzangu na kwa kweli tunafurahi sana tunapoonza kwamba vyama vya siasa vinatoa fursa kwa vijana wao. Sisi CHADEMA tulianza mapema nafasi kubwa za CHADEMA zinashikwa na vijana. Kwa hiyo, naamini kabisa Chama cha Mapinduzi kimeona huo ndio mwelekeo ambao unatakiwa kuwa na sisi tutawapa ushirikiano ambao watauhitaji maana yake lengo letu ni kuijenga nchi yetu ili iweze kuwa na maendeleo. Nawapongeza sana vijana wenzangu ambao wamepata fursa ya kutumikia chama chao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nina mambo mawili tu katika huu Muswada ulioko mbele yetu. Mengine Waziri Kivuli wa Viwanda na Biashara ameyazungumza katika taarifa yake. Jambo la kwanza mwaka 2002 ndio kwanza tulitunga Sheria ya *Economic Processing Zones* na kuunda mamlaka zinazotakiwa. Mwaka 2006 tukatunga Sheria *Special Economic Zone* na tukaipitisha hapa Bungeni. Natoka mwaka 2002 na 2006 mpaka sasa tumekuwa tukifanya mabadiliko mbalimbali katika Sheria hizi. Leo sasa tumekuja kufanya mabadiliko kwa ajili ya kuunganisha mamlaka moja kusimamia *Special Economic Zone* na vile vile kusimamia *Economic Export Processing Zones (EPZ)*.

Mheshimiwa Spika, lakini pia miaka miwili iliyopita tulitunga Sheria nyingine tena ya *Economic Development Zones (EDZ)*. Kwa hiyo, unakuta kwamba mfumo mmoja wa kuhakikisha tunaongeza uwekezaji katika uzalishaji wa mazao na hasa kuuza nje tumeutungia sheria tatu. Kila wakati tunakuja kuzirekebisha. Hii inaonyesha dhahiri kwamba, hatujiandai vya kutosha. Ndio maana ukiangalia takwimu ambazo Waziri Kivuli wa Viwanda na Biashara amezitoa kwamba toka tumeanza mipango hii mwaka 2002 mpaka sasa mauzo nje yanayotokana na mipango hii ni ya thamani ya bilioni 700 tu. Ukichukua *accumulation* ya mauzo nje kwa ujumla wake utaona kwamba tumeuza sana, mwaka 2009 tu peke yake tumeuza nje mazao ya thamani ya zaidi ya shilingi trilioni nne. Lakini kutoka mwaka 2002 mpaka sasa miaka tisa kutokana na haya maeneo maalum tumeuza bilioni 700 tu.

Mheshimiwa Spika, lengo hasa la haya maeneo maalum ni kuongeza ajira na kukuza mauzo yetu ya nje. Ndio maana tunatoa *incentives* nyingi sana katika haya maeneo. Nadhani imefikia wakati tufanye *review* ya hiki kitu tuweze kuona kama kinatusaidia au hakitusaidii. Ni kweli kabisa kwamba baadhi ya maeneo ya nchi zingine hasa nchi za Asia, *Export Economic Zones* imewasaidia sana. Malaysia, Singapore, Vietnam nako imewasaidia sana, lakini haina maana ya kwamba kama kule wamefanikiwa basi na huku lazima tutafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya maeneo ambayo yametengwa kwa muda mrefu, kwa mfano, Kigoma *Special Economic Zone*, imetengwa kutoka mwaka 2006. Nakumbuka nilikuwa Waziri Kivuli wa Uchumi mwaka 2006. Wakati wa bajeti tulitenga shilingi milioni 600 kwa ajili ya *SEZ* ya Kigoma. Mpaka leo hakuna kitu kinachoonekana. Sisi ambao ni Wabunge na viongozi tunajua, sijui kuna upembuzi yakinifu, kuna nini lakini mwananchi wa kawaida haelewi upembuzi yakinifu ni nini, haelewi sijui tathmini ni nini. Kwa hiyo, inabidi tufanye vitu ambavyo wananchi wataviona moja kwa moja na wanaweza wakafaidika navyo.

Mheshimiwa Spika, sasa nadhani pamoja na kwamba tunaangalia haya marekebisha ya Sheria kwa ajili ya kuondoa zile *abnormalities* na kuweza kurekebisha. Kwanza ushauri wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara kuihuisha pia na ile Sheria ya *EDZ* pamoja na hizi zingine zifanye kwa pamoja ili tuwe na sheria moja tu ambayo inasimamia masuala yote haya kwa umoja wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, sheria zetu hizi zinatoa vivutio sana kwa wawekezaji wanaowekeza kwenye haya maeneo hawalipi *cooperative tax* miaka kumi, hawalipi ushuru wa forodha miaka kumi, hawalipi *VAT* miaka kumi. Kwa hiyo, tunabakia na nini ambacho tunafaidika nacho, ni ajira na mauzo nje. Lakini ukiangalia *trend* kama nilivyosema kwenye *EPZ* toka tumeanza mwaka 2002 imetengeneza ajira 10,000 kwa wastani. Lakini toka mwaka 2002 mpaka sasa chukua sekta moja tu ya kilimo na iko nje ya *EPZ*, sekta ya Madini peke yake imetengeneza ajira 13,000 iko nje ya *EPZ*.

Kwa hiyo, kuna haja ya kuweza kuona hizi *incentives* ambazo tunazitoa kwenye maeneo ya *EPZ* kweli zinasaidia, kweli ndio zinazochoecha uwekezaji katika haya maeneo ajira ambazo zinazotengenezwa na bahati mbaya kwenye maeneo ya *EPZ* wafanyakazi wale hawaruhusiwi kuwa *unionist*, Vyama vya Wafanyakazi haviruhusiwi kwenye maeneo ya *EPZ*. Kwa hiyo, inawezekana kabisa kwamba hata hao watu 10,000 ambao wameajiriwa katika hayo maeneo bado kuna tatizo kubwa sana la ajira zisiwe ni ajira ambazo zinaweza kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba hili nilisisitize, sina tatizo kabisa na Muswada kama jinsi ambavyo Waziri Kivuli alisema na maoni yetu ambayo tumeyatoa. Lakini kuna haja kubwa sana na labda Serikali itoe *commitment* hapa Bungeni, kwamba tufanye *review* ya huu mfumo mzima wa *Special Economic Zone* na mfumo mzima wa *Export Processing Zones* kuona kama je, zinatusaidia? Hizi *incentives* tunazowapa kweli zinawavutia wawekezaji wakaja, je, hakuna haja ya kuangalia maeneo ya wafanyabiashara wadogo wadogo wenye viwanda vidogo vidogo tukawaandalia maeneo ya aina hiyo ya *EPZ* na *SEZ*. Watu wenyewe ambao watazalisha bidhaa ambazo zitaingia kwenye soko kwa sababu bahati mbaya zaidi ni kwamba bidhaa hizi ambazo zinazalishwa kwenye *EPZ* na *SEZ*, asilimia themanini ni *export*.

Mheshimiwa Spika, Nigeria wao wali-*break that rule* wakaamua kwamba pamoja na kwamba kuna bidhaa mtaweza kuuza lakini zingine zitaingia ndani ya soko la ndani kwa sababu kuna maeneo kutokana na jinsi ambavyo *economy* yetu bado haijawa *well integrated*, kuna maeneo ambayo bado hata bidhaa zinazozalishwa ndani hazifiki. Mfano, *cement* Kigoma, bei ya *Cement Dar es Salaam* ikiwa shilingi 10,000 Kigoma ni mara mbili yake. Kwa hiyo, tunaweza tukaruhusu watu ambao wanawekeza katika maeneo kwa bidhaa ambazo ni muhimu kwa wananchi sheria iache kwamba kama unazalisha *cement* katika eneo kwa mfano la *SEZ* ya Bagamoyo, basi uruhusiwe ile *Cement* kama unaipeleka Songea, Shinyanga, Kigoma ambako bei ya *Cement* ni kubwa mwaga kwenye

soko ili bei ya *cement* iweze kushuka. Haya ni baadhi ya maeneo ambayo tunaweza tukayaangalia kwenye sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naona mchakato huu wa kuibadilisha hii sheria ni *transitional*, bado tunahitaji *a comprehensive review* ya sheria zote za *economic zones* ili tuweze kuwa na sheria moja ambayo ita-*provide incentives* siyo tu kwa *foreign investors* lakini pia i-*provide incentives* kwa *local investors* na hasa hasa watu wa viwanda vidogo vidogo na tunaweza tukaitumia *SIDO* katika jambo kama hili kwa ajili ya kuweka maeneo ambayo watu wetu wataingia, watazalisha bila kodi kama jinsi ambavyo *foreign investors* wanavyonyimwa na kuweza kuingiza yale mazao katika soko la ndani.

Mheshimiwa Spika, hayo tu ndiyo ambayo nilikuwa nataka kuchangia kuhusu hizi *review, status* ya *SEZ* ya Kigoma na maeneo mengine ambayo yamepangiwa *SEZ*. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini vilevile naomba kumpongeza Mheshimiwa Rais na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwa ujumla kwa uteuzi uliofanyika hivi juzi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Umefanyika jana.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Spika, samahani umefanyika jana. Nasema sisi wanachama wa Chama cha Mapinduzi tutafanya kazi nzuri, tutaunga mkono na nina imani kabisa mwaka 2015 ni vumbi tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sheria ya *Economic Development Zone Act* ya mwaka 2011 naunga mkono kwa asilimia mia moja. Naweza kusema imechelewa kuletwa kwa sababu ni sheria ambayo inataka kuunganisha mpango mzima wa *EPZ* na *SEZ* ili kuwa na mfumo ili kuwe na mamlaka itakayoweza kuongeza hii mifumo miwili katika kuboresha nchi yetu ya Tanzania. Hakuna nchi duniani, hakuna Serikali duniani inaweza ikasema sisi tumeendelea sisi kama sisi bila kuwa na *private* sekta. Ndio maana katika nchi za *Far East* kulikuwa na mifumo mingi sana. Moja katika mifumo hii ni hii hii ambayo sasa tumefanya ya *EPZ*, leo sheria yake tunaipitisha hapa ili waende wakafanye kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, faida yake nini, siyo tu ajira au kufanya *processing*, kuuza mauzo ya nje asilimia themanini, ndani ikawa asilimia ishirini ni pamoja na ku-*gain foreign exchange*. Tunapata fedha za kigeni. Tatizo kubwa lililopo sasa hivi shilingi inaposhuka ni kutokana na kwamba hatuna fedha za kutosha na hii ni moja ambayo itasaidia nchi yetu. Serikali haina ubavu bila kuwa na *private sector* wala hakuna wafanyabiashara, inaweza ikafanya kazi bila kuwa na Serikali. Naamini kabisa katika mpango huu mzima Serikali yetu itapiga hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, tumeanza mpango huu muda mchache sana zaidi ya miaka mitatu au minne iliyopita lakini mafanikio yake yataonekana huko mbele ya safari. China leo wana miaka 35, faida ya mifumo yao yote ile imeonekana miaka kumi tu iliyopita, lakini walianza miaka thelathini iliyopita. Hata ukitaka kufanya biashara unaweza

ukaanza na *loss*, ukajitahidi ukaja kwenye *break even*, ukajitahidi ukaanza ku-*make profit*. Sasa suala la nchi kama hii kuandaa mifumo hii huwezi ukaona faida yake leo.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara na taasisi zote hizo wameanza kuonyesha mafanikio mazuri tu na ina maana kwamba ndani ya miaka mitano au miaka kumi kutakuwa na ajira nyingi, kutakuwa na fedha nyingi, *foreign exchange* tutapata za kutosha na hizo *foreign exchange* ndio zitakazoweza kuongeza fedha zetu za bajeti ya kila mwaka katika bajeti yetu ya Tanzania na kuondoa yale ambayo mnaongea sasa, huku hakuna maji, huku hakuna barabara, ndio hizi fedha zitakazoweza kutasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashauri kupanua uwigo, nchi yetu ni kubwa. Kwa hiyo, nashauri kuandaa maeneo haya mazuri, Mkoa wa Shinyanga pale tumeshaandaa Kahama, nina imani kabisa Kigoma na vilevile na Mbeya. Hii itasaidia sana kwa sababu Jiografia ya nchi yetu tumezungukwa na nchi nyingi sana. Tukipanua uwigo Shinyanga tukawa na viwanda vya kutosha, Kigoma tukawa na viwanda vya kutosha, Mbeya tukawa na viwanda vya kutosha nchi zilizo jirani na nchi yetu watakuja kununua bidhaa kule kule maana yake *export processing zone* hii haimaanishi tu kwamba ni kwa ajili ya kuuza nchi za *Europe* na China, hapana, hata nchi hizi za Afrika kuna soko la *East Africa*, kuna soko la *SADC*, kuna soko la Afrika. Yote kwa pamoja na tunazingatia.

Mheshimiwa Spika, halafu naomba niseme hivi, niko kwenye Kamati ya Viwanda na Biashara, mfumo huu siyo kwa ajili ya wageni tu na Watanzania. Naomba nitoe wito hapa kwamba, kama kuna Mtanzania anataka kuwekeza Shinyanga aje hapa tushikiriane na Sheria hii, tumpe kipaumbele ili tuje tufanye kazi vizuri katika Mkoa wa Shinyanga, katika mfumo huu aweze kusaidia kuuza mali zetu nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa linalojitokeza au kinachofanya sisi tuonekane kidogo bado hatujajiandaa kuna vile vikwazo vidogo vidogo vinavyoonekana katika *process*, suala zima la usajili wa leseni ama *process* kwa maana ya *export* na ku-*import* ama malighali ama bidhaa zilizo tayari kutoka nchi za nje. Nashauri na nazidi kushauri *TRA*, *EPZ* wanalalamikia *TRA*, *TIC* wanailalamikia *TRA*, Bandari wanailalamikia *TRA* na ndio asilimia kubwa ya matatizo yote yanayojitokeza sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, nashauri katika maoni ya Kamati yetu aliyotoa Mheshimiwa Mwenyekiti na naiomba sana Serikali huyu Afisa wa *TRA* katika *EPZ* kwa maana hii *service centre* apewe *authority* kabisa kumaliza. Sasa siyo *TRA* tu ningepomba na hata Afisa wa *TPA* maana masuala mazima yakimalizika pale inakuwa ni *one day, two days* kama ni *export* kama ni ku-*import* pale bandarini mambo yote yanakwisha. Hii itaweza sana kusaidia na tutaonekana kweli tuko vizuri na tumejiandaa vizuri katika uwekezaji huu.

Mheshimiwa Spika, ikiwezekana hata na *BREILA*, ukitazama nchi zingine kama za *Far East* nilikuwa nafanya *research* kidogo tu, nimeomba nikasema nataka kuwekeza katika nchi yenu, walinijibu sekta zote, *BREILA* ile nchi wakanijibu tunaomba hiki, tunaomba hiki tukusajili unataka jina gani, yuko hapa. Sekta ile kwa maana kwamba

kutoa hii *Corporation Certificate* na kadhalika wakanijibu, *TRA* wa nchi ile wakanijibu, ina maana wote wako kwenye *centre* moja, wakanijibu vizuri na wakasema tutakusajili, tutakufanyia kazi zote ukiwa huko, wewe ukija hapa tunakukabidhi tu leseni yako na ofisi yako uanze kazi. *Tariff* zetu ni hizi na hizi. Kwa hiyo, mafanikio ya masuala haya hayawezi yakaonekana kwenye nchi ndani ya miaka mitatu tu. Hebu tuipe nafasi, nina imani kabisa tutafanya kazi vizuri, *foreign currencies* tutaipata vizuri huko mbele ya safari.

Mheshimiwa Spika, kuna *TIC* haiko kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara lakini ni mfumo huo huo. Kwa maana mtu anataka kuwekeza ndani anapita kwenye mfumo wa *Tanzania Investment Centre* pale ndio wanapopata masuala yote haya. Ningesauri *TIC*, *EPZ*, *EDZ* wangepata pamoja, wangepata na *centre* moja kwa mtu ambaye anataka kuwekeza ndani ya nchi anapita kwenye mfumo wa *TIC*, kwa mtu ambaye anataka kuwekeza kwa maana nchi za nje apite kwenye mfumo huu ambao tunapitisha Sheria hii sasa.

Mheshimiwa Spika, naiomba vile vile bajeti ambayo tuliipitisha sisi hapa kwa ajili ya *compensation* ya hawa ambao maeneo yao walikuwa tayari wameridhika kuyakabidhi kwenye *EPZ*. Mwaka 2008/2009, *EPZ* waliomba *14 billion*, Bunge likapitisha bilioni nane, wakapewa bilioni tano tu. Kwa maana tayari kuna bilioni tatu hawakupewa mpaka hivi sasa. Mwaka 2010/2011, waliomba bilioni 83 tukawapa bilioni tano, wakapewa bilioni mbili na hizi bajeti ambazo wameomba ni kwa ajili ya *compensation* kuwalipa wale wananchi ambao tayari walisharidhika kwamba hili eneo sasa liwe chini ya *EPZ*. Naomba tushirikiane Wabunge wote kwa pamoja na Wizara isisitize na ijitahidi kwamba hizi fedha kama tulishapitisha hapa zipo wapewe ili wakakamilishe kazi ya kuwalipa hawa ambao tayari wamekwishauza maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *SIDO* unapokuwa na maeneo makubwa ya nchi, unapokuwa na viwanda vikubwa kwa mfano China, unaweza kukuta kiwanda kikubwa hakitengenezi hata kitu kimoja imefikia mahali tu wana *assembly* ya asilimia 70, vile vitu vidogo vidogo wanakuwa wanavi-*order* kwenye viwanda vidogo vidogo kwa maana kwetu huku ni *SIDO*, unaweza kuwa na kampuni hapa ya *assembling* ya *tractor* wakafanya *assembling* lakini kuna vitu ambavyo wanaweza wakatengeneza *SIDO*, waka-*supply* pale wakaichukua wakaiunganisha ikawa *one unit complete*.

Mheshimiwa Spika, *SIDO* ni eneo ambalo ni muhimu sasa kwa maana ya sheria hii. Tukiwaendeleza *SIDO* tukawapa uwezo na hasa vijana wetu hawa walio-*qualify* kwenye *VETA* wamesomea vizuri tukajiandaa, tukaunganisha baina ya *SIDO* na wawekezaji wakubwa hawa tutakuwa tumeunganisha ajira baina ya *investors* wakubwa hawa wa ndani ya nchi na nje ya nchi wanauza nje na ndani pamoja na viwanda vidogo vidogo vya *SIDO*. *(Makofi)*

Naishauri Serikali, kupitia *SIDO* tutenge fedha za kutosha mwaka huu, kwa ajili ya kuinua sasa suala zima la *SIDO*. *SIDO* wawe na maeneo yao tuwaandalie maana yake kero kubwa ni kwamba hawana maeneo ambayo yako tayari, maana yake wale hawana

*capital* ya kutosha, tuwaandalie maeneo ya kutosha, waingie pale wakute tumeshawaandalia kama ni umeme, maji, kama ambavyo tunaandalia sasa hivi wa *EPZ* kwa ajili ya *Export Processing Zone*. (Makofi)

Tukipanga vizuri *SIDO* ajira sasa hapo inapatikana, tunaunganisha nguvu ya *SIDO* na nguvu hii ya sheria tunayoipitisha sasa hivi kama ambavyo mafanikio ya nchi zilizofanikiwa kama China. China mimi mwenyewe *physically* nimetembelea huko na nimeona hivyo. Asilimia kubwa ya viwanda vya China wanafanya hivyo. Utakuta viwanda vikubwa hasa hawafanyi vitu wanatengeneza asilimia 30 tu asilimia 70 wana-*order* kwenye viwanda vidogo vidogo hivi ili kujenga ajira kwa ajili ya hawa viwanda vidogo vidogo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kupanua uwigo, jiografia yetu, nasisitiza hili kwa sababu natoka Mkoa wa Shinyanga, Jimbo la Solwa. Katika Mkoa wetu wa Shinyanga, kuna rasilimali kubwa sana na huwezi kuongelea kilimo kwanza tu, ukasema kilimo kwanza, ukamsaidia mkulima akaanza kulima pamba, akapata pamba nyingi, utakuwa una-*encourage* kilimo kwanza kwa ajili ya ku-*export raw material*. Sasa ku-*add value* kwa ajili ya raw material ni kuwa na viwanda vya uhakika kwenye maeneo yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, vile viwanda ndivyo vitakavyokuwa vinanua rasilimali kwa maana mazao wanayolima wakulima wetu. Naiomba sana Serikali, Wizara ya Viwanda hebu sisitiza katika Mkoa wa Shinyanga tuweke bajeti nzuri, tujenge eneo zuri ili sasa wakulima wa Shinyanga, Jimbo la Solwa ni maarufu sana kwa dengi pamoja na pamba. Kuna maeneo mazuri sana Shinyanga, tuna tumbaku, pamba, asilimia 60 ya pamba haiwezekani kuona kwamba Mkoa wa Shinyanga unakosa kiwanda kweli cha uhakika na hii sasa itatusaidia sana. Hapo sasa ndipo ajira inapopatikana, tukipata viwanda ndipo ajira inapopatikana kwa wakulima, tukipata viwanda ndipo soko la uhakika linapopatikana kwa wakulima. Leo pamba kilo moja shilingi 1,100/=, hivi tukiweka kiwanda pale si itafika shilingi 2,000/=?

Mheshimiwa Spika, unaposaidia katika suala zima la kilimo kwanza, tutazame na uwekezaji wa viwanda kwenye maeneo yetu, ukifanya hivyo hivyo Kigoma. Mchikichi kule kwa maana ya kwamba Kiwanda cha Mafuta, ukifanya kule Mbeya tunapanua wigo, nchi zetu za jirani Burundi, Rwanda wanaweza wakaja nchini wakanunua, wakaondoka, nchi za kule karibu na Mbeya, Zambia, Malawi na kadhalika wanaweza wakaja pale wakanunua wakaondoka. Hili suala ni muhimu sana, tusidharau hata safari ya kilomita 100 au kilometa milioni moja unanza na hatua moja. Hapa tulipofikia miaka mitatu ni mafanikio mazuri sana.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (Makofi)

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia huu Muswada muhimu kwa maendeleo ya Watanzania. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri ambaye ametuletea Muswada huu na nina amini malengo yake yatafikiwa, lakini kabla sijachangia niseme kwamba

nakipongeza sana Chama changu Chama cha Mapinduzi chini ya Uongozi wa Mwenyekiti wetu wa Taifa, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kikao kilichofanyika wiki hii cha *NEC* na maamuzi tuliyofikia na nawapongeza wenzetu ambao wamefanikiwa kupata hizo nafasi. Naamini watazitemikia vizuri na hii ni dira sasa, kujivua kwa gamba hili sio tu kwa ngazi ya juu bali iteremke katika ngazi zote ndani ya Chama chetu na kwenye Serikali yetu ambayo tunaiongoza.

Mheshimiwa Spika, nadhani hata Muswaada huu umelenga kuvua gamba, badala ya kuwa na maeneo ambayo yanagongana na vizuri kuwa na eneo moja ambalo litashughulikia masuala ya uwekezaji kwa ajili ya mauzo ya nje na ndani kwa ujumla. Lakini pia nitoe changamoto ambazo tulizipata wakati tunajadili Muswada huu. Kwa hili niseme kwamba, ndugu zangu wananchi tunapokuwa tunapitisha Miswada katika zile hatua za kujadili na kuweka mambo ambayo tunaona kwamba yangetusaidia ni vyema tunapoitwa tuwe tunashiriki kikamilifu. Inaonekana kwamba kuna baadhi ya Miswada ambayo tunaipa nguvu zaidi, lakini mingine tunakuwa kama hatuna hamu nayo sana, matokeo yake Sheria zinapita sisi wenyewe tunakuwa hatuna ufahamu wa kutosha kuhusu ile sheria na hivyo kushindwa kutumia fursa ambazo zingeweza kutusaidia kwa maendeleo yetu.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Viwanda na Biashara pamoja na Wajumbe wote kwa jinsi ambavyo tumeshirikiana, lakini hasa katika kuangalia ni mambo gani tuyaboreshe na ndiyo maana hata wenzetu kwa mfano, Mheshimiwa Mnyika amesema kwamba tumeweka vitu vingi sana vya kuboresha kama Muswada. Huu ndiyo wajibu wetu kama Wabunge kuhakikisha kwamba Muswada unaboreshwa ili utoke unavyostahili.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wangu hasa naomba leo nilisisitize suala la kuhusisha maeneo kwa ajili ya wawekezaji wa ndani, hasa nawazungumzia wajasiriamali wadogo na wa kati. Sera yetu ya ujasiriamali ya mwaka 2003 inazungumzia wazi changamoto zinazowapata wajasiriamali wetu wadogo na wa kati katika kupata maeneo ya kufanyia kazi na katika mikakati iliyopo ni pamoja na kutenga maeneo hayo. SIDO tumeipa kazi hiyo ya kuwaendeleza wajasiriamali wa viwanda vyetu vidogovidogo, lakini hawana maeneo ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, tuna ndugu zetu maarufu kwa jina la Wamachinga, wanafanya kazi zao vizuri sana, wako katikati ya miji, wanahangaika kutafuta maeneo ya kufanyia kazi, kuna mifumo ambayo ingewawezesha kufanya kazi kama *cluster*, kongani kwa neno la Kiswahili kwamba waweze kushirikiana kwa pamoja. Mwenye kuweza kutengeneza chuma, mwenye kuweza kuchomelea wakae pamoja na ndivyo wanavyoweza kupata tija, lakini wanashindwa kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa mara nyingi tukiangalia wawekezaji wakubwa hususan wageni na hilo niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliochangia. Haiwezekani tuangalie tu wawekezaji wakubwa tukaacha hawa wadogo ambao ni wengi, taarifa zetu zinaonesha kwamba karibu asilimia 60 ya viwanda vidogovidogo ambavyo havijulikani viko kwetu sisi wenyewe na ndivyo vinavyotumia soko la ndani ambalo ni



sisi wenyewe. Kwa hiyo, itakuwa hatujitendei haki kuona mwananchi wetu wa kawaida ambaye anaishi kwa kufanya shughuli zake hizi ndogo ndogo anahangaika na hatumpi ufumbuzi. Katika suala hilo Kamati yetu chini ya Mwenyekiti wangu, Mheshimiwa Mahmoud tulikubaliana kwa pamoja na bahati nzuri tumeongea pia na Mheshimiwa Waziri kusema kwamba suala hili kwa sasa lifanyiwe kazi na lisichukue muda tena, Watanzania wamechoka kuhangaika, inabidi tuwape ufumbuzi wa matatizo yao.

Mheshimiwa Spika, nikirudi pia katika suala la msongamano wa kibiashara Jijini Dar es Salaam, Bandari yetu imejaa lakini katika maeneo hayo tunayoyatenga sasa hivi, tunalo eneo kama la Bagamoyo ambalo pia litawezesha kuwa na Bandari itakayosaidia kupunguza mzigo wa msongamano katika Bandari ya Dar es Salaam. Tatizo mpaka sasa hivi hili eneo bado halijakamilisha kupata hela za kutosha kulipa fidia. Sasa ninachowaomba tukiamua jambo tufanye kweli, kwa sababu hii mikakati inayochukua muda mrefu sana bila kuipa uzito kwa wakati muafaka tija yake inakuwa ni ndogo na ndiyo maana tunahojiwa, kwa nini Serikali mpaka leo hatuoni matunda, kwa sababu tunawekeza kidogo kidogo, ni sawa na ng'ombe, unajaribu kumkamua wakati humlishi, iko haja ya kusaidia maeneo haya ili yaweze kutimiza madhumuni ambayo yalikusudiwa.

Mheshimiwa Spika, nikizungumzia hilo pia niseme tu kwa ujumla wake, ukweli ni kwamba matatizo yote tunayoyapata Waheshimiwa Wabunge yanatokana na Wizara ya Viwanda na Biashara kupewa bajeti ndogo mno ikilinganishwa na majukumu yake, mojawapo ndiyo kama hili tunaloliona leo. Kwa bahati nzuri Kamati yetu tuliwaita wadau wote wanaohusika na kila mtu ametueleza jinsi wanavyoweza kuhusiana katika kuhakikisha kwamba Muswada kama huu wadau mbalimbali wa Kamati ya Viwanda na Biashara kwa eneo linalowahusu wanahusika vipi kusaidia. Kwa hiyo, niseme tu kwamba, Mheshimiwa Waziri kwa maelezo ambayo Waheshimiwa Wabunge wamechangia, tunaomba yale yanayowezekana kuingizwa katika kuboresha yaingizwe, lakini hali kadhalika naomba kabla hatujafikiria kufanya jambo kwa ajili tu ya wageni, lakini msisitizo wetu uwe kwa kuanzia Watanzania ambao ni wengi na ndiyo wenye uwezo wa kutumia fursa zilizopo jirani na wao wenyewe na hivi kupata faida kubwa zaidi kwa maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, maisha bora kwa kila Mtanzania yanawezekana endapo tutaamua kuwashirikisha kwa umoja wao Watanzania wa ngazi zote ili wote kuchangia katika maendeleo ya Taifa lao kwa kuwapa fursa zinazostahili. Suala la fidia kwenye ardhi nikianza na Mkoa wangu wa Ruvuma pale Mkuza, Mwengemshindo tunawaombeni sana, wananchi wanachelewa, Wabunge wao tunawahamasisha kwa kila hali wajitahidi kujiletea maendeleo, wamesimama, tunaomba Serikali itenge katika bajeti yake mwaka huu pesa za kutosha ili kuwezesha kulipa fidia zinazostahili katika maeneo ya Ruvuma, Bagamoyo na maeneo ya Bunda kama ambavyo imeelezwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Dakika nilizonazo ni kumi, anayetaka kuchangia dakika hizo kumi tu nampa ruhusa. Mheshimiwa Susan Kiwanga unaweza kuchangia hizo dakika? Maana yake dakika zetu ni dakika kumi na tano, hizi ni kumi tu.

**MHE. SUSAN L.A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Hata hivyo, nilikuwa sina mengi sana ya kuchangia kwa sababu michango mingi imeshatolewa na Wabunge wenzangu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nitoe mchango wangu mchana huu wa leo ili niwe katika kumbukumbu za kuwatetea Watanzania kwa ujumla wao. Katika mpango mzima wa Sheria hii ya *EPZ* na *SEZ* naona kilichozingatiwa sana katika hii sheria ni kuunganisha sasa iwe Bodi badala ya Baraza. Lakini ukiangalia katika mpango mzima tangu mwaka 2002 mpaka kufikia mwaka 2011 kwamba kuna mambo makubwa sana ambayo yamewagusa moja kwa moja Watanzania katika mpango mzima wa *EPZ* na *SEZ* na kama michango ya Wabunge wenzangu waliotangulia kwamba kuna mambo mengi ya kuyaangalia na sio hili tu, kuna changamoto zake na tumejifunza sasa kwa sababu ulivyoingia tu tulikuwa hatujui ndani ya mchakato huo, kufikia malengo tuliyokusudia kwa mpango huu, yatakuwa na faida gani kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, tumejionea wenyewe katika maeneo mengi ya uwekezaji pamoja na kuwa na mpango huu umezalisha ajira elfu kumi lakini ukizichambua kwa undani hizo ajira ni akina nani wanaofaidika na hizo ajira elfu kumi, je, watu wa nje wanaokuja kuwekeza katika hizo ajira zao wanazotoa katika mpango huo na je, katika uwekezaji huu, watu wa ndani wana manufaa makubwa kiasi gani na watu wanaojiri kutoka kwao wana manufaa makubwa kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika ajira hizo wanazotoa kwamba hawa wawekezaji wanapojiri watu kutoka katika Mataifa yao wanapewa viwango vikubwa sana vya mishahara na marupurupu makubwa sana kuliko watu wa ndani ambao wako ndani ya nchi hii wanaojiriwa katika maeneo hayo ya uwekezaji. Kwa hiyo, haya ni masuala ambayo tulipaswa kuyaangalia ili hata kama tunasema tumezalisha hizi ajira, wanafaidika kiasi gani katika maisha ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, katika masuala mazima ya hizo ajira utaangalia kwamba hao walioajiriwa ambao ni Watanzania unyanyaswaji wao katika maeneo hayo yako kwa kiwango gani. Tumeshuhudia kuna manyanyaso ndani yake yanayofanywa na hawa wawekezaji. Je, sheria zinawalindaje sasa ili kuondoa haya manyanyaso wanayopata hao walioajiriwa?

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la uwekezaji na *EPZ* ni kwamba unakuta kuna sheria zinasema huyu mwekezaji anawekewa mazingira mazuri sana, vivutio na misamaha ya kodi na miundombinu, lakini ukiangalia sasa katika haya maeneo ya uwekezaji ni maeneo gani, unakuta kwamba hizo barabara zinazozungumziwa, maji, umeme basi hao wanakimbilia sana sehemu za mijini na wanaacha maeneo ambayo kumbe hayo marupurupu na hivyo vivutio vingekuwa sasa vinapelekwa pembezoni basi nadhani leo nchi yetu ingekuwa na barabara nyingi sana katika maeneo ya pembezoni, kungekuwa na umeme na maji, lakini utakuta wanaelekeza maeneo ambayo hizi huduma tayari zipo, kwa hiyo unakuta kwamba bado mpango mzima hauleti faida sana kwa wananchi wa kawaida katika suala zima la uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, nachukulia mfano kwenye Kiwanda cha Sukari Kilombero, pale wapo wawekezaji lakini utaangalia wale wananchi wa pale wanafaidika nini? Hata pale Turiani wanafaidika nini? Ufaidikaji wao ni mdogo sana. sukari inazalishwa pale Kilombero....

**SPIKA:** Mheshimiwa hiyo sio *EPZ* sasa, ile ni kiwanda tu sio *EPZ*, tuendeleo.

**MHE. SUSAN L.A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa marekebisho hayo. Huu ni usongo tu unachanganya mambo kutokana na mfaidiko wa wananchi katika suala zima la uwekezaji na *EPZ*, lakini ahsante kwa kuniongoza. Sasa *EPZ* tukiangalia suala zima la kusimamia na kuangalia hii sheria na mabadiliko haya ni wazi kwamba kama walivyokuwa wanasamehewa kodi kwa muda wa miaka kumi bado najiuliza, wakishasamehewa kodi miaka kumi, je huyu mwekezaji ataendelea kuwepo au atajibadilisha sasa ameshapata labda faida yake anaingia mwingine asamehewe tena kodi miaka kumi. Kwa hiyo, hilo nalo ni tatizo katika huu mpango mzima na tuangalie namna gani kushirikisha wananchi.

Mheshimiwa Spika, naungana sana na wenzangu kwamba kushirikisha sana wananchi wa kawaida ili wafaidike na waelimishwe katika suala zima la *SIDO*, nadhani leo tungekuwa tunazungumzia mambo mengine, tunapata takwimu katika mpango mzima wa *EPZ*, wameshirikisha vipi *SIDO* na tumenufaika vipi kama Watanzania kwa sababu *SIDO* inajitambulisha zaidi kwa Watanzania mpaka katika maeneo ya pembezoni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo katika mpango mzima katika kunufaisha na kuelimisha ili hawa wahitimu wetu wa Vyuo Vikuu vya Ufundi mbalimbali sasa kama wataelimishwa kutokea huko mashuleni kwa sababu hakuna ajira ya moja kwa moja Serikalini kwa kupitia mpango wa *SIDO* na vivutio hivyo vinavyowekwa na *EPZ*, basi nadhani moja kwa moja watajiona kwamba kuna umuhimu wa kuweka vikundi na vivutio kama hivyo na watachagua maeneo mazuri ya uwekezaji na vivutio ili kuwanufaisha na kujipatia ajira inayoweza kuleta tija zaidi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naona hata dakika kumi nisimalize, nisije nikaenda kwingine maana nina usongo. Naomba niishie hapa. Ahsante.

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Waziri na watendaji wake wote kwa kuleta Muswada huu kwa nia ya kufanya marekebisho. Malengo ya msingi ni kuipa nguvu mamlaka kuongeza uzalishaji wa mauzo ya nje. Marekebisho haya ya muundo kwa mfano, yanayotengenezwa kuondoa migongano ya *EPZ* na *SEZ* kwa kuleta ufanisi wa shughuli za biashara za nje.

Mheshimiwa Spika, mchango wa *EPZ* na *SES* katika biashara ya nje bado ni mdogo sana na hivyo bado haujakidhi matarajio ya wananchi. Bidhaa zinazosafirishwa nje ya nchi zinatakiwa kuwa na ubora wa Kimataifa. Suala la kujiuliza ni kwa kiasi gani

suala hili linafuatiliwa. *SES* na *EPZ* inatoa vivutio vya Wafanyabiashara ili wazalishe. Vivutio hivyo vinalalamikiwa kuwa vinawanufaisha zaidi wageni kwa sababu uwekezaji ni mkubwa kwa upande wa Serikali lakini kinachopatikana ni kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, pengine faida mojawapo ya *SES* na *EPZ* ni kuongeza ajira kwa wazawa pamoja na manufaa ya kijamii iliyozunguka maeneo ya Mamlaka hizi, hilo pia halijafikiwa. Hivyo, ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kuwa *EPZ* na *SEZ* inaongeza ajira na inaleta manufaa ya moja kwa moja kwa jamii iliyozunguka maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, tatizo la misamaha ya kodi ya aina mbalimbali inaonyesha kuwa haisaidii kufikia lengo la kukuza uchumi wa nchi. Kwa hiyo, ni bora Serikali ikatafakari upya kwa kuangalia jinsi nchi nyingine za Asia wanavyofaidika na mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, huu ndio mchango wangu mfupi na naunga mkono hoja.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia yafuatayo kwenye Muswada huu. Kwa kuwa Muswada unalenga marekebisho kwenye maeneo kadhaa, napenda kuchangia kwenye Maeneo Maalum ya Kiuchumi, Sura ya 420 kwa ajili ya kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji wa kigeni na wa ndani.

Mheshimiwa Spika, suala la uwekezaji ni suala zuri kama linafanywa kwa usawa kati ya *external investors* na *internal/local investors*. Hii ni kuweka mazingira sawa kwa wote kama ambavyo wawekezaji wa nje wanavyoandaliwa mazingira ya kuvutia, mgeni kufutiwa kodi mbalimbali za forodha, VAT, mitambo na kadhalika vivyo hivyo iwe inafanywa kwa wawekezaji wa ndani ili kuwafanya nao waweze kufurahia mali na rasilimali za nchi yao kama ambavyo wageni wamekuwa wakifanyiwa.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unalenga katika kuwaandalia mazingira mazuri wawekezaji wa nje kwa masuala ya miundombinu ya barabara, maji, umeme na kadhalika. Kwa hilo nashauri kwamba wawekezaji wasiwe wanaandaliwa mazingira ya namna hii wakati huo huo wanasamehewa kodi kwa miaka 10 ya utendaji kazi/uzalishaji. Wawekezaji wanaweza kutumia muda huu kupora rasilimali zetu na wakati huo huo, wanategea muda wao wa *offer* uishe na wanaweza wasiendeleo tena na uwekezaji baada ya muda wa *offer*, je, hili linapotokea si kwamba wazawa wanakuwa hawajatendewa haki? Ningeshauri kuwa kama mazingira ya namna hii yataendelea kuwekwa basi pawepo na kipengele cha kuwabana pale wanapomaliza mwaka wa 10 na ikitokea wakakatisha uwekezaji wao, basi watupe fidia ya gharama zote ambazo Serikali imeingia katika kuandaa mazingira ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwenye eneo la marekebisho yanayompa mamlaka Waziri mwenye dhamana na ardhi kutwaa ardhi zaidi na kutoa uwezo zaidi kwa mamlaka katika kuridhia na kutoa vibali vya ujenzi chini ya Sheria ya Mipango Miji, Sura ya 355 na kutoa leseni.

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu ni kwamba madaraka makubwa anayopewa Waziri mwenye dhamana ya ardhi yasipodhibitiwa, yanaweza kutumika kwa kuwanyanyasa wananchi wanyonge na maskini. Hii ni kwa sababu, kwa muda mrefu sasa wananchi wa Tanzania, hususani wa vijijini wamekuwa wakiishi katika maeneo ambayo ni ya urithi wa jadi toka kwa mababu na wazazi wao, kwa maana hiyo hawana hatimiliki ya maeneo wanayokaa. Kwa kuwa ardhi ni mali ya Serikali na wananchi ni sehemu ya hiyo Serikali, basi linapokuja suala la mamlaka kutwaa ardhi kwa ajili ya uwekezaji hususani kwenye maeneo ya makazi ya watu, ifanye kwanza tahmini yakinifu ili iweze kuwafidia wananchi stahili zao bila manung'uniko.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na uwekezaji wa kiharamia katika maeneo mengi ya madini na umeme, mfano katika Jimbo la Singida Mashariki, Kampuni ya *Shanta Mining* ilimilikishwa eneo la uchimbaji madini/dhahabu katika Kata ya Mang'onyi na wananchi walihamishwa kwa udhalilishaji mkubwa sana na mpaka sasa bado hawajafidiwa na wengine wamefunguliwa kesi za uvamizi Mahakamani. Si hilo tu la Mang'onyi pia suala la umeme wa upepo katika eneo la Kititimo, Mkoa wa Singida, Halmashauri/Manispaa ya Singida wananchi wamehamishwa kwa nguvu na Kaya kadhaa zimekosa makazi na mpaka sasa bado hawajapata fidia.

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri kuwa, linapokuja suala la uwekezaji kwenye majengo au shughuli mbalimbali za biashara, basi ni vizuri kwa ile Mikoa ambayo ina maeneo makubwa ambayo hayakaliwi na watu, basi ndiyo yawe yanatolewa leseni ili ujenzi uendelee kuliko kuwaingilia wananchi kwenye makazi yao na kuharibu utaratibu wao wa maisha na shughuli zao za kila siku. Hii itaondoa pia ubadhirifu wa fedha na matumizi mabaya ya fedha za Serikali katika kuwafidia wananchi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naomba kuwasilisha.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa hii ili niweze kuchangia mjadala ambao uko mbele yetu wa maeneo Maeneo Maalum ya Kukuza Uchumi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami, Mbunge wa Moshi Vijijini, kwa kuaminiwa na Rais na hivyo kupewa dhamana kubwa yakuendesha sekta muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuchaguliwa kwake kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara kunatokana na uadilifu, uaminifu na uchapakazi wake.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atuelezee/atoe maelezo kuhusu suala zima la kuendeleza eneo maalum la uchumi kuzunguka Bandari ya Mtwara. Eneo hili lilitwaliwa toka kwa wananchi miaka mingi iliyopita hata hivyo hadi sasa hakuna shughuli yoyote inayoendelea katika eneo hilo. Kwa nini Serikali iendelee kutafuta maeneo mengi zaidi wakati yale ya awali hayajaendelezwa?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. STEPHEN M. WASIRA:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba maoni yafuatayo; kimsingi nakubaliana na hoja ya kuunganisha Sheria ya *EPZ* na *SEZ*. Naomba Mamlaka ya *EPZ/SEZ* ichukue hatua za haraka kuwalipa fidia wananchi wa kijiji cha Tairo ambao eneo lao limechukuliwa ili kuwezesha *EPZ* kufanya kazi. Malipo haya yamecheleweshwa sana na kuwafanya wananchi wa kijiji hiki kufarakana na Serikali.

Naomba kauli ya Wizara ili wananchi wa eneo wajue haki na hatima ya maombi yao.

**MHE. NAOMI M. KAIHULA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuchangia Muswada huu wa maeneo ya Uwekezaji Huru ya Kukuza Uchumi.

Nikiwa mmojawapo wa Kamati hii napenda nitambue umuhimu wa Sheria hii ya Uwekezaji (*EPZ*). Ukweli ni muhimu sana kwamba maeneo haya kama vile jina lake lilivyo maeneo maalum ya kukuza uchumi yaishi kweli kuwa hivyo. Kwani hadi sasa wananchi wengi hawana ufahamu wa kina juu ya maeneo ya uwekezaji licha ya kuwa yamekuwa katika ardhi yao na pengine kupora ardhi yao bila ya kuwafaidisha kama ambavyo wangepaswa kufaidika.

Mheshimiwa Spika, kuisitiza pendekezo la Kamati kwamba Sheria zifafanuliwe kutoka lugha ya kisheria kuwa katika lugha ya kawaida yaani Kiswahili chepesi (*popular language*) au lugha pendwa inayoweza kueleweka na wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, pia kwa ajili ya ufanisi wa utendaji wa haraka wa kuwavutia wawekezaji wengi ingefaa sana kuwaweka watoaji maamuzi wote wa masuala muhimu katika kituo kimoja yaani *one stop centre*, hii itawezesha ufanisi kupunguza ukiritimba wa kuchukua muda mrefu sana kabla vibali havijatolewa na kukatisha tamaa wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, suala hili halijakidhi lengo lake la kukuza uchumi kwa vile bado wananchi wengi hawajui matumizi yake na faida zake hazielekei kuonyesha kuwa kuna mapato ya kutosha. Hivyo wananchi wengi kuona kuwa ni kituo cha kufaidisha wageni zaidi ya wananchi. Pendekezo ni kuona *SEZ* inasimamiwa vizuri ili iwe kipenyo kwa wawekezaji wadogo wa ndani. Maana yake juhudi za makusudi zichukuliwe kuwaingiza *SIDO* katika mpango huu na kwa sasa Kanuni ziandaliwe kuwezesha jambo hili la *SIDO* kufikiwa. Faida kubwa ni kufaidisha wananchi wanaochukuliwa ardhi zao.

Mheshimiwa Spika, ni vema suala la hisa za wazalendo likapewa umuhimu.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ninapenda nichukue nafasi hii, kuipongeza Serikali, kwa kuleta Miswada hii ambayo imechelewa sana kulingana na umuhimu wake kwa Watanzania. Hivyo, kabla sijaanza kutoa maoni yangu, ninapenda kutamka rasmi kuwa, ninaunga mkono Miswada hii yote miwili.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutambua juhudi kubwa zilizofanywa na Kamati, kutoa ushauri kuhusu Miswada yote miwili, ambao umesaidia sana kuboresha Miswada hii; hivyo, ninaomba ushauri wa Kamati uzingatiwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wawekezaji wa ndani na nje, ninapenda kuishauri Serikali kuwa, ni vema katika kuinua uchumi wa nchi hii na kuondokana na migogoro ya wawekazaji hasa wa nje ni vema mikataba kuwa wazi na yenye kuzingatia sheria na kanuni za nchi yetu. Pia ni vema wawekezaji wa ndani wapewe kipaumbele ili kusaidia Watanzania hasa akina mama na vijana, kuinua vipato vyao. Hii itasaidia utajiri wa nchi yetu kunufaisha Watanzania wenyewe.

Mheshimiwa Spika, ni vema kuweka uangalizi na udhibiti wa uhakika ili mali yetu isiwape wawekezaji wa nje kutuibia mfano udongo wa madini kupelekwa kuchambuliwa nje ya nchi, inawezekana wawekezaji wakaendelea kunufaika.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumalizia kwa kumpongeza Mheshimiwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa aliyoifanya na kukisafisha Chama cha Mapinduzi kwa kuvunja Sekretarieti na Kamati Kuu, kwa lengo la kuimarisha chama na kurudisha matumaini kwa Wana-CCM na Wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, vile vile niwapongeze wote walioteuliwa kuwa Wajumbe wa NEC, Wajumbe wa Kamati Kuu pamoja na Sekretarieti ya CCM wakiwemo Mheshimiwa January Makamba, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba Mwigulu, Ndugu Wilson Mukama kuwa Katibu Mkuu wa CCM, Mheshimiwa Capt. John Chiligati kuwa Naibu Katibu Mkuu wa CCM, Ndugu Nape Mnauye kuwa Katibu Mwenezi wa CCM, Ndugu Asha Abdallah na Ali Omary Heri. Nina matumaini makubwa sasa chati ya Chama chetu itakuwa juu, Wapinzani matumbo moto.

Narudia tena kuunga mkono Miswada hii na Mungu atawatangulia katika utekelezaji.

**MHE. SHAWANA BUKHETI HASSAN:** Mheshimiwa Spika, ninapongeza na ninaunga mkono hoja ya Muswada wa Sheria ya Marekebisha ya Maeneo Maalum ya Kukuza Uchumi.

Mheshimiwa Spika, mimi nikiwa kama Mjumbe wa Kamati, ninaomba kusesitiza suala la Wananchi kulipwa ardhi ambayo itatumika kwa uwekezaji kwa wakati ili kuondoa tatizo la migongano kati ya wenye ardhi na wawekezaji.

Pia ninaomba kusesitiza suala la kushirikisha Wananchi kabla eneo linalohitajika halikuchukuliwa kwa uwekezaji halijachukuliwa ili kuondoa malalamiko kwa Wananchi juu ya Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, ninashauri Wizara kuipatia kipaumbele Taasisi hii na kuipa fedha kwa wakati na kwa kiwango walichokipanga, kwa mujibu wa bajeti yao ili waweze kufikia malengo yao.

Vilevile ninaomba kusesitiza juu ya suala la *TRA* kuwa, awepo afisa mwenye maamuzi kamili katika suala la kuondoa urasimu kwa mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninampongeza Mheshimiwa Waziri na ninaunga mkono hoja ya kutuletea Muswada mzuri utakaoleta tija na kuongeza mapato katika nchi yetu. Ahsante.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono marekebisho hasa kwa kuzingatia muda tulionao.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa ushauri kwa kumwomba Waziri wa Ardhi wakati wa kutwaa eneo la ardhi kwa madhumuni ya matumizi yaliyokusudiwa awasiliane na wakazi/wamiliki wa eneo husika kwa kuwapa elimu ya kutosha kuhusu eneo ambalo linatakiwa litumike kwa matumizi mengine. Lakini pia Serikali pale wakazi wa eneo hilo mbali na elimu, utaratibu wa kuwalipa fidia ufanyike kwa uwazi bila upendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba nikukumbushe kwamba *EPZA* na *ZSEZ* zikisimamiwa vizuri zitaongeza ajira, fedha za kifani kwa kuuza nje bidhaa na upatikanaji wa bidhaa kwa karibu vyenye ubora.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono.

**MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niunge mkono hoja hii ya marekebisho ya sheria hii kwani kuna mwingiliano mkubwa kati ya *EPZ* na *SEC*, hii itaipa nguvu *EPZA* kwa kusimamia pia Sheria ya *SEC*.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna masuala muhimu sana ili kuboresha suala zima la *EPAZ* kuwa *more friendly* kwa Watanzania wote. Tunajua kuwa lengo la *EPZA* ni kuchochea uwekezaji katika maeneo maalum ya uwekezaji nchini na kuinua uchumi na hasa mauzo nje ikiwa ni mojawapo ya utekelezaji wa Sera ya Maendeleo endelevu ya Viwanda (1996 – 2020).

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza hili lifanikiwe vizuri ni lazima kuwe na mafunzo maalum ili kwanza wananchi waelewe nini dhamira ya Serikali katika *zones* hizo na yeye mwananchi wa chini kabisa atafaidika na nini katika maeneo hayo ya uwekezaji. Vile vile utaratibu unaotumika katika kuchukua hayo maeneo, mimi siungi mkono hata kidogo, kwani sio utaratibu mzuri hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaweza ikawa na nia njema lakini Watendaji wanapotosha sana taratibu zake kwa mfano Tanga kuna eneo la *EPZA* ambalo limefanyiwa tathmini kihuni na mipango miji ni eneo lenye wakazi takriban 300 wanaondolewa katika eneo hilo. Wananchi wa eneo hilo wameichukia sana Serikali kwa



sababu wanaona kama wanafukuzwa kwenye eneo hilo kwa kudhulumiwa na vile vile hawaelewi wao na wakazi wa Tanga kwa ujumla watafaidikaje na uwekezaji huo. Nisisitize kuwa elimu ya kutosha inahitajika maeneo husika hasa hawa watu wa chini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, naunga mkono mapendekezo ya Kambi ya Upinzani, ni vizuri yakipewa kipaumbele ili kuboresha marekebisho hayo ya sheria.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa maslahi ya Watanzania na marekebisho haya yawalenge zaidi Watanzania.

**SPIKA:** Nashukuru sana, kwa mujibu wa Kanuni zetu kuna mijadala ya aina mbili. Tunapojadili kwa mfano hotuba ya bajeti, Waziri Mkuu atakapowasilisha hotuba yake ya makadirio pale unaweza ukaongelea jambo lolote, lakini inapokuja kwenye Muswada kabisa kabisa ni vizuri mkajadili Muswada kwa sababu *impression* tunayotoa kwa wananchi, tunatoa kitu kingine kabisa nje ya ule Muswada tunaohusika nao. Kwa hiyo, nitaomba Mheshimiwa Waziri utakapokuwa una-*wind* ueleze kabisa madhumuni ya Muswada kwa kiundani kusudi watu waweze kuelewa tofauti ya haya tuliyozungumza na hasa wewe ulikuwa unawasilisha kitu gani. Kwa hiyo, nitakuomba ufanye hivyo na kwa sababu tuna *Miscellaneous Amendment* aina mbili, hii ilikuwa maalum, halafu iko nyingi ya ujumla.

Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja, lakini kabla ya hapo naomba niwatangazie kwamba Kamati ya Uongozi tunakutana sasa hivi, halafu bado Ofisi inawakumbusha wale wanaohitaji kuonana na Ofisi ya Vizazi na Vifo wapo hapa Bungeni kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa Wabunge na familia zao ambao hawana vyeti. Kwa hiyo, kama bado mnahitaji bado wako hapa kwa hiyo, mnaweza kupata huduma hiyo.

Waheshimiwa Wabunge nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja.

*(Saa 6.57 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*  
*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

## **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Maeneo ya Maendeleo ya Kiuchumi wa Mwaka 2011** *(The Economic Zones Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2011)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Moja kwa moja, naomba nimwite Mheshimiwa Waziri, Dkt. Cyril Chami, kwa ajili ya kupitia hoja za Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Waziri karibu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yao waliyoitoa kwa Muswada wa Sheria uitwao (*The Economic Zones Laws (Miscellaneous Amendment Bill)*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, naishukuru Kamati ya Viwanda na Biashara chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, kwa michango yake iliyoboresha Muswada huu. Aidha, napenda kumshukuru Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, kwa mchango alioitoa alipokuwa akichangia Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya Wabunge 22 wamechangia Muswada huu. Wabunge 13 kati yao wakiwa wamechangia kwa kauli na Waheshimiwa Wabunge tisa wakiwa wamechangia kwa maandishi. Nawashukuru sana. Napenda kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, , Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Lucy Fidelis Philemon Owenya, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakosa, Mheshimiwa Regia Eslekatus Mtema, Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere na Mheshimiwa Mansoor Sharif Hiran. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa John John Mnyika, Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengea Kamani, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mheshimiwa Zitto K. Zuberi, Mheshimiwa Ahmed Ali Salum, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya na Mheshimiwa Susan L.A. Kiwanga. Aidha, Wabunge wafuatao wamechangia kwa maandishi. Mheshimiwa Christowaja G. Mtinda, Mheshimiwa Naomi Mwakayoma Kaihula, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Amina Mwidau, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Hawa Abdallah Ghasia, Mheshimiwa Shawana Bukheri Hassan, Mheshimiwa Stephen M. Wasira na Mheshimiwa Diana M. Chilolo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutoa shukrani kwa wataalam wa Wizara yangu ambao wamenisaidia katika kuandaa majibu ya hoja hizi. Kabla sijaanza kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, naomba kutoa ufafanuzi ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada ulioletwa katika Bunge lako Tukufu si wa kuunda Sheria mpya au wa kuanzisha mamlaka mpya, bali ni Muswada wa kufanyia marekebisho Sheria ya EPZ na ile ya SEZ ili mamlaka ya EPZ ambayo tayari ipo iweze kusimamia pia Sheria ya SEZ. Hii itapunguza gharama za uendeshaji wa mifumo hii kwa vile badala ya kuwa na taasisi mbili za kusimamia EPZ na SEZ, sasa mifumo hii itasimamiwa na Taasisi moja ya EPZA. Aidha, sheria zinazosimamia mifumo hii ni mbili tu, hamna Sheria ya tatu inayojulikana kama Sheria ya *Economic Development Zone* kama ilivyotamkwa na baadhi ya Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na Sheria moja inayounganisha sheria za *EPZ* na *SEZ*. Hata hivyo, kwa kuanzia, ilikuwa ni muhimu kuziweka sheria hizi mbili chini ya mamlaka ya *EPZ* ili kuwa mwendelezo wa mafanikio yaliyokwishapatikana katika utekelezaji wa mifumo ya *EPZ* chini ya mamlaka ya *EPZA*. Matarajio ya Serikali katika siku za usoni, ni kutunga Sheria moja itakayounganisha Sheria hizi mbili kama ilivyoshauriwa na Waheshimiwa Wabunge. Kwa maana hiyo, majibu nitakayoyotoa yatajikita katika hoja zilizolenga Muswada uliowasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja za jumla. Ziko hoja tatu kubwa za jumla ambazo zimetolewa ama na Wabunge karibu wote au zimerudiwarudiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Hoja ya kwanza ilikuwa ni hoja ambayo imetolewa na Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis. Hoja hii ilihoji ufanisi wa mfumo huu nchini na kuhoji kama kweli kuna haja ya kuwa na mfumo huu, mbona hatuoni mafanikio yake tangu umeanza kama mambo yanakwenda vizuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kufafanua, pamoja na kwamba Sheria ya *EPZ* ilitungwa na Bunge lako Tukufu mwaka wa 2002, mamlaka ya *EPZ* yenyewe imeundwa mwaka 2006 na kuanza kazi mwaka 2007. Taarifa zilizopo ni kwamba katika miaka minne ambayo mamlaka ya *EPZ* imefanya kazi, tayari makampuni 41 yanazalisha chini ya mfumo huu na tayari yanauza nje zaidi ya dola za Kimarekani milioni 350 kwa mwaka, yameajiri zaidi ya watu 11,220 siyo 10,000 kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge na yamewekeza mtaji wa zaidi ya dola za Kimarekani 650 milioni. Haya si mafanikio ya kubeza kwa kipindi ya miaka minne. Kwani kutokana na mafanikio haya haya, Benki ya Dunia imependekeza Tanzania iwe mwenyeji wa Mkutano Mkuu wa Pili wa Shirikisho wa Maeneo Huru ya Uwekezaji Afrika na pia Mkurugenzi Mkuu wa *EPZA* amechaguliwa na Shirikisho la Maeneo Huru ya Uwekezaji Duniani yaani *World Free Zones Convention* kuwa Balozi wake wa Heshima wa Afrika Mashariki. Hii ina maana kwamba kama ufanisi ungekuwa siyo mzuri hayo yote yasingefanyika hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nchi kama China, Malaysia, Thailand, Singapore, zimeweza kufikia maendeleo waliyoyapata kwa vile zimekuwa zikitumia mifumo hii zaidi ya miaka 30 wakati Tanzania ina miaka minne tu. Lengo la kuanzisha mifumo hii katika nchi yetu, ni kuvutia wawekezaji wa ndani na nje katika maeneo maalum na kwa kipindi ambacho mamlaka imekuwa katika utekelezaji ni dhahiri kwamba tunaendelea vizuri. Tukitaka kupata mafanikio makubwa kama nchi, tuwe pia tayari kutoa sadaka ya kuwekeza kwa wingi na pia tuwe tayari kuwa na subira ili mambo tunayowekeza yaweze kupata muda wa kukomaa na kutupatia matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo imesemwa sana na Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge wengi, ni hoja ya misamaha ya kodi. Hoja hii imetolewa kwa misingi kwamba misamaha ni mingi na hakuna faida inayopatikana. Hoja hii pamoja na kutolewa na Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani, vilevile Mheshimiwa Regia E. Mtema, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Zitto Kabwe

na Wabunge wengine, waliongelea kuhusu kodi hizi na wakidai kwamba ni nyingi mno, hazina faida kwa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ieleweke wazi kwamba nchi nyingi duniani zinazotumia mfumo wa *EPZ* na *SEZ*, zinatoa vivutio. Nchi za Asia zikiwemo Malaysia, Thailand, Philippines na Vietnam ambazo leo tunazisifu kwamba zimefanikiwa katika mifumo hii, zote hutoa misamaha ya kodi. Hapa Afrika nchi zote zinazotumia mifumo ya *EPZ* wakiwemo majirani zetu wa Kenya na Rwanda, wanatoa vivutio vya misamaha ya kodi. Je, Tanzania isipotoa vivutio hivyo, nani atakuja kuwekeza hapa kwetu? Si jambo la ajabu ukasikia Mtanzania anaondoka kwenda kuwekeza Kenya na Rwanda kwa sababu wana vivutio kwa sababu sisi tumeviondoa hapa kwetu! Aidha, ijulikane kwamba upotevu wa mapato unaonekana leo, unaonekana tu baada ya mwekezaji kuja lakini kinachomvutia mwekezaji huyo, ni hivyo vivutio. Hii ina maana kwamba mwekezaji asipokuja hakuna kodi itakayopatikana. Hivyo, tukiwanyima vivutio, wakaacha kuja, tutakosa vyote. Tutakosa mapato na vilevile tutawakosa wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia msamaha huu wa kodi ambao unaongelewa kuwa ni wa muda mrefu mno, kwa sababu ni wa miaka 10, kwa hakika kwa wale wote ambao wamewekeza kwenye viwanda, miaka 10 si miaka mingi mno kwa mtu kuanzisha kiwanda, kukiendesha mpaka kifike mahali ambapo kinaanza kupata faida. Uzoefu tulionao na wenye viwanda wote ni mashuhuda, kuanzia kiwanda kuanza ngazi ya chini ujenzi mpaka ufikie pale ambapo sasa mapato yanawiana na matumizi yaani kwa maana kwamba mwenye kiwanda anaanza kupata faida sasa, ni wastani wa miaka nane. Kwa hiyo tukimpa mtu miaka 10 akafanya uwekezaji pale baada ya miaka nane sasa ndiyo akaanza kupata faida, ile miaka miwili ni muda mdogo sana, lakini baada ya miaka ile miwili ataanza kulipa kodi, atatoa ajira, ataongeza mauzo nje, teknolojia mpya zitakuja katika nchi yetu na kadhalika. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge walielewe hilo kwamba kwenye upande wa viwanda siyo sawa na mtu ambaye anapewa msamaha wa kuingiza magari, akiingiza magari yake anauza palepale. Katika eneo la viwanda, ni msamaha mtu anaopewa anaanza kujenga kiwanda, kutafuta masoko, kujiweka sawa na kipindi hicho ni kirefu miaka nane kama nilivyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tatu kubwa ambayo imezungumzwa ni umuhimu wa *SIDO*. Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia umuhimu wa kuhakikisha kwamba katika mkakati mzima wa *EPZA* na *SEZ* kwa maana hiyo *SIDO* imejumuishwa. Sisi tunakubali kwamba *SIDO* ni Taasisi muhimu kwa sababu inagusa maeneo yote ya nchi yetu na kwa kweli uchungu wa Waheshimiwa Wabunge umeonekana na ambao sisi kama Wizara tunaungana nao. Lakini nataka nitoe taarifa tu kwamba Wizara ya Viwanda na Biashara ina Taasisi 17 na kila Taasisi imeundwa kwa Sheria yake na kila Taasisi ina majukumu yake na Sheria yake kama ilivyo kwa hii *EPZA*. Taasisi ya *EPZ* imepewa kushughulikiwa wawekezaji katika maeneo maalumu ambayo haya ni ya *EPZ* na *SEZ*. Taasisi ya *NDC* kwa mfano inashughulikia viwanda mama kama mnavyoona Mchuchuma na Liganga, *Soda Ash* na kwingineko. Taasisi ya *SIDO* inashughulikia viwanda vidogo vidogo. Hivyo haitakuwa rahisi kwa *EPZ* kufanya kazi za Taasisi nyingine zote kama *SIDO*, *NDC* na kwingineko. Isipokuwa *SIDO* ambayo nayo iko chini ya Wizara inatumia sheria yake kuhamasisha viwanda vidogo na

milango ya *EPZ* na *SEZ* iko wazi kwa wawekezaji wadogo ambao watapenda kuwekeza katika maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo wewe kama ni mwekezaji mdogo ambaye uko katika utaratibu wa *SIDO* unaruhusiwa kwenda katika eneo la *Special Economic Zone* kuwekeza, unaruhusiwa kwenda eneo la *Export Promotion Zone* kuwekeza, hakuna kizuizi kinachokuzuia. Lakini ukisema kwamba katika Sheria hii ya *EPZ* tuingize na *SIDO*, tutakuwa tunaingia kwenye Sheria nyingine ambayo ipo na inafanya kazi vizuri na kwa kweli *SIDO* nao wanafanyakazi nzuri kama Taasisi zingine zinavyofanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, imetolewa hoja kubwa kwamba jamani watu wadogo, Watanzania wapate nafasi, uwekezaji huu katika *EPZ* na *SEZ* unalenga watu kutoka nje tu. Napenda kusema kwamba masharti ya uwekezaji katika maeneo ya *EPZ* na *SEZ* yamerahisishwa kwa wawekezaji wa Kitanzania ambapo kiwango cha chini cha kuwekeza kwa Mtanzania ni moja ya tano ya mwekezaji kutoka nje. Kwa mfano kiwango cha chini kwa Mtanzania ni dola laki moja katika maeneo haya maalumu kwa mtu anayetaka kuwekeza pale wakati kiwango cha chini kwa mtu kutoka nje ni dola laki tano. Kwa maana hiyo, tunapoweka kiwango kidogo ni kuweka fursa zaidi kwa Mtanzania aweze kupata nafasi ya kuwekeza katika maeneo haya. Pia kwa kuzingatia umuhimu wa wawekezaji wadogo katika mchango wa Taifa, maeneo yote yanayotengwa kwa ajili ya *Special Economic Zone* yatakuwa na sehemu maalumu ya wawekezaji wadogo. Hili linafanyika na tunaahidi kwamba tunaendelea kulifanya siku zijazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya kutoa majibu kwa hizo hoja tatu kubwa za jumla, naomba sasa niende kwenye hoja moja moja ambazo zimetolewa na Wajumbe wa Kamati mbalimbali, Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza ni hoja ambayo imetolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara. Hoja hii inasema kwamba zifanyike juhudi za kuunganisha Sheria za *EPZ* na *SEZ* ili kuwa na Sheria moja ya mfumo wa Maeneo Maalumu ya Kukuza Uchumi, yaani *Economic Development Zones* utakaosimamiwa na Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Kukuza Uchumi. Hoja hiyo nimeshaijibu katika maelezo yangu ya jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili, uko umuhimu wa maeneo ya *EPZ* na *SEZ* kutengwa kwa ajili ya wawekaji wadogo wa ndani. Aidha, Kifungu kifanyiwe marekebisho na kuongezeka maneno “*and to small and medium entrepreneurs*” ili kuleta tija kwa viwanda vidogo. Hoja hii siyo tu imesemwa na Mwenyekiti wa Kamati lakini Mheshimiwa Lucy Owenya vilevile ameizungumzia alipokuwa anazungumzia wawekezaji wadogo wa ndani, Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mbunge wa Viti Maalum pia amezungumzia hoja hii na hata Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati yetu, Mheshimiwa Stella Manyanya ameisisitiza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi maeneo ya *EPZ* na *SEZ* yanahusisha wawekezaji wakubwa na wadogo bila upendeleo. Wawekezaji chini ya mfumo wa *EPZ* wana sharti moja tu nalo ni kuuza nje asilimia 80 ya bidhaa wanazozalisha bila kujali ni wakubwa au wadogo wakati mfumo wa *SEZ* hauna masharti yoyote na mwekezaji yuko huru kuwekeza ama kwa ajili ya soko la nje au kwa soko la ndani. Kwa hiyo, ukiwa mdogo, ukiwa mkubwa *SEZ* ruksa. Ukiwa mdogo, ukiwa mkubwa *EPZ* ruksa mradi tu uuze nje angalau asilimia 80.

Mheshimiwa Naibu Spika, inashauriwa neno “*acquire*” litolewe tafsiri kama litakavyotumika katika Muswada huu. Hii ni hoja ambayo ametoa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara. Neno *acquire* limetolewa ufafanuzi katika Sheria ya *EPZ*, Kifungu cha 29(1) na (2) ambapo inaelezwa kuwa Sheria ya Utwaaji wa Ardhi yaani *Land Acquisition Act*, itazingatiwa na fidia kulipwa kwa kila eneo litakalotwaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya nne ilikuwa ni Muswada huu ukipitishwa na kuwa Sheria, Serikali iharakishe kutengeneza Kanuni ili iweze kutekelezwa na Mwenyekiti ametoa hoja hiyo pia. Serikali itafanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba Kanuni zinaandaliwa mapema iwezekanavyo ili Sheria ya *SEZ* iweze kuanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tano ilikuwa ni ulipaji fidia kwa wananchi wa maeneo ya *EPZ* na *SEZ* ufanyike hasa katika maeneo ya Bagamoyo, Bunda, Songea na kwingineko. Ulipaji wa madeni ufanyike mapema na ufanyike kwa wazi bila upendeleo. Hoja hii imetolewa na Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Stephen Wasira, Mbunge wa Bunda, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mbunge wa Sumve, Mheshimiwa Regia Mtema, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Amina Mwidau, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ulipaji wa fidia kwa maeneo yaliyotwaliwa ni muhimu na la msingi. Kwa sasa Serikali ilikwisha nusu ya fidia kwa wananchi wa Bunda na itaendelea kulipa fidia kwa maeneo yaliyobaki kadri fedha zitakavyopatikana. Aidha, kwa mujibu wa *Land Acquisition Act*, baada ya utathmini wa mali kufanywa na Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali yaani *Chief Government Valuer*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya sita kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ilikuwa ni Mamlaka ya *EPZ* itangaze na kuwaelimisha wawekezaji wa ndani na wajasiriamali wadogo juu ya fursa za uwekezaji katika maeneo ya *EPZ* na *SEZ*. Hoja hii sio tu kwamba ilitolewa na Mwenyekiti wa Kamati hii, lakini Mheshimiwa Amina Mwidau na Mheshimiwa Mansoor Shanif Hiran, walisisitiza hilo. Ushauri wa Kamati utazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha Mamlaka ya *EPZ* imekuwa ikihamasisha jamii kupitia mikutano ya uwekezaji, matangazo redioni na kwenye runinga, vipeperushi na mikutano katika Halmashauri za Wilaya na Mabaraza ya Madiwani. Kwa sasa Mamlaka

ya *EPZ* imekwishafanya mikutano ya uelimishaji kwa Halmashauri na Madiwani wa Kigoma, Bagamoyo, Meru na Manyara. Juhudi za kutoa elimu kwa maeneo mengine zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya saba ilikuwa ni kwamba Kamati inashauri masuala yote yanayohusu ardhi na uwekezaji yafanyike kwa kufuata Sheria ya Ardhi na Sheria ya Ardhi ya Vijiji yaani *Land Village Act*. Pamoja na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara vilevile Mheshimiwa Mansoor Shanif Hiran, Mbunge wa Kwimba, alisisitiza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utwaaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji umekuwa ukifanyika kwa mujibu wa Sheria ya *EPZ*, Kifungu cha 29(1), ambacho kinahusu utwaaji wa ardhi kwa kutumia Sheria ya Atwaaji wa Ardhi yaani *Land Acquisition Act*. Aidha, katika utwaaji wa maeneo ya uwekezaji, Sheria ya Ardhi ya Vijiji huzingatiwa, ambapo mikutano ya Serikali ya Vijiji hufanyika na kuhusisha Mabaraza ya Madiwani na ushahidi ni kwamba hata kule Bagamoyo hili tumelifanya kwa wale wanavijiji na Waheshimiwa Madiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya nane ilikuwa ni Katibu Mkuu wa *TUCTA* awe Mjumbe wa Bodi, Mkurugenzi Mtendaji wa *EPZA* awe Katibu wa Bodi na mwakilishi wa *TRA* aondolewe kwa vile Katibu Mkuu wa Wizara Fedha yupo kwenye Bodi. Kwa mujibu wa Kifungu cha 17(3) cha Sheria ya *EPZ*, Mkurugenzi Mkuu wa *EPZA* ndio Katibu wa Bodi. Aidha, ushauri wa kumweka Katibu Mkuu wa *TUCTA* na kumwondoa mwakilishi wa *TRA*, utazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tisa. Neno “*minerals*” katika Kifungu cha 6 kinachofuta maneno ya Kifungu cha 14 na kubadilisha maneno mengine liondolewe na kuwekwa neno “*energy*”, Mwenyekiti wa Kamati alilizugumzia hili. Kiambatanisho cha Marekebisho yaani *Schedule of Amendments* kilichosambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge, kimezingatia ushauri huo na marekebsho yameshafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kumi ilikuwa ni kuondokana na tatizo la urasimu katika kitengo cha *TRA* unaochelewesha malighafi bandarini. Kamati inashauri kwamba Afisa wa *TRA* atakayekuwepo katika eneo la uwekezaji apewe mamlaka kamili ya maamuzi yanayohusu kodi. Pamoja na Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mheshimiwa Naomi Mwakyoma Kaihula, Mbunge wa Viti Maalum, alisisitiza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa kwa wawekezaji katika maeneo ya *EPZ* na *SEZ* zinakuwa na ufanisi mkubwa, Serikali inakamilisha taratibu za kuanzisha Kituo Kimoja cha Huduma yaani *One Stock Service Centre*, katika eneo la Benjamin William Mkapa – *SEZ*. Kituo hiki kitahusisha wawakilishi wa taasisi zote muhimu katika masuala ya uwekezaji kama vile *TRA*, Uhamiaji, Wizara ya Kazi yaani masuala ya kazi, Mazingira – *NEMC* na kadhalika. Baada ya eneo la Benjamin William Mkapa, tukianzisha eneo lingine likikamilika tutaweka *One Stock Service Centre* vilevile. Aidha, Serikali itazingatia ushauri wa

Kamati kwa kuziomba taasisi husika, hususan Wizara ya Fedha na *TRA*, kuleta Maafisa watakaoweza kutoa maamuzi kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niende kwenye hoja ambazo zimetolewa na Kambi ya Upinzani. Kambi ya Upinzani inasema kwamba tafiti nyingi zilizofanyika zimeonesha mashaka makubwa ya faida zipatikanazo na mipango ya namna hii, Mheshimiwa Lucy Owenya, alisema. Inawezekana kabisa kama Mheshimiwa Owenya, ameona tafiti za zamani, lakini hali halisi duniani ni kwamba nchi nyingi hususan za Asia na Mashariki ya mbali zimeweza kukua kiuchumi na kujenga uchumi kwa kupitia mifumo hii. Aidha, maendeleo ya kukua uchumi kwa nchi kama China, Vietnam, *South Korea*, Falme za Kiarabu, ni kupitia mifumo hii. Zaidi ya 60% ya bidhaa zinazouzwa nje ya nchi nchini China, zinazalishwa katika maeneo ya *EPZ* na *SEZ* na wafanyabiashara wanaokwenda China na hata Waheshimiwa Wabunge mkienda China mtagundua kwamba maeneo haya ndiko ambako bidhaa nyingi za kuja Tanzania zinatoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili, mipango ya *EPZ* na *SEZ* inanufaisha wachache hususan wale wanaotoka nje. Hilo nimeshalijibu lakini nirudie tu kwa msisitizo kwamba mipango ya *SEZ* na *EPZ*, ipo wazi kwa wawekezaji wote na sio wa nje tu. Tunapooonga twende kwa takwimu; takwimu nilizonazo mimi zinaonesha kuwa kwa sasa hivi 44% ya wawekezaji wa *EPZ* ni Watanzania, 15% ni makampuni ya ubia kati ya wageni na Watanzania na 41% ndio makampuni ya wageni pekee. Kwa hiyo, sio sahihi kusema kwamba *EPZA* inapendelea wageni na kuwaacha wazawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii, maadam milango ya *EPZ* ipo wazi, maadam milango ya *SEZ* ipo wazi, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tuwahimize wafanyabiashara, tuwahimize watu wenye mitaji na sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge, tuna mitaji kidogo, twende tukawekeze katika maeneo haya na kama kuna mtu ambaye atazuiwa, basi aje hapa Bungeni atoe ushuhuda kwamba *SEZ* inapendelea mtu ambaye ni wa nje. Lakini milango ipo wazi, nawaombeni sana Waheshimiwa, badala ya kusema tu bila *data*, twendeni tukawekeze ili na sisi tuweze kunufaika na mfumo huu ambao upo hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tatu ni kwamba tathmini inaonesha kwamba miradi hii haijakidhi madhumuni ya kuanzishwa kwake, hoja hii imesemwa vilevile na Kambi ya Upinzani na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani na yeye amesema hivyo. Hoja hii nimeshajibu katika maelezo yangu ya awali. Mfumo huu una miaka minne tu, wenzetu ambao tunajilinganishanao wamekaa miaka 30 na zaidi. Tujipe muda na tuwekeze kwa nguvu, tutaona mafanikio ya mfumo huu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya nne ilikuwa ni kwamba hakuna taarifa za miradi ya Mbegani Bagamoyo na Kigoma *Special Economic Zone*, kuhusiana na misaada kutoka Serikali ya China na Benki ya Maendeleo ya China. Hili sio tu kwamba kalisema Mheshimiwa Owenya, vilevile Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mbunge wa Kigoma Kaskazini amelisema. Miradi ya Bagamoyo *SEZ* na Kigoma *SEZ*, iliwasilishwa katika Benki ya Maendeleo ya China yaani *China Development Bank* na mazungumzo ya kupata



msaada wa Serikali ya China yapo katika hatua nzuri. Aidha, ujumbe kutoka Benki ya Maendeleo kutoka China, utafika nchini Ijumaa tarehe 15 April, 2011 kujadili suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tano ni kwamba vivutio vinavyotolewa ni vingi na hii ni mbinu ya kuiuza nchi yetu kwa wageni. Hoja hii nimeshaitolea maelezo, hatuna mpango wa kuuza nchi yetu kwa sababu kwanza wanaowekeza kule walio wengi zaidi ni Watanzania lakini natumia fursa hii kurudia kusema kwamba *SEZ* na *EPZ* ipo wazi kwa kila mtu. Sisi Watanzania badala ya kuwaogopa wageni, ninatoa wito, Watanzania twendeni tukawekeze kwa nguvu. Hata kama ni kiwanda kidogo *SEZ* inakufungulia, hata kama ni kiwanda kidogo *EPZ* inakufungulia, ilimradi lakini uhakikishe kwamba unauza angalau 80% ya bidhaa zako nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya sita, ni kwa nini atajwe Rais wa *TCCIA* na Mwenyekiti wa *TPSF* badala ya mwakilishi kutoka katika asasi hizo. Katika Bodi, tumemtaja Rais na Mwenyekiti halafu uwakilishi wa asasi za kiraia na vyama vya wafanyakazi pamoja na wawakilishi kutoka Mikoani uwepo kwenye Bodi ya *EPZA*. Hiyo ni Kambi ya Upinzani lakini vilevile Mheshimiwa Mansoor Shanif Hiran, Mheshimiwa Mbunge wa Kwimba na yeye vilevile aliisisitiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wa *Tanzania Chamber of Commerce and Agriculture* na Mwenyekiti wa *Tanzania Private Sector Foundation*, wameteuliwa kutokana na nafasi zao. Hawa ni watu walioteuliwa na wawakilishi wao hivyo hakuna haja ya kuwatilia mashaka. Kwa hiyo, kama kesho watabadilishwa na taasisi zao, sisi tutawapokea wale wapya ambao watakuwa wamebadilishwa. La pili, sio rahisi kuweka wawakilishi wa taasisi zote, labda kila Mkoa kumweka mwakilishi; isipokuwa kwa upande wa Mikoa, Wakuu wa Mikoa, wanawakilishwa na Katibu Mkuu – *TAMISEMI* ambaye ni Mjumbe wa Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kujibu hoja hizo, sasa naingia kwenye hoja moja moja za Waheshimiwa Wabunge. Hoja ya kwanza ni ya Mheshimiwa Naomi Mwakyoma, Mbunge wa Viti Maalum, inasema kwamba Sheria ya *EPZ* na *SEZ* zifafanuliwe kwa Kiswahili, *popular version*, ili wananchi wote wazielewe. Ushauri wa Mheshimiwa Mbunge utazingatiwa wa kuandaa makala rahisi kwa lugha ya Kiswahili ili kurahisisha utoaji wa elimu ya mifumo ya *EPZ* na *SEZ* kwa wananchi, hasa wakati unakwenda kufanya ile huduma katika Mikoa na katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ni ya Mheshimiwa Chritowaja Gerson Mtinda, Mbunge wa Viti Maalum, ambaye anasema kwamba mazingira ya uwekezaji yawekwe sawa kwa wawekezaji wote wawe wa nje na wa ndani, kwani wawekezaji wa nje wamekuwa wanapewa vivutio vingi kama kutolipa Kodi za Forodha, *VAT* kwenye mitambo na kadhalika. Narudia tena, mazingira ya uwekezaji yako sawa kwa wawekezaji wote. Waheshimiwa Wabunge, tumieni fursa zenu, tembeleeni maeneo haya ya *EPZ* na mtagundua kwamba hata ukienda pale kutafuta, utapata fursa sawa na mgeni isipokuwa wewe utaambiwa kwamba uwe na mtaji kidogo zaidi kwa sababu tunafahamu hali yetu ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namba tatu ni wawekezaji wanapewa vivutio vingi pamoja na kuhakikishiwa miundombinu na kusamehewa kodi miaka 10. Amesema Mheshimiwa Christowaja, Mheshimiwa Leticia Nyerere na yeye amelisema hili. Nimeshalijibu hili vizuri kabisa kwamba kabla ya mwekezaji yeyote kuruhusiwa kuwekeza katika maeneo ya *EPZ* hutakiwa kuingia mikataba kati yake na mamlaka ya *EPZ* ambayo huwa na vigezo maalum vya utekelezaji. Katika kipindi cha utekelezaji, mamlaka ya *EPZ* hufuatilia utendaji wa mwekezaji husika kwa karibu. Endapo itabainika kwamba mwekezaji hatekelezi wajibu wake kulingana na mkataba, mamlaka ya *EPZ* huwa na mamlaka ya kuuvunja mkataba huo. Hii huwabana wawekezaji ili watekeleze majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongezee hapo, unaposema mtu amewekeza kwenye kiwanda, ametoa mtaji wake katika nchi yake au katika mfuko wake, hata kama ni Mtanzania, akawekeza labda dola milioni 10 katika eneo, sasa itakuwa ni sababu nzito sana kwake yeye aondoke aache kile kiwanda pale maana akiondoka akakiacha kile kiwanda pale ni kwamba *EPZ* itakichukua na kumkodisha mtu mwingine, kwa hiyo atakuwa amepoteza yeye. Ingekuwa ni mtu anayenunua bidhaa nje na kuiuza hapa, hapo ungeweza kuwa na hofu hiyo lakini kwa sababu ni mtu ambaye analeta mtaji wake, anawekeza *structure*, anawekeza mitambo, sasa akiamua kuondoka ni kwamba amepata hasara yeyé lakini *EPZA* itakuwa imepata faida kwa sababu itamchukua mtu mwingine na kumweka pale na yule mtu anatalipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya nne ilikuwa ni uwekezaji katika maeneo ya *EPZ* na *SEZ* uangalie maeneo nyeti kama vile kilimo ili kuwakwamua wananchi. Hii imetolewa na Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum. Mfumo wa *SEZ* unahusisha uwekezaji unaolenga maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na viwanda, biashara, kilimo na kadhalika. Hivyo, mwekezaji yeyote aliye tayari kuwekeza katika kilimo chini ya mfumo wa *SEZ* anakaribishwa. Aidha, Mamlaka ya *EPZ* itaendelea kuhamasisha uwekezaji katika maeneo mbalimbali likiwemo kilimo chini ya *SEZ* kama alivyosema Mheshimiwa Nyerere, tuweke mpaka *horticulture* na kadhalika. Tunawakaribisha watu wanaopenda kuwekeza katika *horticulture* waje na tutawapatia maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namba tano ilikuwa ni, utengaji wa maeneo ya uwekezaji ulenge sehemu zenye maeneo makubwa badala ya kuingilia maeneo ya wananchi yasiyo makubwa na kuleta usumbufu kwa wananchi na kuleta ubadhirifu wa fedha za Serikali; Mheshimiwa Christowaja, amezungumzia hili. Utwaaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji umekuwa ukifanyika kwa mujibu wa Sheria ya *EPZ*, Kifungu cha 29(1) kama nilivyosema, ambacho kinahusu utwaaji wa ardhi kwa kutumia Sheria ya Utwaaji Ardhi, yaani *Land Acquisition Act*. Aidha, katika utwaaji wa maeneo ya uwekezaji, Sheria ya Ardhi ya Vijiji huzingatiwa ambapo Mikoa, Wilaya na Mikutano ya Serikali za Vijiji hufanyika na kuhusisha Mabaraza ya Madiwani. Kwa hiyo, ni wananchi wenyewe ndio wanaomba kwamba jamani tuna eneo hapa na tuko tayari kulipwa fidia ili eneo hili liweze kutumika kwa ajili ya viwanda na sisi tunafanya vile kwa sababu ya faida ambazo nimezitaja pale awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya sita, ni eneo la *EPZ* linalozunguka bandari ya Mtwara, lilitengwa muda mrefu na hakuna shughuli inayoendelea. Ni kwa nini Serikali iendelee kutafuta maeneo zaidi wakati yale ya awali hayajaendelezwa? Hilo limeulizwa na Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini. Eneo linalozunguka bandari ya Mtwara liko chini ya Mamlaka ya Bandari ya Tanzania ambapo uwekezaji utafanyika kwa kushirikiana na Mamlaka ya *EPZ*. Nia ya Serikali kutafuta maeneo katika Mikoa mbalimbali ni kuhakikisha kuwa kila Mkoa una maeneo ya uwekezaji na uendelezaji wa shughuli za kiuchumi ambako mwekezaji akipatikana eneo la uwekezaji linakuwepo. Kwa hiyo, tuna eneo pale Mtwara kweli, lakini bado tunahitaji maeneo katika Mikoa mingine kwa sababu Watanzania wote wanahitaji kunufaika na fursa za *EPZ* na *SEZ*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya saba ilikuwa ni eneo la Benjamin Mkapa *SEZ*, bado halijaweza kuvutia wawekezaji kwa kuwa lina kiwanda kimoja tu kinachofanya kazi. Aidha, eneo hili lina maji ya kutosha wakati maeneo ya jirani na pia eneo la *Millenium* hayana maji. Mamlaka ya *EPZ* itoe huduma kwa jamii *corporate social responsibilty* na hili limesemwa vizuri sana na Mheshimiwa John Mnyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio makubwa yamepatikana kutokana na kuanzisha eneo la Benjamin William Mkapa *SEZ*, ambapo tayari viwanja vyote vimeshakodishwa kwa wawekezaji ambao watajenga viwanda 15. Aidha, viwanda 10 tayari vimeanza ujenzi wa majengo na kiwanda kimoja kimeanza uzalishaji. Viwanda hivi vitaajiri zaidi ya wafanyakazi 2,000 na tayari mipango imewekwa kwa kushirikisha Serikali ya Mtaa wa Makuburi ili wananchi wa eneo hilo wapewe kipaumbele kwenye ajira kulingana na sifa na ujuzi. Pia Mamlaka ya *EPZ* imekuwa ikitoa huduma mbalimbali kwa jamii inayowazunguka kwa mfano ujenzi wa mifereji ya maji taka, kununua samani za Ofisi ya Mwenyekiti wa Mtaa wa Makuburi na mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba kwa haya yote kufanyika kwa kipindi cha miaka minne, nina hakika Mheshimiwa Mbunge wa Ubungo ataona kwamba angalau tunajitahidi. Ni kweli kiwanda ni kimoja, lakini kama vinakuja 15 ndani ya miaka michache, nafikiri Mheshimiwa Mbunge wa Ubungo angeamua baadaye atumie busara zake aunge mkono hoja hii ili wale wafanyakazi na wananchi wa Ubungo ambao anawatumikia waweze kuona kwamba anaunga mkono kitu ambacho kinahitaji muda kwa kweli. Kuanza kiwanda sio sawa na kuanza biashara tu ya kuingiza magari au kuingiza nguo. Kwa hiyo, hofu kwamba hakuna kinachofanyika, naomba iondoke. Ni uwekezaji wa muda mrefu na tukipata kuungwa mkono na wewe Mheshimiwa Mnyika na Waheshimiwa Wabunge wengine, nafikiri matunda ambayo tunayategemea kama Wabunge na kama Watanzania, tutayaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hili la Bodi ya Mamlaka ya *EPZA*, ina uwakilishi mkubwa wa watendaji wa Serikali, ikiwemo kuongozwa na Mheshimiwa Waziri kama Mwenyekiti. Hii ni kinyume cha taratibu zinazotumika kwenye taasisi nyingine; ni Mheshimiwa John Mnyika, huyu amesema. Uzoefu wa nchi nyingine zinazotumia mifumo hii umeonesha kwamba Bodi zinazosimamia Mamlaka hizi ni vema zikawa na uwakilishi kutoka ngazi za juu za Serikali ili kuhakikisha kuwa maamuzi yanayotolewa

yanatekelezwa mara moja. Aidha, jukumu kubwa la Bodi ni kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji, jukumu ambalo ni la Serikali. Mfano, nchi ya Ghana na India, Mwenyekiti wa Bodi ni Waziri wa Viwanda na Biashara, ambapo nchi ya Bangladesh Mwenyekiti ni Waziri Mkuu. Aidha, sehemu kubwa ya Wajumbe wa Bodi ya EPZA Kenya, ni Makatibu Wakuu kama ilivyo hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tungeweza kusema kwamba tufanye kama Bodi nyingine zinavyofanya, lakini kwa sababu hapa kuna maamuzi mazito ya kupata maeneo ya ardhi, kuna maamuzi mazito ya kuhakikisha kwamba vivutio vinapatikana, kuna maamuzi mazito ya kuhakikisha kwamba mwekezaji ambaye analeta dola zake milioni 100, 500, hasumbuliwisumbuliwi, ndio maana ikaonekana kwamba ni vizuri Bodi hii ikawekwa katika namna ambayo inaweza ikafanya maamuzi na maamuzi yale yasichelewe. Wawekezaji hawa sio watu ambao wana muda mrefu wa kupoteza, kwa hiyo ikaonekana kwamba ni vizuri, hata mwekezaji wa hapa Tanzania akiamua kuwekeza katika maeneo ya EPZ na SEZ asingependa kukaa mwaka mzima akiwa anasubiri Serikali kufanya maamuzi; ndio maana ikaonekana kwamba ni vizuri Bodi hii Waziri akawa ndio Mwenyekiti mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejitahidi kwa kadri ya uwezo wangu kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge na nina uhakika nimezimaliza karibu zote. Kama kuna ambazo nimeziacha basi nafikiri wakati wa Vifungu Waheshimiwa Wabunge, wasisite kuuliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa majibu hayo, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

## **KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Maeneo ya Maendeleo ya Kiuchumi wa Mwaka 2011 *(The Economic Zones Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2011.***

Kifungu cha 1  
Kifungu cha 2  
Kifungu cha 3  
Kifungu cha 4

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Mabadiliko yake)*

Kifungu cha 5

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha marekebisho kwa Kifungu husika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba nisome, *amendment of section 3(1) ya Principal Act to insert Kifungu cha 5 kinachosema, the Principal Act is amended in section 3(1) by inserting the following sub-paragraph:-*

*(c) establish Small and Medium Export Centers within the Export Processing Zone established under this Act.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa mujibu wa Kanuni nieleze kidogo sababu za marekebisho haya, pamoja na maelezo mazuri ambayo ameyatoa Waziri kuhusiana na fursa za wafanyabiashara kwamba ziko sawa kwenye uwekezaji, kwenye eneo hili kuna ukweli mwingine tofauti katika taarifa ambazo Wizara yake imewasilisha kwa Kamati husika ambazo zinaeleza kiwango cha mitaji ambacho wanaowekeza ndani ya *Exports Zone* wanatakiwa kuwanacho. Kiwango ambacho wafanyabiashara wa kati na wafanyabiashara wa chini hawawezi kuwa nacho. Lakini hawa vilevile nao ni wawekezaji wanaostahili motisha kwa ajili ya Taifa letu na kwa ajili ya kutengeneza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo basi, naomba kupendekeza marekebisho madogo kwenye Sheria kwa kuingiza hiki kifungu (c) *establish Small and Medium Export Centers within the Export Processing Zone established under this Act* ili katika zile *Export Zone* kuwe na *centre* ambazo wafanyabiashara wa kati na wafanyabiashara wa chini watawekewa maeneo yao maalum ndani ya *Export Processing Zone* kwa ajili ya kuboresha vilevile eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mnyika na Waheshimiwa Wabunge kwamba wawekezaji wadogo ni muhimu, lakini napenda nirudie nilichosema kwamba *SME*, hii sekta ya biashara na viwanda vidogo vidogo ni sekta ambayo iko chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara kama ilivyo *EPZ* na inasimamiwa kwa karibu sana *SIDO*. *SIDO* ina Sheria yake, tukichukua Kifungu anachosema Mheshimiwa Mnyika tukaingiza kwenye Sheria hii, ina maana kwamba tunaingiza Sheria moja ndani ya Sheria nyingine kwa mamlaka mbili ambazo ziko chini ya Wizara moja na Wizara ambayo inawahakikishia Waheshimiwa Wabunge na Bunge hili kwamba mambo hayo ambayo nimeyesema kweli yanafanyika. Kwamba ukiwa unawekeza pale *EPZ* kama wewe ni mwekezaji mdogo ukishafikia kile kiwango kidogo cha fedha na tuseme kitu kimoja hapa kwamba ukienda pale kwa mfano kuwekeza kwa ajili ya kuuza nje, dola 100,000 kwa kiwanda kidogo si fedha ya kutisha dola 100,000 ni fedha ya kiwanda cha kawaida kabisa na kama wawekezaji wadogo wakiungana wawili, watatu wanawekeza mpaka dola 500,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo kuweka mpaka dola 100,000 kwa kweli ni kiwango ambacho ni *reasonable* kwa mtu ambaye anauza nje. Lakini kwa *Special Economic Zone* chochote ulichonacho, dola 20,000, dola 10,000 unawekeza pale na hupewi masharti kwamba lazima uuze asilimia 80 nje. Kwa hiyo wewe ukizalisha pale, ukiuza soko la ndani ruksa, ukiamua kuuza nje ruksa na milango iko wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena, Bunge lako liweke kumbukumbu sahihi kwamba milango ya *EPZ* na *SEZ* iko wazi kwa mwekezaji mdogo, wa kati na mwekezaji wa kiwango cha juu. Serikali haioni umuhimu wa kuingiza Kifungu hicho kwenye Sheria hii wakati tayari *a small and medium enterprises* zinakuwa *guided* na Sheria nyingine ambayo iko chini ya *SIDO* na vilevile utekelezaji wa anachosema Mheshimiwa Mnyika unafanyika kwa dhati. (*Makofi*)

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dola 100,000 kwa *exchange rate* ya karibuni ni shilingi takribani milioni 120 mpaka milioni 150 lakini tunapozungumzia kuhusu uuzaji wa mali kutoka nje kama tunataka kuwawezesha wazawa kwa wingi zaidi tunaweza kuwa na wazawa wa mitaji midogo zaidi lakini wenye kuuza mali nyingi na hii haitakuwa kitu kigeni kuweka *centers* ndani ya *zones*, kuna nchi zinafanya haya, Tanzania haitakuwa kisiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi nitaunga mkono Muswada huu kama Kifungu hiki ambacho ni cha kuweka *center* tu wala sio kizibadili *Export Processing Zone* kugeuka kuwa za wajasiriamali wadogo, bali ni kuweka *special consideration*, hata kuwakuza, hakitakubaliwa. Kama Kifungu hiki kitaingizwa, binafsi Mheshimiwa Mwenyekiti niko tayari kuunga mkono Muswada huu. (*Makofi*)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kama malumbano haya yanapoteza lengo la utungaji wa *Economic Processing Zones* na mamlaka ya *SIDO* ya kushughulikia aina ya shughuli za biashara na uzalishaji ambazo anazizungumzia Mheshimiwa Mnyika. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, Sheria hii ni tofauti na haya malengo ambayo Mheshimiwa Mnyika ameyaleta hapa na kwa kweli hiki ni kitu tofauti kabisa ambacho kinashughulikiwa katika sehemu nyingine kwa sababu *SIDO* wanayo mamlaka ya kufanya hivyo. Maeneo haya yametengwa kwa ajili ya madhumuni yale ambayo yamewekwa kwenye ile Sheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika umeridhika?

(*Hapa Mhe. Mnyika alionyesha ishara ya kuridhika*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa naomba niwahoji Waheshimiwa Wabunge kama tulivyofanya jana, tuelewane vizuri kwanza, natumaini tumelewa kuhusiana na

mjadala uliopo wa wazo linalotolewa na Mheshimiwa Mnyika ambalo limeletwa hapa katika *Schedule of Amendment* ambayo ameishaita kwa utaratibu, nalo ni kuanzisha *Export Centers* za wawekezaji wadogo na wa kati kwenye utaratibu ule ambao tunauzungumzia hapa na Serikali inasema kwamba hao wadogo na wa kati wana utaratibu wao mwingine ambao una Sheria nyingine.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 6  
Kifungu cha 7  
Kifungu cha 8  
Kifungu cha 9  
Kifungu cha 10

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 11

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 12

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lako Tukufu liridhie marekebisho kwenye Kifungu cha 12 ambacho kinafanya marekebisho ya kifungu cha 8 kwenye Sheria ya msingi kwa kuingiza Kifungu Kidogo cha 4 kinachosomeka kama ifuatavyo:-

*“For the purpose of effective use of special economic zones, there shall be established Small and Medium Economic Centers within each Specified Economic Zone established under this Act.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya marekebisho haya pamoja na maelezo ambayo yaliyotolewa na Waziri wakati wa Kifungu kile kilichotangulia, ukweli ni kwamba *jurisdictions* yaani mamlaka ya *SIDO* kufanya kazi kwa mujibu wa ile Sheria hayahusu kufanya kazi ndani ya maeneo ambayo yametengwa kuwa maalum kabisa kwa ajili ya shughuli hizi za kiuchumi kwa sababu maeneo yale yametengwa kuwa maalum kabisa na *SIDO* haina mamlaka ya kwenda kufanya kazi kule ndani. Kuna kila sababu ya kuweka vituo maalum mle ndani, *centers* ndogo kwa ajili ya wajasiriamali hawa kwa lengo la kupanua wigo wa uwekezaji wa ndani na kuwajengea uwezo wazawa wa ndani vilevile na kuongeza faida kutokana na wazo hili la kuwajenga wajasiriamali wadogo na kuwakuza hawa ili baadaye wawe wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, iko tofauti kubwa sana kati ya fikra na sera na hili suala kwa kweli ni sera kwa sababu unaweza kusema hata machinga pia waingie kwenye hizi *zones* lakini kwa sera ambayo tunayo na ambayo kwayo tumetunga sheria hii mimi nilikuwa namshauri Mbunge, Mheshimiwa Mnyika akubali kwamba kwa msingi uleule ambao tumeamua kwamba hili suala lishughulikiwe tofauti na anavyopendekeza iwe hivyo hivyo.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na nashukuru kwa maelezo mazuri ya Mwanasheria Mkuu. Mwanasheria Mkuu amezungumzia suala la kisera na mimi nazungumza suala la kisera. Ukiangalia kwenye *objectives* ama madhumuni ya Muswada huu, ni kwamba Muswada unakusudia kufanya Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Maeneo ya Uwekezaji kwa Mauzo ya Nje na kadhalika, kwa ajili ya kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji wa kigeni na wa ndani, hiyo ndiyo *policy*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tunataka kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji *unless* tuambiane kwamba sera ni kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji kwa wawekezaji wa nje na wawekezaji wenye mitaji mikubwa. Mkisema hiyo ndiyo sera basi hii itakuwa haina maana lakini kama uwekezaji haubagui, tunapotoa *preferential arrangement* kwa wawekezaji wakubwa na wa nje, lazima tuangalie mazingira, sio kwamba tunataka kugeuza haya maeneo kuwa maeneo ya wamachinga, wafanyabiashara wachuuzi, tunazungumza kuhusu wazalishaji wadogo na wengine wanazalisha vitu ambavyo vina mauzo makubwa sana nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi bado nasisitiza kwamba tuna haja ya kuzingatia hizi *arrangement* ili kuweka mazingira ya motisha ambapo *SIDO* haina mamlaka ya kuyashughulikia, inaweza kushughulikia nje ya *EPZ*, nje ya *SEZ* lakini haiwezi kushughulikia ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MWENYEKITI:** Mwongozo, Mheshimiwa Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa na mimi ni mdau wa Muswada huu, ni kwamba mazungumzo anayoelezea Mheshimiwa Mnyika ni sawa lakini kwa mujibu wa Muswada huu ni kama ambavyo tulielekezwa na Mheshimiwa Waziri kwamba amekubali kuna maeneo ambayo yatawahusu hao wajasiriamali wadogo na wa kati katika maeneo ya *SEZ*. Sasa ni jinsi gani shughuli hizo zitafanyika hapo na kwa utaratibu upi, nadhani haya yanaweza yakawekwa kwenye taratibu, ahsante.



**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kama alivyosema Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tulishapita katika kipengele hiki na kuhoji Bunge lako Tukufu lakini napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mnyika na Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Watanzania kwamba Wizara ya Viwanda na Biashara inawajali sana wawekezaji na wafanyabiashara wadogo wadogo. Tuna Idara zima inashughulikia watu hawa, tuna Idara ya *DSME* na vilevile tuna *SIDO* ambayo inafanya kazi nchi nzima. Kinachofanya Mheshimiwa Mnyika na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wengine wanazungumzia jambo hili kwa uchungu ni kwa sababu wanaona kabisa kwamba kumbe *SIDO* ikiwezesha inaweza lakini Mheshimiwa Mnyika ajue kwamba hiyo *SIDO* inafanya kazi kwa kupitia taratibu ambazo nazo zinasimamiwa na Wizara yangu mimi na Wizara yangu tunasimamia suala la *SIDO*, *EPZ* na *NDC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaposema kwamba tunatekeleza kama anavyosema Mheshimiwa Mnyika, tunasema kweli kwamba tunatekeleza kama anavyosema katika maeneo yote ya *SEZ* na niseme hapa ili Watanzania wanisikilize katika maeneo yote ya *EPZ* mwekezaji mdogo, wa kati, mkubwa anaruhusiwa kuja kuwekeza pale. Nirudie kwa sababu kuna jambo linafanyika hapa la kuwafanya Watanzania waone kwamba mamlaka hii ipo kwa ajili ya wageni, asilimia ya wageni walioko katika *EPZ* ni 41 tu nyingine zote ama ni wazawa ambao ni 44 na 15% ni ubia kati ya wazawa na watu kutoka nje. Kwa hiyo, niseme kwamba tungekuwa na mitaji, kusingekuwa na haja ya kutafuta mtu kutoka nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe *challenge* kwa Watanzania, hebu leteni mitaji yenu tuone kama Wizara itaruhusu mtu kutoka nje awekeze pale kwa sababu hatuna mitaji ya Kitanzania ndiyo maana tunaruhusu mtu kutoka nje lakini hatumzuii. Hatuna kipengele cha kum-*favor*, cha kumpa kipaumbele mwekezaji kutoka nje na tukamkandamiza Mtanzania. Ndiyo maana nikasema kiwango cha chini cha Mtanzania kuwekeza ni moja ya tano ya kiwango cha chini cha mwekezaji kutoka nje kuwekeza, nikatoa ile *figure* ya dola 100,000 kwa Mtanzania na dola 500,000 kwa mtu kutoka nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaweza tuka-*debate* mpaka asubuhi kwamba dola 100,000 ni nyingi kwa Watanzania na kadhalika lakini kwa watu ambao wana viwanda na mtu ambaye anawekeza kiwanda ambacho anauza bidhaa nje, hakika dola 100,000 sio fedha ya kutisha lakini kama dola 100,000 ni fedha nyingi, maeneo ya *SEZ* yanakuruhusu uende pale hata dola 10,000 ukawekeze pale. Sasa ukiweza kuwekeza kwa dola 10,000 pale ukiona kwamba una-*graduate* unafika dola 100,000 basi una *shift* kutoka *SEZ* unakwenda *EPZ*, unapata vivutio, unanza kuzalisha kwa ajili ya nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nataka niombe tu jamani tulipe *flexibility* kwamba tunaweza tukaongea tu hapa kwa ajili ya kuwafanya watu waone kwamba tuna uchungu nao lakini niwahakikishie kwamba Serikali hii ina uchungu na Watanzania, Wizara ina uchungu na wawekezaji wote, wawekezaji wadogo, wawekezaji wa kati na wawekezaji wakubwa, wote tunawajali kwa sababu wanapowekeza hata yule

mkubwa ambaye tunajifanya kumkandamiza hapa, anapowekeza anajenga ajira. Pale Kisongwa Arusha kuna mwekezaji mmoja ambaye amewekeza *EPZ* pale, anaajiri wafanyakazi 6,000 wa Kitanzania, hiyo ni faida kwa nchi, sio faida?

**MBUNGE FULANI:** Faida!

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Sasa hatuwezi kumkataa kwa sababu tu ni mkubwa, lakini hata kama sisi tumeshindwa kuwekeza basi angalau tunapata ajira. Kwa hiyo, sisi tuliangalie *positively* badala ya kuona kila kitu ambacho Serikali inafanya ni kibaya, kila kitu ambacho inafanya Serikali tunapindisha tu ili tuonekana na wananchi labda kwamba labda sisi ndiyo tunawapenda wananchi kuliko Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwahakikishia Watanzania kwamba Wizara ya Viwanda na Biashara, Mamlaka ya *EPZ* itafanya kila liwezekanalo kuhakikisha kwamba mwekezaji mdogo anapata fursa sawasawa na mwekezaji wa kati, sawasawa na mwekezaji mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika kwa mara ya mwisho, amekubaliana, Kifungu hicho kinaafikiwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 13

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 14

Kifungu cha 15

Kifungu cha 16

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**(Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kufanya Marekebisho katika Sheria ya Kusimamia Maeneo ya Uwekezaji kwa Mauzo ya Nje na Maeneo Maalum ya Kiuchumi kwa Lengo la Kuweka Mazingira Mazuri ya Uwekezaji wa Kigeni na wa Ndani Pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na hayo (*A Bill for an Act to Amend Laws Relating to Economic Development Zones With a View to Rationalize Laws and Functions of the Exports Processing Zone Authority in Relation to Export Processing Zones and Special Economic Zones and to provide for other related Matters*))**

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Muswada wa Sheria wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Maeneo ya Maendeleo ya Kiuchumi wa Mwaka 2011 (*The Economic Zones Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2011*).

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Dr. Cyril A. Chami, umetoa hoja na imeungwa mkono, sasa wajibu wangu ni kuwahoji kuhusiana na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Maeneo ya Maendeleo ya Kiuchumi ya Mwaka 2011, *The Economic Zones Laws Bill, 2011*.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa kwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa taratibu zetu za Kibunge Muswada ulio mbele yetu umeshapita hatua zote tatu na umekamilika. Napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wote waliohusika kwa upande wa Serikali Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Maafisa wote, lakini vilevile na Kamati zetu, Wajumbe wote wa Kamati inayohusika mliopitia Muswada huu na kuuangalia kwa niaba yetu lakini pia Bunge zima.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwakumbushe kwamba wale ambao mngenda kuwa mnashiriki katika hatua ile ya Kamati ya Bunge Zima, kufanya vile ambavyo Mheshimiwa John J. Mnyika amekuwa akifanya, kama una jambo ambalo unahitaji marekebisho basi unahakikisha unafanya jambo hilo kwa wakati, una-move amendments zako, unazifikisha Ofisi ya Bunge na tunayo Idara nzima ya Bunge ya Sheria ambayo inasaidia katika kufafanua na namna ya kuweka sawasawa hoja zako ambazo ungependa zifanyiwe kazi katika hatua ile, vinginevyo ukija hapa na kunyanyuka bila kuwa umeshaleta jambo lile mapema basi labda ni jambo la ushauri tu lakini kama ni jambo la msingi inakuwa ni vigumu sana katika hatua ile kuweza kulichukua jambo hilo.

Kwa jinsi hiyo, Muswada wetu huu sasa utaendelea na safari yake kwenda mbele ya Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kupata idhini yake na baada ya hapo basi niwatakie kila la kheri Wizara ya Viwanda na Biashara katika utekelezaji wa Muswada huu.

Kabla hatujasogea mbele, Mheshimiwa *Chief Whip* kwa upande wa Upinzani ulisimama, karibu!

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. TUNDU A. M. LISSU – CHIEF WHIP UPINZANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo chini ya Kanuni ya 68(7), kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo naloliombea mwongozo kutoka kwako linahusu tendo hili ambalo limekamilika la kupitisha Muswada wa *Economic Zones (Miscellaneous Amendments Act)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria hii ambayo imepitishwa sasa hivi uliletwa mapema leo kwa ajili ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na kujadiliwa na Bunge na tukio hilo lilifanyika na muda mfupi uliopita Muswada huu umesomwa kwa Mara ya Tatu na kupitishwa. Sasa naomba mwongozo wako kama Kanuni za Kudumu za Bunge zinaruhusu Muswada wa Sheria kushughulikiwa kwa hatua zaidi ya moja kwa mujibu wa Kanuni zetu na naomba nirejee masharti ya Kanuni ya 93 (1).

*“Bunge halitashughulikia hatua zaidi ya moja kwa Muswada wowote wa Sheria katika mkutano mmoja wa Bunge”*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia fasili ya (2) na (3) zinatoa *exceptions to that general rule* na *exceptions* ni kwamba hatua zaidi ya moja inawezekana tu iwapo chini ya fasili ya (2) kuna hoja mahsusi imetolewa kwamba Muswada huo ushughulikiwe kwa hatua zaidi ya moja. Lakini *exception* ya pili iko kwenye fasili ya (3) ya Kanuni ya 93 inayohusu Muswada kuletwa Bungeni kwa hati ya dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Muswada ambao umepitishwa, haukuletwa kwa hati ya dharura, hakukuwa na hoja mahsusi yoyote ya kutaka usomwe mara ya pili na mara ya tatu kwenye mkutano huu mmoja wa Bunge. Kwa hiyo, naomba mwongozo wako kama utaratibu uliotumika kuupitisha Muswada huu unakubalika kwa mujibu wa Kanuni za Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Tundu Lissu kwa uliyoyasema, lakini tatizo unasoma vifungu nusunusu, ni kweli ulichosema kuhusu 93(1) kwamba Bunge halitashughulikia hatua zaidi ya moja kwa Muswada wowote wa Sheria katika mkutano mmoja wa Bunge, ni kweli! (*Makofi*)

Lakini bila kuathiri masharti hayo Bunge linaweza kushughulikia Muswada wa Sheria katika hatua zaidi ya moja endapo, umeisoma (a) ya hoja mahsusi lakini umeacha (b) kwamba endapo Spika ataridhika na hiyo. (*Makofi*)

Naomba nikuhakikishie kwamba Spika ameridhika na mimi Naibu Spika nimeridhika na ndiyo maana jambo hili liko kwenye *Order Paper* yetu ya leo kwamba ni katika shughuli ambazo tunapaswa tuzishughulikie leo. Si hili tu, tunaendelea na linalofuata litakwenda kwa utaratibu huohuo. (*Makofi*)

## **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

### ***Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2011 [The Written Laws Amendments Bill 2011].***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na hatimaye kupitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2011 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2011*) pamoja na Jedwali la Marekebisho lililotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuelezea vifungu vya Sheria vinavyohusika na mapendekezo haya, ninapenda kwanza kuwapa rambirambi Watanzania wenzetu waliopatwa na maafa tangu kikao kilichopita hasa wakazi wa Gongo la Mboto na viunga vyake, familia ya Wasanii wa Muziki wa Taarab wa kikundi cha *Five Stars Modern Taarab* waliopata ajali tarehe 21 Machi, 2011. Mwenyezi Mungu awarehemu wote waliopoteza maisha yao na kuwapa matumaini ndugu na marafiki wa Marehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru pia Waandishi wa Sheria na watumishi wengine wa ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali walioandaa Muswada huu. Nachukua nafasi ya pekee kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala na Wajumbe wote wa Kamati hiyo, kwa ushauri na mapendekezo yaliyoboresha mantiki ya Muswada huu kama unavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho lililotolewa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa mwaka 2011 pamoja na Jedwali la Marekebisho unapendekeza marekebisho katika Sheria mbalimbali zipatazo 11. Marekebisho hayo yanayopendekezwa yanalenga kuondoa ama upungufu ambao umedhihirika wakati wa utekelezaji wa masharti yaliyomo

katika Sheria hizo au migongano ya baadhi ya Vifungu katika Sheria hizo. Sheria hizo ni kama ifuatavyo:-

Sheria ya Ushahidi (*The Evidence Act*), Sura ya 6, Sheria ya Kanuni za Adhabu (*The Penal Code*), Sura ya 16, Sheria ya Uchawi (*The Witchcraft Act*), Sura ya 18, Sheria ya Mwenendo ya Makosa ya Jinai (*The Criminal Procedure Act*), Sura ya 20, Sheria ya Chuo cha Teknolojia cha Dar es Salaam (*The Dar es Salaam Institute of Technology Act*), Sura ya 144, Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi (*The Economic and Organize Crime Control Act*), Sura ya 200, Sheria ya Usajili wa Makandarasi (*The Contractors Registration Act*), Sura ya 235, Sheria ya Wakala wa Serikali (*The Executive Agencies Act*), Sura ya 245, Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka ya Miji (*The Local Government Urban Authorities Act*), Sura ya 288, Sheria ya Kubadilishana Wakosaji Watoro (*The Extradition Act*), Sura ya 368 na Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori (*The Wildlife Conservation Act*) Na.5 ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sheria ya Ushahidi, Kifungu cha 4 cha Muswada, kinapendekeza kwamba tafsiri ya maneno *Police Officer* ambayo ilikuwa awe ni Polisi ambaye ana cheo cha Koplo na kuendelea ifutwe na iandikwe upya ili maneno hayo yatafsiriwe kuwa ni Polisi mwenye cheo cha *Constable* au zaidi ya hicho kama inavyotafsiriwa kwenye Sheria ya Polisi na Polisi Wasaidizi, Sura ya 322.

Mheshimiwa Naibu Spika, mantiki ya mabadiliko haya ni kuruhusu Polisi ambao wana vyeo vya *Constable* kuruhusiwa kuchukua maelezo ya washtakiwa katika maeneo au vituo vya Polisi ambapo Polisi mwenye cheo cha Koplo au zaidi ya hapo hayupo. Marekebisho hayo yatafunguza muda wa kuchukuliwa kwa maelezo ya watuhummiwa katika vituo ambavyo Polisi wenye vyeo vya Ukoplo hawapo. Aidha, inapendekezwa kuboresha tafsiri ya maneno *Oral Evidence* ambao ni ushahidi unaotolewa kwa mdomo na mtu aliye Mahakamani yanayotumika katika Kifungu cha 3 ili kuongeza wigo wa aina ya ushahidi ili kuruhusu kuchukuliwa kwa ushahidi wa shahidi asiyekuwepo Mahakamani unaowezeshwa na ujio wa Teknologia duniani na hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sheria ya Kanuni za Adhabu inapendekezwa katika Kifungu cha 6 kufanya marekebisho katika Kifungu cha 132 ili kuweka adhabu mahsusi kwa mtu mwenye umri wa miaka chini ya 18 anayetiwa hatiani kwa kosa la kujaribu kubaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajili ya elimu ya umma, Sheria ilivyo sasa ni kwamba mtu ambaye hajafikisha miaka 10 hawezi kuwajibika kwa jinai isipokuwa kama itathibitishwa kwamba wakati anafanya tendo hilo la jinai alikuwa na uwezo wa kufahamu kwamba hakupaswa kutenda kosa hilo. Ama mwanaume mtoto aliye na miaka chini ya 12 hadhaniwi kwamba ana uwezo wa kujamiiana, ndiyo! Baada ya hapo mtu yeyote akifanya kosa la kujaribu kubaka adhabu yake ni kifungo cha jela cha maisha au miaka isiyopungua 30. Kwa upande mwingine, mtoto mwenye umri kama huo anayepatikana na hatia ya kubaka adhabu yake imeainishwa katika Kifungu cha 131 kilichofanyiwa marekebisho kwa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali, Na.19 ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho haya ni kuwaondoa watoto wenye miaka kati ya 12 na pungufu ya 18 kutopata adhabu ya sasa ila adhabu tunayopendekeza katika Kifungu cha 6 cha Muswada katika ukurasa wa pili. Shabaha ya marekebisho haya ni kulinda haki pamoja na ustawi wa mtoto anayetiwa hatiani kwa makosa ya jinai ili kutoa nafasi kubwa kwake ya kusahihishwa na kujisahihisha kwa adhabu zinazopendekezwa. Aidha, katika Kifungu cha 7 cha Muswada, marekebisho yanayopendekezwa ni kukiandika upya kichwa cha sehemu hiyo ya 17 ya Muswada wa Sheria. Marekebisho haya yanalenga kuongeza makosa haramu au piramidi (*Pyramid Schemes*) kuwa miongoni mwa makosa yaliyo katika sehemu hiyo kwani yameorodheshwa katika sehemu hiyo lakini kichwa cha sehemu hiyo hakionyeshi kama makosa hayo yako chini yake.

Vilevile, marekebisho kwenye Kifungu cha 8 na 9 cha Muswada yanalenga kukiandika upya Kifungu cha 171A ili kujumuisha makosa haramu au *Pyramid Schemes* katika Sheria hiyo na kukifuta Kifungu cha 173B. Jedwali la Muswada linaonesha mabadiliko haya, Sehemu ya A, imeandikwa upya kwenye Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya marekebisho katika Sheria ya Uchawi (*The Witchcraft Act*), Sura ya 18 yanafanyika kwenye Kifungu cha 8(7) ili kuongeza adhabu kwa mtu anayepinga au kukaidi amri halali ya Mkuu wa Wilaya inayotolewa baada ya kufanya uchunguzi wa kina chini ya Kifungu cha 8 cha Sheria hiyo, kuwa ya fedha kwa kiwango kisichopungua shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miaka miwili badala ya ile ya shilingi 150 au kifungo kisichozidi miezi miwili jela kwa Sheria iliyopo sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine adhabu hii pia inaweza kuihusu ile Kamati ya Ufundi ya Timu ya Mpira ambayo ilitangazwa jana hapa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria nyingine inayoguswa na mapendekezo haya ni Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (*The Criminal Procedure Act*), Sura ya 20. Kwenye Jedwali lenye Marekebisho, Kifungu cha 15 kimefutwa.

Katika Ibara ya 16 ya Muswada tunapendekeza kuruhusiwa kwa wapelelezi wa makosa ya jinai kuandika maelezo ya mtuhumiwa kwa mtiririko kwa kufuata masharti yaliyopo kwenye kifungu cha 58 ili kulinda na kuhifadhi haki za Kikatiba za mtuhumiwa. Kifungu hicho kwa sasa kinaeleza kuwa mshitakiwa ndiye anayepaswa kuandika maelezo hayo. Lengo la mapendekezo ya Muswada ni kuonesha kuwa maelezo hayo yanaweza kuandikwa na askari wapelelezi au mtuhumiwa mwenyewe kwa kufuata masharti yaliyomo kwenye kifungu hicho cha 58. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Ibara ya 17 ya Muswada ina mapendekezo ya kukifuta kifungu cha 129A kwa kuwa mambo yanayohusiana na kifungu hicho yameelezwa pia katika kifungu cha 128 (6). Aidha, kifungu cha 192 kinarekebishwa ili kuipa Mahakama Kuu uwezo wa kusikiliza mashauri ya awali (*preliminary hearing*). Mashauri hayo ya jinai ili kufahamu masuala yasiyobishaniwa katika shauri la jinai na

kupunguza muda wa kusikiliza shauri kuu endapo mshitakiwa amekana shitaka. Utaratibu unaopendekezwa unafanana na utaratibu ulivyo kwenye Mahakama za Mahakimu wa Wilaya na Mahakimu Wakazi, ama kifungu hicho kitarekebishwa ili kutaka Wakili anayemtetea mshitakiwa kuwepo mahakamani wakati wa kusikiliza shauri la awali sawa na mshitakiwa, tofauti na sheria ya sasa ambapo Wakili wa Mshitakiwa halazimiki kuwepo mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 19 ya Muswada imeandikwa upya, kifungu cha 226 kinarekebishwa ili kuliwezesha shitaka lililofutwa na Mahakama kutokana na mlalamikaji kutofika mahakamani, kurejeshwa tena mahakamani. Sheria hivi sasa haitoi nafasi hiyo kwa mlalamikaji hata kama ana sababu za msingi zilizosababisha yeye kushindwa kufika mahakamani. Marekebisho haya yatamuwezesha mwendesha mashitaka kuomba Mahakama kurejesha mashitaka na mwenendo wa mashitaka na atalazimika kuelezea na kuonesha ni kwa nini hakufika mahakamani siku shauri lilipopangwa. Kama Mahakama itaridhika na sababu hizo shauri dhidi ya mshitakiwa litarejeshwa mahakamani na litaendelea kusikilizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho mengine yanayopendekezwa yanahusu Kifungu cha 345 katika Ibara ya 22 ya Muswada, ili kuondoa kutaja kiwango cha gharama ambacho Mahakama inaweza kuamuru mshitakiwa kuwalipa waendesha mashitaka wa umma au waendesha mashitaka binafsi na badala yake Mahakama yenyewe iamue kiwango hicho. Lengo ni kufanya gharama husika itolewe na Mahakama kulingana na mazingira ya kesi na baada ya kuona mchango wa mwendesha mashitaka husika. Kifungu hicho kina marekebisho pia kwenye jedwali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yanayohusu kifungu cha 353 cha sheria hii yanalenga kuipa Mahakama mamlaka ya kusimamia na kuhifadhi vielelezo vilivyotolewa mahakamani kama ushahidi na siyo vielelezo vilivyotarajiwa kutumika kama ushahidi.

Katika kifungu cha 383 inapendekezwa kwamba vifungu vidogo vya (1), (2) na (3) vifutwe na kuandikwa upya ili kuweka utaratibu wa Mahakama kushughulikia kutofika mahakamani kwa Warufani au Mwakili wao kwa siku ambapo rufaa imepangwa kusikilizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 392A kinaongezwa kama inavyooneshwa katika Ibara ya 25 ya Muswada kupendekeza utaratibu wa kufikisha maombi ya jinai mahakamani kwa kuwa sheria ya sasa haielezi utaratibu unaotakiwa kufuatwa na waombaji. Marekebisho yamefanywa kwenye jedwali.

Kutokana na kuanzishwa makosa mapya kwenye Sheria ya Kanuni za Adhabu, jedwali la kwanza la Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai linafanyiwa marekebisho ili kuongeza makosa mapya ili kuonesha makosa ambayo mtuhumiwa anaweza kukamatwa bila ya hati, adhabu kwa kosa husika na aina ya Mahakama itakayosikiliza kesi kama inavyooneshwa kwenye Ibara ya 26 ya Muswada.



Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho katika Sheria ya Chuo cha Teknolojia cha Dar es Salaam (*The Dar es Salaam Institute of Technology Act*), Sura ya 144 yanafanyika kwenye vifungu vya 11 na 12 ili kuanzisha nafasi za Naibu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia taaluma na Naibu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia Utawala na Fedha na pia kuwafanya Wakurugenzi hao kuwa Manaibu wa Mkuu wa Chuo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi (*The Economic and Organised Crime Control Act*), Sura ya 200 Ibara ya 31 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 29(1) ili Mahakama za Hakimu Mkazi ziwe na mamlaka ya kupokea na kusikiliza kesi za uhujumu uchumi. Ibara ya 32 kwenye Muswada imefutwa, makosa yaliyomo kwenye Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya mwaka 2007 yatabakia kwenye Sheria hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya marekebisho yanafanywa pia kwenye Sheria ya Usajili wa Makandarasi. Inapendekezwa kwamba kifungu cha 10 kirekebishwe kwa kuongeza kifungu kidogo kipya ili kuweka sharti kwamba kampuni ya kandarasi inayomilikiwa na mtu mmoja isajiliwe katika daraja la sita na saba tu kwa kandarasi za kawaida au katika daraja la pili na tatu kwa kandarasi maalum. Aidha, kifungu cha 13 kinaandikwa upya kwa kufuta aya ya (c) ya kifungu cha kwanza ili kuweka uhibitaji wa usajili wa makandarasi, kulipa ada ya usajili kwa wakati na kuzuia makandarasi wote wasiolipa ada ya mwaka ifikapo tarehe 30 Desemba ya kila mwaka kusitisha shughuli za ukandarasi. Aidha, Bodi ya Makandarasi inapewa mamlaka ya kuwasimamisha au kuwafuta kutoka katika orodha ya makandarasi, wale wasiolipa ada hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yanafanyika marekebisho pia katika Sheria ya Wakala wa Serikali, Sheria ya Wakala wa Serikali (*The Executive Agencies Act*), Sura ya 245 na marekebisho hayo yanafanyika katika kifungu cha sita kuruhusu Afisa Mkuu “A principal officer” kutoka Wizara inayoanzisha Wakala kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Bodi ya Wakala hiyo.

Vilevile kifungu cha 6A kinarekebishwa ili kuzuia Mtendaji Mkuu wa Wizara husika kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Bodi ya Wakala. Marekebisho tunayowasilisha yatawezesha Wizara zetu kudhibiti uwajibikaji wa Wakala.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Miji) (*The Local Government (Urban Authorities Act)*), Sura ya 288 Muswada unapendekeza kuongezwa kwa kifungu kidogo cha 5 kipya kwenye kifungu cha 94 ili kuipa mamlaka maeneo ya uzalishaji wa bidhaa za mauzo ya nje (*The Export Processing Zones Authority*) uwezo wa kutoa kibali cha ujenzi kwa wawekezaji katika maeneo ya uzalishaji wa bidhaa za mauzo ya nje ambayo mamlaka hiyo inayamiliki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 11 ya Muswada yenye vifungu vya 41 na 42 imeondolewa kwenye marekebisho haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho kwenye Sheria ya Kubadilishana Wakosaji Watoro (*The Extradition Act*), Sura ya 368, inayoweka utaratibu wa

kumrejisha mtu aliyefanya makosa nje ya nchi au anayetakiwa kujibu tuhuma nje ya nchi katika Muswada huu tunapendekeza kuongezwa kwa kifungu kipya cha 13A ili kuruhusu Afisa wa Polisi kumkamata Mkosaji Mtoro aliyefanya kosa nje ya nchi bila kulazimika kuwa na hati ya kumkata iliyoidhinishwa na mamlaka ya nchi alipotenda kosa au hati ya muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye jedwali la marekebisho inapendekezwa kurekebisha Sheria ya Hifadhi ya Wanyapori *(The Wildlife Convention Act)* Sura ya 283 kwa kufuta aya za (a) na (b) za kifungu cha 38(3) na kuziandika upya kama inavyoonesha kwenye jedwali la marekebisho. Aidha, inapendekezwa kuongeza aya mpya ya (c) kwa lengo la kuwezesha kupata mtaalamu atakayewakilisha vyuo vilivyokusudiwa kupatikana kutokana na sifa za utaalamu badala ya cheo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya napenda kupitia kwako kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kuujadili Muswada huu na kuupitisha katika hatua mbili, Kusomwa Mara ya Pili na Kusomwa Mara ya Tatu. Nina imani kwamba Bunge lako litaridhia marekebisho yote haya yanayopendekezwa na litakubali marekebisho haya yawe sehemu ya Sheria za nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mawasilisho yako na hoja yako imeungwa mkono. Sasa naomba nimuite Mwenyekiti wa Kamati iliyochambua mapendekezo yaliyoletwa mbele yetu, Kamati ya Katiba na Sheria. Anakuja Mwenyekiti mwenyewe, Mheshimiwa Pindi Chana. *(Makofi)*

**MHE. PINDI H. CHANA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kushukuru kupata nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2011 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments Bill ya 2011)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa leo ni siku ya kwanza kuwasilisha maoni ya Kamati yangu, naomba kwanza kabisa kuwapongeza Wajumbe wote waliochaguliwa kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Lakini vilevile nichukue nafasi hii kuwashukuru sana kwa kunipa kibali cha kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, mimi na Makamu wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na Watanzania wote kutoa pole kwa wenzetu wahanga wa janga la Gongo la Mboto na waliopata ajali ambayo tumepata taarifa sasa hivi kwenye lori lililokuwa limebeba mafuta ambalo limegongana na treni katika maeneo ya Manyoni. Kwa wale waliopata matatizo tunasema pole na kwa wale waliofariki dunia Mungu aziweke mahali pema roho za marehemu, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nielezee hatua iliyotangulia wakati wa kuujadili Muswada huu. Katika kukidhi masharti ya Kanuni ya 84(2) na 114(9), Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, tarehe 28 Machi, 2011 katika utaratibu wa Bunge wa kuwashirikisha wananchi katika mchakato wa kutunga sheria, Kamati yangu iliwaalika wadau kadhaa waliofika mbele ya Kamati kutoa maoni yao. Wadau hao walitoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (*OUT*), Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (*LHRC*), Kituo cha Msaada wa Sheria cha Wanawake (*WLAC*), Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (*TAWLA*) na *Tanganyika Law Society*, (*TLS*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) na kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, sasa naomba kuwasilisha maoni ya Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kueleza kwamba Muswada huu ni mzuri na umekuja kwa wakati muafaka. Kamati inaamini kuwa marekebisho yaliyokusudiwa yakipitishwa kuwa Sheria na kufanyiwa kazi ipasavyo yatasaidia sana kuboresha maeneo mbalimbali yaliyokuwa na upungufu kama yalivyoinishwa katika Muswada. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu uliwasilishwa katika kikao cha Kamati kilichofanyika tarehe 28 Machi, 2011 katika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam na Mheshimiwa Jaji Frederick Werema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye alielezea azma na madhumuni ya Serikali ya kuzifanyia marekebisho Sheria zifuatazo ambazo Kamati ilijielekeza katika kuzifanyia uchambuzi. Sheria hizo ni Sheria ya Ushahidi (*The Evidence Act*) Sura ya 6, Sheria ya Kanuni za Adhabu (*The Penal Code*) Sura ya 16, Sheria ya Uchawi (*The Witchcraft Act*) Sura ya 18, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (*The Criminal Procedure Act*) Sura ya 20, Sheria ya Chuo cha Teknolojia cha Dar es Salaam, (*The Dar es Salaam Institute of Technology Act*) Sura ya 144 na Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi (*The Economic and Organised Crime Control Act*), Sura ya 200.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria nyingine ni Sheria ya Usajili wa Makandarasi (*The Contractors Registration Act*) Sura ya 235, Sheria ya Wakala wa Serikali (*The Executive Agencies Act*) Sura ya 245, Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Miji) (*The Local Government (Urban Authorities Act)*) Sura ya 288, Sheria ya Kubadilishana Wakosaji Watoro (*The Extradition Act*) Sura ya 368 na Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori (*The Wildlife Convention Act*) Act No. 50 ya mwaka 2009. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Kamati kupokea maelezo ya Serikali, kimsingi Kamati inakubaliana na mapendekezo yaliyowasilishwa. Pamoja na hayo yapo maeneo kadhaa ambayo Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri katika kuuboresha zaidi Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sheria ya Ushahidi, Kamati inakubaliana na mapendekezo yaliyotolewa na Serikali ya kufuta tafsiri ya neno "*Police Officer*" katika kifungu cha 3 cha Sheria hiyo na kutoa tafsiri mpya ili kuondoa mgongano kati ya Sheria

hii na Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi kama alivyowasilisha mtoa hoja. Kamati inaamini kuwa mapendekezo hayo yataongeza ufanisi wa utekelezaji kazi wa Jeshi la Polisi. Aidha, Kamati inapendekeza kuboresha zaidi ushahidi unaotolewa kwa njia ya mdomo (*oral evidence*) ili kuongeza wigo wa aina hii ya ushahidi na hivyo kuruhusu kuchukua ushahidi wa shahidi asiyekuwepo mahakamani kwa kutumia teknolojia ya mawasiliano hususan kwa kutumia televisheni au *video*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushahidi wa aina hii siyo tu utaipunguzia gharama Serikali kuita shahidi aliye nje ya nchi au aliye mbali, lakini vilevile utaiwezesha kuwapata mashahidi muhimu ambao katika mazingira mengine wasingeweza kupatikana, inawezekana ni wagonjwa na kadhalika. Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa ushahidi wa namna hiyo uchukuliwe kwa tahadhari kubwa kwani inawezekana pia katika maendeleo ya sayansi na teknolojia ushahidi wa aina hiyo unaweza kuvurugwa. Hii ni kwa kuzingatia kuwa Mahakama huwa katika nafasi nzuri zaidi ya kupokea na kutathmini ushahidi inapojiridhisha na hali ya muonekano wa shahidi anapokuwa mbele ya Mahakama na hivyo kuwa katika nafasi nzuri ya kupata ushahidi wa kuaminika au kutoaminika kutokana na hulka ya shahidi inavyojitokeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Kanuni ya Adhabu imependekeza kufanya Marekebisho katika Kifungu cha 132 ili kuweka adhabu mahsusi kwa mtu mwenye umri wa chini ya miaka 18 anayetiwa hatiani kwa kosa la kujaribu kubaka (*attempt rape*).

Kamati ilitafakari kwa kina pendekezo hili kwa kuzingatia mabadiliko mbalimbali ya kijamii na hasa yanayohusu haki za mtoto. Kimsingi, Kamati inakubaliana na pendekezo hili ili kuwaondoa watu wenye umri chini ya miaka 18 yaani watoto kutopata adhabu ya sasa ya kifungu cha maisha au miaka isiyopungua 30 kwenye kosa la kujaribu kubaka ili kulinda haki za mtoto anayeshitakiwa kwa makosa haya ya jinai. Aidha, Kamati inampongeza mtoa hoja kwa kukubali ushauri wa Kamati wa kubadilisha neno *recidivis*” au mhalifu sugu na kuweka neno *habitual* au mhalifu aliyekubuhu kama ilivyoonyeshwa katika kifungu cha 6 aya ya C. (*Makofi*)

Vilevile Kamati inakubaliana na marekebisho katika Ibara ya 7 ya Muswada ili kukiandika upya kichwa cha habari cha Sehemu ya 17 ya Sheria na hivyo kuongeza makosa haramu ya piramidi (*Pyramid Schemes*) kuwa miongoni mwa makosa yaliyo katika sehemu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ibara ya 10 ya Muswada, Serikali imewasilisha pendekezo la kurekebisha kifungu cha 287A cha Sheria Na. 5 ya mwaka 2004 kiandikwe upya ili kutofautisha kosa la unyang’anyi wa kutumia silaha na kosa la unyang’anyi wa kutumia nguvu unaohusisha zaidi ya mtu mmoja. Kutokana na kuongezeka kwa vitendo vya uhalifu wa aina hiyo, Kamati inakubaliana na mapendekezo haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sheria ya Uchawi (*The Witchcraft Act*), Sura 18, Serikali imewasilisha mapendekezo ya kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 8(7) ili kuongeza adhabu kwa mtu anayepinga au kukaidi amri halali ya Mkuu wa Wilaya inayotolewa chini ya kifungu cha 8 cha Sheria hiyo kuongeza kiwango cha fedha au

kwenda jela kwa muda usiopungua miaka miwili badala ya adhabu ya zamani ya shilingi mia moja na hamsini au kifungo kisichozidi miezi miwili jela kama ilivyo sasa. (*Makofi*)

Kutokana na mabadiliko ya wakati, Kamati inakubaliana na mapendekezo hayo. Aidha, Kamati inashauri kuwa kwa kuwa suala la uchawi ni la kiimani zaidi, Serikali iweke utaratibu mzuri wa kulinda haki za watuhumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya mtoa hoja kama ilivyoielezwa kwenye Ibara ya 16 ya Muswada huu ili kuboresha utaratibu wa uendeshaji na mwenendo wa makosa ya jinai na kuweka masharti mapya ya taratibu za kufuatwa na mpelelezi wakati wa kuandika maelezo ya mtuhumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, inapendekezwa pia vifungu vya 222, 226 na 235 vifanyiwe marekebisho ili kuipa Mahakama mamlaka ya kuondoa shtaka na kumwachia huru mshtakiwa baada ya kufuta kesi ili kutoa nafasi ya kulirudisha shtaka Mahakamani kama kutakuwa na sababu za kufanya hivyo baadaye. Kamati inakubaliana na mapendekezo hayo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho mengine yanayopendekezwa yanahusu Kifungu cha 345 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (*Criminal Procedure Act*) ili kuondoa kutaja kiwango cha gharama ambacho Mahakama inaweza kuamuru mshitakiwa kuwalipa waendesha mashtaka ya umma au binafsi. Kamati inakubaliana na mapendekezo hayo ili gharama ziadane na wakati wa hivi sasa na kuipa Mahakama nafasi ya kuona kiwango kinachokidhi.

Aidha, katika kifungu cha 383 vifungu vidogo vya (1), (2) na (3) vinavyopendekezwa vifutwe na kuandikwa upya ili kuweka utaratibu mpya wa Mahakama kushughulikia kutofika Mahakamani kwa warufani au mawakili wao siku ambapo rufaa imepangwa kusikilizwa, Kamati inaafiki mapendekezo ya Serikali. (*Makofi*)

Vilevile Kamati inakubaliana na mapendekezo ya kuanzisha makosa mapya na kulifanyia marekebisho Jedwali la Kwanza ili kuongeza makosa mapya ya jinai katika Sheria na aina ya Mahakama inayoyasikiliza kama inavyooneshwa kwenye Ibara ya 26 ya Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ibara ya 27, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Chuo cha Teknolojia cha Dar es Salaam yanayofanyika kwenye vifungu vya 11 na 12 ili kuanzisha nafasi ya Naibu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia masuala ya taaluma, Naibu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia masuala ya utawala na fedha na pia kuwawezesha Wakurugenzi hao kuwa Manaibu wa Mkuu wa Chuo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sheria ya Uhujumu wa Uchumi, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya makosa ya aina hiyo yaliyoainishwa katika Ibara ya 31 ya Muswada ambapo katika Kifungu cha 29(1) Mahakama za Hakimu Mkazi zinapewa

mamlaka ya kupokea na kusikiliza kesi za uhujumu uchumi. Aidha, makosa ya rushwa sasa yanafanywa kuwa miongoni mwa makosa ya uhujumu uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sheria ya Usajili wa Makandarasi sura ya 235 Kamati inakubaliana na mapendekezo yaliyotolewa. Kamati inaamini kuwa mapendekezo hayo yataongeza ufanisi wa Makandarasi na kuiongezea uwezo zaidi Bodi ya Makandarasi katika kutekeleza majukumu ya sekta hiyo. Aidha, Kamati inakubaliana na kuweka sharti kwamba Kampuni inayomilikiwa na mtu pekee isajiliwe katika daraja la sita na la saba tu kwa kandarasi za kawaida au katika daraja la pili na la tatu kwa kandarasi maalum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya IX ya Muswada katika Ibara ya 38(a) katika Sheria ya Wakala wa Serikali (*The Executive Agency Act*) Sura ya 245, Kamati inampongeza mtoa hoja kwa kukubali ushauri wa Kamati wa kubadilisha maneno yaliyopo kwenye Ibara ya 38 ya Muswada kutoka “*An officer of a position of Assistant Director or above*” na kuwa “*A principal officer*” kama inavyooneshwa kwenye kifungu kidogo cha 3 cha Ibara hiyo.

Vilevile Kamati inakubaliana na pendekezo lililotolewa la kufanya marekebisho katika Kifungu cha 6(a) ili kuzuia Mtendaji Mkuu wa Wizara husika kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Bodi ya Wakala wa Serikali kwa lengo la kuiwezesha Wizara kudhibiti uwajibikaji wa Wakala.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya X ya Muswada katika Ibara ya 40 katika Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Kamati inakubaliana na mapendekezo ya kuongezwa kwa kifungu kidogo cha 5 kwenye kifungu cha 94 ili kuzipa Mamlaka za Miji uwezo wa kutoa kibali cha ujenzi kwa ajili ya wawekezaji watakaokuwa wanawekeza katika maeneo ya uzalishaji wa bidhaa zitakazouzwa ndani ya nchi. Aidha, Kamati inampongeza mtoa hoja katika Ibara ya 39 kwa kubadilisha maneno “*National Security Council Act*” kama inavyooneshwa kwenye Ibara ya 39 ya Muswada na kuweka maneno “*Local Government (Urban Authority)*.” (*Makofi*)

Sehemu ya XI ya Muswada katika Ibara ya 44 inahusu Sheria ya kubadilishana wakosaji watoro (*The Extradition Act*) Sura ya 368 ya Sheria, ambapo imependekezwa kuongezwa kwa kifungu cha 13A ili kuruhusu Afisa Polisi kumkamata mkosaji mtoro aliyefanya kosa na kukimbilia nje ya nchi bila kulazimika kuwa na hati ya kumkamata iliyoidhinishwa na mamlaka ya nchi alipotendea kosa. Kamati inakubaliana na mapendekezo haya ambayo yataweka utaratibu mzuri wa kumrejsha kwenye nchi alikotenda kosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Jedwali la Marekebisho, inapendekezwa kurekebisha Sheria ya Hifadhi Wanyamapori (*The Wildlife Conservation Act*, sura ya 283) kwa kufuta aya za (a) na (b) za kifungu cha 38(3) na kuziandika upya. Kamati inakubaliana na mapendekezo haya ikiwa ni pamoja na marekebisho ya kuongeza aya mpya ya (c) ili kuwezesha kupata mtaalam atakayewakilisha Vyuo kutokana na sifa ya utaalam badala ya cheo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo maoni na mapendekezo ya Kamati yangu wakati ilipouchambua Muswada huu. Naamini kuwa yale ambayo sikuyazungumzia Wajumbe wa Kamati yangu watayazungumzia watakapopata fursa ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nihitimishe kwa kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Frederick Werema na wataalamu wake kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati wakati Kamati ilipokuwa ikiujadili na kuchambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2011. Vilevile, Kamati inawapongeza wadau wote walioitikia wito wa kushiriki katika vikao vya mashauriano na kutoa maoni yao juu ya Muswada huu. Kamati inathamini sana maoni yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kutoa maoni yao katika kuboresha Muswada huu. Ujuzi na uzoefu wao wa muda mrefu katika sheria, utawala na nyanja mbalimbali za kijamii umeiwezesha Kamati kuuboresha Muswada huu kufikia hatua inayoonekana katika Jedwali la Marekebisho lililowasilishwa humu Bungeni tofauti na Muswada huu ulivyowasilishwa kwenye kikao cha Kamati katika hatua zake za awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwatambue kama ifuatavyo, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mwenyekiti, Mheshimiwa Angellah Kairuki, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mheshimiwa Zahra Ali Hamadi, Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Azza Hamad, Mheshimiwa Mustapha Akunaay, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy, Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina na Mheshimiwa Jason Rweikiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kutoa shukrani kwa Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kasililah pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, napenda kuwashukuru Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Peter Magati na Ndugu Grace Bidya pamoja na msaidizi wa Kamati Ndugu Catherine Kitutu kwa kuratibu vikao vya Kamati na kuyakamilisha maoni haya kwa wakati muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali na kuridhia hoja hii ya Serikali kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono Muswada huu na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kutupatia maoni ya Kamati yako. Sasa ni zamu ya Kambi ya Upinzani. Anakuja Mheshimiwa Tundu Lissu. *(Makofi)*

**MHE. TUNDU A. LISSU – MSEMaji WA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii mbele ya Bunge lako Tukufu kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Muswada wa kufanyia Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2011 (*Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2011*), kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 53(6) (c) Toleo la mwaka 2007. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Kanuni za Bunge lako Tukufu zingekuwa zinaruhusu kutoa ripoti inayopingana na ripoti ya Kamati basi pengine ripoti yangu au maoni yangu leo yangekuwa ni *dissentient*. Lakini nimeangalia Kanuni za Kudumu ya Bunge lako Tukufu sijaona mahali ambapo zinarusu Mjumbe wa Kamati kutoa a *dissenting report*. Kwa hiyo, *my dissentient will not be forthcoming*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jedwali la marekebisho lililowasilishwa leo na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tarehe 28 Machi, 2011 Kamati yako ilipokutana kujadili Muswada huu Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali alileta jedwali la marekebisho lililopendekeza kuongeza sheria nyingine ambazo hazikuwepo katika Muswada uliochapishwa katika gazeti la Serikali na baadhi ya sheria alizopendekeza Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuziongeza katika Muswada ilikuwa ni Sheria ya Ardhi, Sheria ya Mahakama ya Migogoro ya Ardhi pamoja na Sheria ya Uhifadhi ya Wanyamapori. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kikao hicho Wajumbe wa Kamati walihoji uhalali wa kuleta jedwali la mabadiliko katika hatua ya Muswada baada ya kusomwa kwa mara ya kwanza kabla haujadiliwa na Kamati na kabla haujapelekwa mbele ya Bunge kwa ajili ya kusomwa mara ya pili. Hoja hiyo ilitokana na masharti ya Kifungu cha 86(7) cha Kanuni za Kudumu zinazohitaji mjadala wakati wa Muswada kusomwa mara ya pili kuhusu ubora na misingi ya Muswada tu. Kanuni zetu zinakataza jedwali la marekebisho kuingiza sheria ambazo hazikuwepo katika Muswada uliochapishwa katika Gazeti la Serikali na Muswada wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori haikuwa moja ya Miswada iliyochapishwa katika gazeti la Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipohoji Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali baadae aliondoa mapendekezo ya kubadili Sheria ya Ardhi na Sheria ya Mahakama ya Migogoro ya Ardhi kwa sababu nilizozitaja. Lakini kwa bahati mbaya Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori haijaondolewa na inaletwa kinyume kabisa cha Kanuni za Kudumu za Bunge lako Tukufu na naomba mapendekezo ya kubadili hiyo sheria ambayo haikuwepo katika Muswada uliochapishwa katika Gazeti la Serikali yasiyadiliwe na Bunge hili Tukufu kwa sababu kufanya hivyo itakuwa kwenda kinyume na Kanuni za Kudumu za Bunge letu Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya kusema hayo, naomba basi nitoe maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu mapendekezo ya kubadili sheria ambazo zilitangazwa sawasawa katika Gazeti la Serikali. Nianze na mapendekezo ya kubadili Sheria ya Ushahidi.



Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada ya Sheria ya Mabadiliko ya Sheria (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2011*) umechapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 14 Januari, 2011 na kusomwa Mara ya Kwanza katika Mkutano wa Pili wa Bunge la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Muswada ulijadiliwa katika vikao viwili vya Kamati ya Sheria, Katiba na utawaka vilivyoketi Dar es Salaam tarehe 28 na 29 Machi, 2011.

Katika kikao cha Kamati cha tarehe 28 Machi Mheshimiwa Mwanasheria wa Mkuu wa Serikali aliwasilisha Jedwali la Marekebisho (*Schedule of Amendments*) ambalo lilipendekeza mabadiliko kadhaa katika Muswada wenyewe. Jedwali hilo lililetwa chini ya Kanuni ya 86(10)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mabadiliko hayo, mambo muhimu yalikuwa ni mapendekezo ya kufanya mabadiliko katika vifungu kadhaa vya Sheria ya Ardhi, Sura ya 113, Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216 na Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori, Sura ya 283 ya Sheria za Tanzania. Sheria zote tatu hazikuwepo katika Muswada na kwa hiyo mapendekezo hayo yalizua suala la uhalali wa Jedwali la Marekebisho lililowasilishwa na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kwamba mapendekezo yaliyokuwa katika Jedwali la Marekebisho tarehe 28 Machi, 2011 yamebadilishwa kwa mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria ya Ardhi na Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi kuondolewa. Hata hivyo, Jedwali la Marekebisho lililowasilishwa kwenye Kamati tarehe 11 Aprili 2011, limebakiza mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori, Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji uhalali wa kubakizwa kwa mapendekezo ya kubadili sheria hiyo ambayo hayapo kabisa katika Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu uliletwa kwenye Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala chini ya Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Kudumu mara baada ya kusomwa Mara ya Kwanza kwa mujibu wa Kanuni ya 83. Kwa mujibu wa Kanuni ya 84(3) ya Kanuni za Kudumu, “Kamati iliyopekewa Muswada itakuwa na uwezo wa kufanya marekebisho katika Muswada wa Sheria kwa kumshauri Waziri au Mbunge anayehusika na Muswada huo kufanya mabadiliko...”

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu unahusu Muswada yote ya Serikali lakini hauhusu Muswada Binafsi kwa mujibu wa Kanuni ya 84(3) ya Kanuni za Kudumu na kwa kufuatana na Kanuni ya 84(4), Muswada wa Sheria uliofanyiwa mabadiliko unatakiwa kurudishwa kwenye Kamati kwa madhumuni ya kuzingatia mabadiliko hayo kabla ya kupelekwa Bungeni kwa ajili ya Kusomwa Mara ya Pili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa Serikali kufanya mabadiliko katika Muswada wake wa Sheria umewekwa na Kanuni ya 86 ya Kanuni za Kudumu inayohusu Muswada Kusomwa Mara ya Pili. Chini ya Kanuni ya 86(10)(b) ya Kanuni za Kudumu, “... iwapo mtoa hoja anataka kufanya mabadiliko katika Muswada wa Sheria kutokana na

ushauri uliotolewa ama katika Kamati au wakati wa Muswada wa Sheria Kusomwa Mara ya Pili au kwa sababu nyingine yoyote, iwapo Muswada huo ni wa Serikali atamjulisha Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria ili atayarishe na kumkabidhi Katibu ambaye atagawa kwa kila Mbunge nakala ya ... Jedwali la Marekebisho au mabadiliko yanayokusudiwa kufanyika.”

Kwa vile Jedwali la Marekebisho lililoletwa tarehe 11 Aprili, 2011 limeingiza mambo ambayo hayakuwepo kabisa katika Muswada uliosomwa Mara ya Kwanza na kisha kupelekwa kwenye Kamati, itakuwa ni makosa kwa Bunge kujadili mabadiliko yanayohusu Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori. Hii ni kwa sababu, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(7) ya Kanuni za Kudumu, “mjadala wakati wa Muswada Kusomwa Mara ya Pili utahusu ubora na misingi ya Muswada huo tu.” (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inamshauri Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuzingatia Kanuni za Kudumu za Bunge zinazohusu uwasilishaji wa Jedwali la Marekebisho kwa Miswada ya Sheria ya Serikali kwa siku za baadaye. (*Makofi*)

Sasa naomba kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, kujadili mapendekezo ya mabadiliko ya sheria mbalimbali yaliyopo katika Muswada huu nikianzia na Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6 ya Sheria za Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mabadiliko katika Sheria ya Ushahidi, Muswada unapendekeza kufanya mabadiliko katika sehemu ya tafsiri iliyopo kwenye kifungu cha 3 cha Sheria ya Ushahidi kwa kubadili tafsiri ya maneno “Afisa wa Polisi” na “ushahidi wa maneno”. Inapendekezwa kwamba tafsiri ya maneno “Afisa wa Polisi” ibadilishwe kutoka tafsiri ya sasa ambayo ni “Mtumishi yeyote wa Jeshi la Polisi mwenye cheo cha koplo au zaidi” na kuwa “mtumishi yeyote wa Jeshi la Polisi mwenye cheo cha Konstebo au zaidi.” Lengo la mapendekezo haya linaelezwa katika “Madhumuni na Sababu” za Muswada huu kuwa ni “... kuondoa mkinzano uliokuwepo kati ya Sheria ya Ushahidi na Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi ..., Sura ya 322.”

Mheshimiwa Naibu Spika, hii tafsiri inayopendekezwa si tafsiri ndogo. Hii tafsiri inayopendekezwa katika kifungu cha 3 cha Sheria ya Ushahi si tafsiri ndogo. Kwa sababu gani? Sheria ya Jeshi la Polisi na Sheria ya Sheria ya Ushahidi sio zinazotafsiri hilo neno “Afisa wa Polisi.” Nitoe mfano wa Sheria yetu ya Mwenendo wa Jinai, neno Afisa wa Polisi maana yake ni “Mtumishi yeyote wa Jeshi la Polisi na mtumishi yeyote wa jeshi la mgambo wakati anapotekeleza wajibu wa polisi kwa mujibu wa sheria yoyote inayotumika kwa sasa.” Hii ina maana kwamba wanamgambo, sungusungu au wanausalama ambao wanatambuliwa na Sheria ya Jeshi la Mgambo, Sura ya 111 ya Sheria za Tanzania ni maafisa wa polisi kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Jinai na wana mamlaka yote ya Kipolisi Kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Muswada unapendekeza tafsiri itakayodhibiti hao ambao Sheria ya sasa inawaita Afisa wa Polisi maana yake kama pendekezo hili

litakubaliwa Afisa wa Polisi atakuwa ni polisi yeyote mwenye cheo cha kostebo kwenda juu. Mgambo, sungusungu wanausalama na vikundi vya aina hiyo ambavyo kwa Sheria za Tanzania za sasa wanaweza wakafanya kazi za polisi hawatakuwa na *police powers* kwa sababu hawatakuwa *police officers* kwa mujibu wa Sheria. Ninachotaka kusema ni kwamba mapendekezo haya yanaleta mgongano wa Sheria, yanaleta *conflict of laws* kati ya Sheria ya Ushahidi na Sheria ya Mwenendo wa Jinai ya sasa hivi. Kwa misingi au Kanuni za Kutafsiri Sheria panapotokea mkinzano wa aina hii katika tafsiri ya neno moja la kisheria basi namna ya ku-*resolve* hiyo *conflict of laws* ni kusema kwamba hiyo Sheria iliyopitishwa baadae ndiyo itakayosimama Sheria iliyokuwa ya mwanzo itaanguka maana yake ni kwamba tukikubali pendekezo hili hiyo Sheria ya Ushahidi hilo neno Afisa wa Polisi maana yake itakuwa ni polisi tu kama tunavyowajua, mgambo, sungusungu na wengine hawatakuwa na mamlaka za kipolisi. Kwa hiyo, si tafsiri ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye mapendekezo ya kubalidi neno ushahidi wa maneno. Muswada unapendekeza kubadili tafsiri ya maneno “Ushahidi wa Maneno” katika Sheria ya sasa ya Ushahidi ili kuruhusu ushahidi kutolewa na/au kupokelewa kwa njia ya teknolojia za kisasa za mawasiliano kama vile *video links*, *video conferences* na vitu kama hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko haya yanayopendekezwa kama yatakubaliwa maana yake ni kwamba hilo neno ushahidi wa maneno sasa utaweza kutolewa kwa njia za *video*. Sasa pamoja na nia njema na kwenda na wakati inayodhihirishwa na pendekezo hili Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba huu si muda muafaka wa kufanya mabadiliko yanayopendekezwa. Hii ni kwa sababu zifuatazo za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu wa Sheria za sasa kifungu cha 212 cha Sheria ya Mwenendo wa Jinai kinailazimisha Mahakama inaporekodi ushahidi, inapochukua ushahidi Mahakama inalazimika sio tu kuchukua maelezo ya shahidi anayetoa ushahidi wake Mahakamani bali pia Mahakama inatakiwa kurekodi tabia au mwenendo wa huyo shahidi anapotoa ushahidi wake Mahakamani na hii ni kwa sababu *body language* au lugha ya kimwili mara nyingi inaonesha mambo muhimu kiushahidi kuliko ambayo shahidi anayasema. (*Makofi*)

Sasa tukiruhusu ushahidi utolewe kwa njia ya *video*, *teleconference*, *skype* au kwa njia zingine za mawasiliano ya TEKNOHAMA uwezo wa Mahakama wa kurekodi *demeanour* ya shahidi Mahakama itarekodi namna gani?

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Naomba tumruhusu amalize. Muongozo wa Spika.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nafuatilia hotuba ambayo Mheshimiwa Tundu Lissu anasoma lakini napata taabu kwa sababu naona kama anahutubia, anasoma sehemu nyingi napotea anaanza kuhutubia. Sasa nilitaka chini ya Kanuni 68(7) utupe muongozo wakati tuna hotuba ambayo imeandikwa na mhutubiaji anahutubia tufuate kipi, anachozungumza pale au ambacho kimeandikwa kwenye hotuba yake? Maana ni vitu viwili ambavyo vinatupa taabu kufuatilia. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Asante. Mwongozo ni kwamba anapaswa kufuata kilichoandikwa. (*Makofi*)

**MHE. TUNDU A. LISSU - MSEMaji MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante. Kuna matatizo mengine yanayotokana na pendekezo hili la kubadili ushahidi wa maneno. Chini ya kifungu cha 199 cha Sheria ya Mwenendo wa Jinai ya sasa, mtu yeyote anayekataa kuapishwa ili atoe ushahidi au anayekataa kujibu maswali baada ya kuapishwa kutoa ushahidi anaweza kuwekwa rumande kwa amri ya Mahakama kwa muda wa siku nane hadi hapo atakapokubali kutoa ushahidi au kuapishwa kutoa ushahidi.

Sasa kama pendekezo la kutoa ushahidi kwa *video link* au kwa *skype* au kwa TEKNOHAMA zingine litakubaliwa ni namna gani Mahakama itamlazimisha shahidi aliyeko Ulaya au Amerika ya Kaskazini au aliyeko Arusha Mahakama iko Dar es Salaam kukubali kuapishwa ili kutoa ushahidi au kutoa ushahidi huo baada ya kuapa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo lingine kwamba Sheria ya sasa shahidi akishamaliza kutoa ushahidi wake mahakamani huwa anaamriwa kubaki ndani ya ukumbi wa mahakama ili asipate fursa ya kuwasiliana na kuwafundisha mashahidi wengine ambao bado hawajatoa ushahidi wao. Sasa kama ushahidi wa TEKNOHAMA utaruhusiwa mahakamani, haijulikani shahidi anayetoa ushahidi wa aina hiyo atadhibitiwaje ili kumzuia asiwafundishe mashahidi wengine juu ya ushahidi watakaotoa kwa kuwapigia simu au kuwatumia ujumbe wa maandishi kwa simu za mkononi au *e-mail* au *blackberry* au *skype* au aina nyingine nyingi za TEKNOHAMA. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri maswali yote haya kisheria yapatiwe majibu ya kuridhisha kabla mapendekezo ya haya muhimu hayajaletwa Bungeni ili yapitishwe na kuwa Sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niende kwenye mapendekezo ya kubadili Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 ya Sheria za Tanzania. Kambi Rasmi ya Upinzani haina matatizo na mapendekezo ya kubadilisha kichwa cha Sehemu ya XVII ya Sheria hiyo wala mapendekezo ya kubadili vifungu vya 170, 171A na kufuta kifungu cha 173 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu. Kuhusiana na mapendekezo ya kubadili vifungu vya 285, 287A na 287B vya Kanuni ya Adhabu kwa kutofautisha kosa la ujambazi wa kutumia silaha lililoko chini ya kifungu cha sasa cha 287A na kosa la ujambazi wa genge. Nimetumia ujambazi wa genge *a quick translation* kama inavyopendekezwa kuwa chini ya kifungu kipya cha 285(2), Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba hakuna sababu yoyote ya kisheria ya kufanya mabadiliko hayo. (*Makofi*)

Kwanza, vitendo vinavyoashiria kosa la ujambazi wa kutumia silaha Walatini wanaita *Actus Reus* ni lile lile katika makosa yote mawili. Vilevile nia ovu au nia ya kufanya kosa inayoitwa na walatini *mens rea* ni ile ile kwa makosa yote mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, adhabu inayopendekezwa kwa kosa jipya la ujambazi wa genge ni ile ile iliyowekwa kwa kosa la ujambazi wa kutumia silaha yaani kifungo kisichozidi miaka thelathini jela pamoja na viboko au bila viboko. Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kwamba mapendekezo haya yanatokana na uelewa potofu wa maneno mtu yeyote yaliyotumika katika kifungu cha 287A kudhaniwa kwamba yanahusu mtu mmoja tu anayetuhumiwa kufanya kosa la ujambazi wa kutumia silaha. Lakini kama kifungu cha 8(c) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya Kwanza ya Sheria za Tanzania kinavyoweka wazi, pale kifungu cha sheria kinapotumia neno la umoja (*singular*) kinahesabika kwamba kimetumia neno la uwingi vilevile na *vice versa*.

Kwa hiyo, Sheria inaposema mtu yeyote katika kifungu cha 287A ina maana hiyo hiyo wakifanya wawili au mia mbili, kwa maana hiyo mapendekezo ya kubadilisha vifungu hivyo hayaongezi thamani yoyote katika sheria husika na kwa hiyo, hayana ulazima wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inatofautiana pia na mapendekezo ya kubadilisha kifungu cha 132 cha Kanuni ya Adhabu kwa kuweka adhabu ya viboko au vifungo vya miezi sita au kumi na mbili jela kwa watoto wa chini ya miaka kumi na nane wanaopatikana na kosa la kujaribu kubaka. Kwanza, mapendekezo haya hayajafafanua umri hasa wa mtoto anayeweza kufanya kosa hilo la kujaribu kubaka. Kama alivyosema Mwanasheria Mkuu wa Serikali Kifungu cha 15 cha Kanuni ya Adhabu, kimeweka *Principles of Criminal Responsibility* na inasema wazi kifungu kidogo cha (3) mtoto wa umri wa miaka kumi na mbili au chini yake anahesabika kuwa hana uwezo kisheria wa kufanya tendo la ngono. Kama hawezi kutenda tendo la ngono, mtoto wa umri huo hawezi kubaka au kujaribu kubaka. Nazungumzia Sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha chini ya kifungu cha 15(1) cha Sheria hiyo, kinasema mtoto wa miaka kumi au chini yake anahesabika kuwa hana uwezo wowote kisheria wa kutenda kosa lolote la jinai na vilevile mtoto wa umri wa miaka kumi na mbili au chini yake hana uwezo wa kufanya kosa lolote la jinai vinginevyo uwepo ushahidi wa kuthibitisha kwamba wakati anafanya kosa hilo alikuwa na uwezo wa kufahamu kwamba hatakiwi kulifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mapendekezo ya kubadili kifungu cha 132 hayajazingatia kanuni hizi za uwezo wa kisheria wa watoto katika makosa ya jinai. Cha hatari zaidi endapo mapendekezo haya yatapitishwa kama yalivyo yanaweza yakatafsiriwa na Mahakama zetu kwamba yana nguvu kuliko matakwa ya kifungu 15 cha Kanuni ya Adhabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufuata hizo *Principles of Statutory Interpretation* nilizoielezea mwanzoni kwamba kuna mkinzano wa kisheria, Sheria iliyotungwa

baadae ndiyo inakuwa na nguvu kuliko Sheria iliyotungwa mwanzo. Tunaweza tukawa tunafanya *amendment by implication* kwa kupitisha Muswada kama huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile mapendekezo haya hayajazingatia matakwa ya kifungu cha 119(1) cha Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 ambacho kinakataza adhabu ya kifungu jela kwa watoto. Aidha, mapendekezo ya kutoa adhabu ya viboko dhidi ya watoto yanakwenda kinyume na Mikataba ya Kimataifa ya Haki za Binadamu na Haki za Watoto ambayo Tanzania imeridhia. Hatua hii ina hatari ya kuifanya Tanzania ionekane kwamba inaridhia Mikataba ya Kimataifa ya Haki za Watoto sio kwa lengo la kuitekeleza, bali kwa lengo la kupatia misaada kutoka Taasisi za Kimataifa zinazohusika na haki za watoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria ya Uchawi sura ya 18 ya Sheria za Tanzania. Mapendekezo yaliyoletwa kuhusiana na Sheria ya Uchawi ni kuongeza adhabu za kifungu au faini zilizopo kutoka faini ya shilingi mia moja na hamsini hadi shilingi milioni moja na kuongeza kifungu kutoka miezi isiyozidi miwili hadi kifungu kisichozidi miaka miwili. (*Makofi*)

Kambi Rasmi ya Upinzani haikubaliani na mapendekezo haya. Kwanza, kosa linalopendekezwa kuongezewa adhabu sio kosa la kuwa mchawi chini ya kifungu cha 3 au makosa mengine yaliyotajwa na Sheria hiyo. Kinachoongezewa adhabu ni kosa la kutotii amri ya Mkuu wa Wilaya au ya Mkuu wa Mkoa au Rais inayomlazimu mtuhumiwa wa uchawi kuishi katika eneo tofauti na makazi yake ya kawaida. Kwa hiyo, kinachoadhibiwa hapa sio kosa la uchawi ni la huyo ambaye anaitwa mchawi akiambiwa nenda Nachingwea akikataa kwa mapendekezo haya ataambiwa alipe faini ya shilingi milioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa utaratibu mzima wa Sheria ya Uchawi hauruhusu *due process*. Hairuhusiwi huyo mtu anayeitwa mchawi kushtakiwa Mahakamani, kujitetea anapochunguzwa na Mkuu wa Wilaya Sheria haiweki wazi kwamba anaweza akaoneshwa ushahidi dhidi yake na vitu kama hivyo. Ndiyo maana miaka 20 iliyopita Tume ya Rais ya Uchunguzi wa Mfumo wa Kisiasa wa Chama Kimoja au Vyama Vingi vya siasa ilipendekeza katika ripoti yake ya mwaka 1991 kwamba Sheria ya Uchawi ifutwe kwa sababu inapingana na haki za msingi zinazotambuliwa na kulindwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Kuendelea kuwepo kwa Sheria hii katika vitabu vyetu vya Sheria kuna hatari ya kutufanya tudhahiwe na watu wengine kwamba hata katika Karne ya 21 Serikali ya Jamhuri ya Muungano bado inaamini mambo ya kichawi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende katika Sheria ya Mwenendo wa Jinai ambayo vilevile inapendekezwa ifanyiwe marekebisho makubwa. Kambi Rasmi ya Upinzani haiafikiani na mapendekezo ya kurekebisha vifungu vya 222 na 226 vya Sheria ya Mwenendo wa Jinai. Kifungu cha 222 cha Sheria ya sasa kinaiielekeza Mahakama kumfutia hatia na kumwachia huru mtuhumiwa wa kosa la jinai pale ambapo mlalamikaji

ambaye alikuwa anataarifa ya siku ya kusikiliza kesi ana mahala pa kusikiliza kesi anaposhindwa kufika Mahakamani.

Lakini pamoja na Mamlaka hayo ya Mahakama kufuta hatia na kumwachia mtuhumiwa huru bado kifungu hicho hicho kinairuhusu Mahakama kwa sababu maalum na kama itaona inafaa kuahirisha kesi hadi wakati mwingine. Kwa hiyo, kifungu cha 222 hakiipi Mahakama *automatic power to acquit the accused person*, ikiangalia mazingira ikaridhika kwamba hili kosa ni *serious* zaidi inaweza isifute hatia ikaelekeza kesi iendelee siku nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wake, kifungu cha 226 cha Sheria hiyo, Mahakama vilevile inapewa mamlaka hayo ya kuwafutia watuhumiwa hatia na kuwaachilia huru pale ambapo walalamikaji wanashindwa au kupuuzwa kwenda mahakamani wakati wa kusikiliza kesi za jinai. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa inapendekezwa Muswada huu kwamba badala ya Mahakama kuwa na mamlaka ya kufuta hatia, Mahakama iwe na uwezo wa kufuta kesi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nieleze tofauti, ni tofauti kubwa sana. Mahakama inapofuta hatia chini ya Kifungu cha 222 cha Sheria ya Mwenendo wa Jinai, huyo aliyefutiwa hatia hawezi akashitakiwa tena kwa kosa hilo hilo, kwa matendo hayo hayo kwa mujibu wa Kifungu cha 137 cha Sheria ya Mwenendo wa Jinai. Kwa hiyo, *aquito*, Mahakama inapo-*acquit*, inapofuta hatia, mtuhumiwa hawezi akarudishwa tena Mahakamani. Pale ambapo kwa upande mwingine, Mahakama inapofuta kesi, inapom-*discharge the accused person*, anaweza akashitakiwa tena kwa kosa hilo hilo, kwa matendo hayo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa maana nyingine, mapendekezo yaliyoletwa kubadili vifungu hivi viwili ni kuwezesha kukamatwa na kushitakiwa upya kwa watuhumiwa ambao vinginevyo wangeputiwa hatia na kuachiliwa huru na kama mapendekezo haya yatapitishwa kuwa sheria, ni wazi yatakuwa na madhara makubwa sana kwa ulinzi wa haki za wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa sheria kuruhusu vitendo vya kuwakamata mara kwa mara na kuwashitaki upya watuhumiwa waliokwishaachiliwa huru na Mahakama, ni sawa na kuwatendea kama watu ambao tayari wamepatikana na hatia ya makosa ya jinai na wanatumikia adhabu za makosa hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili kama ambavyo taarifa ya mwaka ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, ripoti yake ya mwaka 2008 ilivyosema Jeshi la Polisi limekithiri kwa vitendo vya kubambikizia wananchi kesi za uongo kwa lengo la kuwakomoa au kuwakamua kwa kuwadai rushwa ili waachiliwe. Aidha, kufuatana na taarifa hiyo ya Tume ya Haki za Binadamu, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka ya Jinai inakabiliwa na tuhuma nyingi za ucheleweshaji wa kesi za jinai. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ni mbaya zaidi kwa kuwa kutokana na sababu za kisheria, makosa mengi ya jinai katika sheria zetu yamefanywa kuwa hayana dhamana. Kwa sababu hiyo, watuhumiwa wengi wa makosa ya jinai wanakaa Magereza ya rumande kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niseme neno moja kuhusiana na huu uwezekano wa kuwarudisha watu Polisi na Mahakamani kila mara. Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Ibara ya 13(6)(b) inakataza mtu aliyeshitakiwa kwa kosa la jinai kutendewa kama mtu mwenye kosa hilo mpaka itakapothibitika kuwa anayo hatia ya kutenda kosa hilo. Aidha, Ibara ya 107A(2)(b) ya Katiba inazielekeza Mahakama kutokucheleweshwa haki bila sababu ya msingi pale zinapotoa uamuzi wa mashauri ya jinai kwa kuzingatia sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, Tume ya Haki za Binadamu imesema ucheleweshaji wa upelelezi wa kesi na uendeshaji ni ukiukwaji wa Haki za Binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora. Kama vifungu hivi vitabadilishwa kama inavyopendekezwa, milango itakuwa wazi ya kuweka watu wetu Magereza, Magereza yakafurika, Haki za Binadamu na Misingi ya Utawala Bora itakuwa imekiukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani haina pingamizi lolote juu ya mapendekezo ya kubadilisha vifungu vya 58, 192(1), 345, 383 na 392 vya Sheria ya Mwenendo wa Jinai. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchunguzi wetu wa Sheria ya Mwenendo wa Jinai, hatujaweza kuona Kifungu cha 129A, na kwa hiyo tunaamini kwamba mapendekezo ya kubadili Kifungu hicho yameletwa kimakosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani vile vile haina matatizo na mapendekezo ya kubadilisha vifungu tajwa vya Sheria ya Chuo cha Teknolojia cha Dar es Salaam, Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi, Sheria ya Usajili wa Wakandarasi, Sheria ya Wakala za Kiutendaji (*Executive Agency's Act*) na Sheria ya Mamlaka za Miji katika Serikali za Mitaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Sheria ya kurejesha watoro, Kifungu cha 13(1) cha hiyo *Extradition Act*, kinamruhusu Hakim Muziki kutoa mamlaka ya muda ya kumkamata mtuhumiwa pale ambapo mamlaka kamili ya kumkamata haijaridhiwa (hiyo mamlaka kamili kutoka nchi nyingine ambayo tuna *Extradition Treaty* nayo).

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa inapendekezwa kwamba Maafisa wa Polisi kwa sasa wawe na uwezo wa kuwakamata watuhumiwa bila mamlaka ya kuwakamata kuridhiwa na Hakim na hata bila kuwepo kwa mamlaka ya muda ya kuwakamata.

(*Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji*)

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, imekwisha?



**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Tundu Lissu kwa maoni hayo ya Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Niunge mkono! Heheee! *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa kweli muda hauko upande wetu sana, kwa jinsi hiyo itategemeana na wachangiaji wangu kama watachangia kwa kifupi, tunaweza tukapata wawili. Wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa na kama muda utaruhusu, tutampata Mheshimiwa Assumpter Mshama. Mheshimiwa Mchungaji Msigwa karibu.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kabla sijachangia Muswada huu, naomba nitoe pole kwa Manispaa ya Iringa kwa kumpoteza Diwani mmoja wa CCM ambaye amefariki dunia na wamemzika leo. Wananchi wa Manispaa ya Iringa tuko pamoja, poleni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda umeenda sana, nilitaka tu nichangie kwa kifupi pamoja na mambo mengi yaliyozungumzwa na pamoja na mapendekezo ya Kambi ya Upinzani, lakini kuna sheria nyingi ambazo zinakinzana na Haki za Binadamu. Kwa hiyo, pamoja na mapendekezo mazuri na nia njema ambayo Serikali inayo, kwa mfano, haifafanui vizuri katika kipengele hiki ambacho ni cha mtoto ambaye ana umri chini ya miaka 18. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria inasema kwamba mpaka ithibitishwe kwamba alipokuwa akitenda kosa awe anajua alikuwa anatenda. Lakini Serikali inaweza ikatuambia inaweza ikathibitisha vipi kwa sababu huyu ni mtoto haelewi, sasa uthibitisho utakuwaje? Kwa hiyo, pamoja na kwamba tunaweza tukalazimisha kuyapitisha, ni mambo ambayo hayaelezi kiufasaha unathibitisha vipi kwa sababu ni mtoto yupo chini ya umri wa miaka 18. Sasa tutathibitisha vipi na sheria inasema kwamba yeye hana uelewa huo. Kwa hiyo, sheria kama hizi tukizipitisha kwa haraka haraka, tunaweza tukajikuta baadaye zinakinzana na zinaleta madhara katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sheria nyingi, pamoja na hizi ambazo zimejadiliwa, kuna sheria zingine ambazo ni za kuwakamata watu, wanapelekwa mara kwa mara polisi kama hii ambayo imejadiliwa tena hapa, utakuta mtu amekushitaki, lakini bado hafiki Mahakamani, na sheria bado inasema kwamba ukifutiwa kesi bado unaweza ukakamatwa tena. Kwa hiyo, ikitokea sheria kama hii, mtu akiwa na chuki na wewe, inaweza ikawa ni mchezo tu wa kushinda Mahakamani, unakwenda unarudi, unafutiwa kesi, unarudi. Kwa hiyo, ikawa ni mchezo ambao hauwezi ukamsaidia mwananchi na inakuwa ni usumbufu mkubwa kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile kuna sheria hii ambayo inampa madaraka Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa, yeye anaweza akaamrisha kwamba uhamie mahali fulani. Lakini *let's say* sasa hivi Wakuu wa Wilaya wengi na Wakuu wa Mikoa wengi ni makada wa vyama, anaweza akamtuhumu tu Mwenyekiti wa CHADEMA au wa *TLP* au wa *CUF* kwamba ni mchawi, kwa hiyo akaamua tu kwamba aondoke. Sheria kama hizi kama hazitawekwa mipaka maalum na zikawekwa mazingira mazuri, zinaweza zikawakandamiza sana wananchi wa Tanzania na hatimaye zikatuletea madhara, kama hazitafafanuliwa vizuri, zikatuweka katika mazingira mazuri, namna gani tunaweza kuzifanya. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kama maoni ya Kambi ya Upinzani Rasmi yanavyosema, ni sheria ambayo inamlinda anayetoa amri ambaye ni Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya, lakini haizungumzi huyu ambaye ametuhumiwa uchawi, haielezi anajitetea vipi, kwa hiyo, mtu anapewa amri tu na Kiongozi wa Serikali, lakini mhusika mwenyewe hana nafasi ya kujitetea.

Kwa hiyo, katika mazingira kama haya, nadhani ni vizuri tukafafanua kwa upana ni namna gani mtu anaweza kujitetea. Lakini vile vile, huyu mtu anahamishwa kutoka eneo fulani kwenda eneo fulani, sasa kama kweli ni mchawi, hilo eneo kwa nini limpokee? Kwa nini eneo lingine limpokee huyu mtu kama ni mchawi? Nani anataka kupokea wachawi? Kwa hiyo, bado ni sheria ambayo haiendi na wakati, inaturudisha nyuma kama watu ambao tunakwenda na teknolojia ya sasa. Ningependekeza sheria hii ifutwe, haitusaidii, haina tija. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, kwa ajili ya kuokoa muda kwa watu wengine, asante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Asante sana. Mheshimiwa Assumpter Mshama, ukienda kifupi pia nitakushukuru. (*Makofi*)

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Na mimi nataka nitoe mchango wangu juu ya Sheria hizi katika Ibara ya 10 ya Miswada ya Serikali iliyowasilishwa, Kifungu Na. 287 hii Sheria Na. 5. Mimi nilikuwa tu nataka kujikita sana katika habari ya namna gani kesi zinavyochukua muda mrefu Mahakamani. Utakuta kesi moja ni kosa la jinai kama ilivyosemwa au mtu ameuua mwenzake au kesi ina siku nyingi, miaka mitano, hata kesi zingine zinafikisha miaka kumi.

Mimi nilichokuwa naomba tu hiki kifungu kiweze kunisaidia, ni namna gani wale Mahakimu ambao wanakaa na kesi hizi za jinai kwa muda mrefu, wanawezaje kutusaidia au wao sheria hii inasema nini juu yao. Mtu anakaa na kesi, anazaliwa mtoto anakuta baba ana kesi, miaka mitano inapita na baadaye kesi hii inaweza ikaisha maana vidhibiti vinaweza hata kupotea. Kwa hiyo, mimi ningependekeza au ningepomba tu Serikali, msemi pia upande wa Hakimu anayeshughulika na zile kesi za kuchukua muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho mengine yanayopendekezwa, yanayohusu Kifungu cha 345, ukiangalia nchi yetu kuamua tu mtu yeyote kusema ni

namna gani pesa zinazotakiwa kulipwa kwa uwezo wa mtu au Hakimu kuamua, kwa nini isiwekwe sheria ya kwamba ni shilingi ngapi na kiasi gani ambacho mtu anaweza kutozwa ili kuondoa rushwa zinazoweza kutokea katika kesi za namna hiyo. Kwa hiyo, pia hata katika ile kesi ya kuchelewesha kesi muda mrefu, kwa nini tusiweke siku au kesi ikifikisha miaka miwili, kama ni ya jinai ya namna yoyote, hata kama kuna upelelezi au kipindi kinapita kwa sababu ya kesi kupelelezwa, lakini ni vyema tukaweka muda ili Hakimu atakayekuwa amehusika na hiyo na hiyo kesi, hiyo kesi isemwe miaka mitatu kesi hiyo iwe imeisha au ni namna gani kesi isiendelee kuwa Mahakamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba kwa kweli, tumeona kesi zinakaa sana, watu wanapoteza ushahidi, watu wengine wanafungwa bila kosa. Unakuta kipindi kinapita muda mrefu hata tunapoteza ushahidi, na watu wengine hufa wakati kesi zinaendelea Mahakamani. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nachangia pia Mahakimu waweze kupewa kipindi maalum kwamba kama ni kesi isizidi miaka mitatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi huo ndio mchango wangu katika makosa ya jinai. Tumeona nchi yetu...

#### **TAARIFA**

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Tundu Lissu!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwa Mheshimiwa Mbunge anayezungumza sasa hivi kwamba chini ya Sheria ya sasa hivi ya Mwenendo wa Jinai, Kifungu cha 225(4), kesi ya jinai inatakiwa iwe imeanza ndani ya siku 60 na iwe imeisha ndani ya miaka miwili *maximum*. Kwa hiyo, siyo kwamba hakuna utaratibu, hiyo *limit* ya kuendesha kesi za jinai. Asante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Assumpter!

#### **TAARIFA**

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Taarifa, Mheshimiwa Zainab Kawawa!

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, msemaji aliyepita ametoa taarifa lakini hakutuelekeza kwenye Kanuni za Bunge. Asante.

**NAIBU SPIKA:** Asante sana kwa wote. Wote mko sahihi, lakini suala la taarifa linamtegemea sana aliyekuwa akiongea, endapo hiyo inaweza ikamsaidia katika mchango wake au vinginevyo. Kwa hiyo, kwa kawaida, kiti kinamrudishia Mheshimiwa Assumpter Mshama kuona kama inaweza ikamsaidia katika mchango wake au

vinginevyo, na anaruhusiwa kuipokea au kutoipokea. Mheshimiwa Assumpter, endelea! (*Makofi*)

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee na mawazo yangu kwa sababu kama hiyo sheria ipo, ninachoomba mbele ya Bunge lako tukufu kwamba hiyo sheria ifanye kazi ili hizo kesi ziweze kutoka Mahakamani mapema kuliko kurundikana na kesi ndani ya Mahakama. Kwa mchango wangu juu ya sheria hiyo, naomba sasa wazo langu lichukuliwe kama nilivyoomba. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Assumpter Mshama. Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli tulikuwa na lengo kama ingewezekana tumalize jambo hili lililo mbele yetu linalohusiana na Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, tungependa kumaliza leo. Lakini hata kwa mamlaka niliyopewa ya kuongeza nusu saa, kwa vyovyote vile hatuwezi kumaliza. Kwa jinsi hiyo itabidi jambo hili liendelee kesho asubuhi pamoja na mambo mengine. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa na wachangiaji kama wawili, watatu tu, lakini hapa mwishoni nikapata vikaratasi vingi kwa mpigo. Niwakumbushe tu Waheshimiwa, usipoomba kuchangia mpaka *session* ya asubuhi ikaisha, huwa siyo rahisi sana kwa jioni kama sasa hivi ukapata nafasi. Kwa vile tutaendelea kesho, basi tutaangalia hali ilivyo na watakochangia hiyo kesho, basi tutatoa orodha yake kesho hiyo hiyo asubuhi. Nafikiri wengine wanachangamka baada ya kusikiliza hoja mbalimbali, lakini wanakuwa wamechelewa kidogo.

Sasa kuna mambo mawili, matatu; moja ya sababu kwa nini vile vile tunasogeza mpaka kesho, ni kwamba Wabunge wengi hamjapata nakala za hotuba aliyoisoma Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wala nakala za Maoni ya Kambi ya Upinzani. Tuna hakika zitapatikana, kila mmoja awe nazo kusudi kuupeleka mjadala vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani yeye ameniuliza kwamba wakati Msemaji wa Kambi ya Upinzani akisoma hotuba ile mara kwa mara alirudia maneno ya msimamo wa Kambi Rasmi ya Upinzani, akaniuliza kwani Kambi isiyo Rasmi ya Upinzani ni ipi hapa Bungeni? (*Makofi*)

Nijibu tu kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani kufuatana na Kanuni yetu ya 14(2), ni Wabunge wote ambao hawatoki Chama Tawala, hao ndio Kambi Rasmi ya Upinzani.

Kama ikitokea likachaguliwa Bunge, Wabunge wa Upinzani wote kwa ujumla wao wasiwe ile asilimia 12.5 inayozungumzwa humu, kama hawakufikia idadi hiyo, hawataweza kupata Kiongozi wa Upinzani wala kuunda Kambi Rasmi ya Upinzani. Kwa hiyo, hao wachache watakuwepo tu lakini hawatatambulika kwa maana ya Bunge. Lakini ikishakuwa Wabunge wote wa Upinzani wanazidi ile *threshold* ambayo imewekwa

kwenye Kanuni zetu, basi tunawatambua kwamba ni Kambi Rasmi ya Upinzani kama ilivyo sasa. (*Makofi*)

Nisome matangazo kama mawili, la kwanza, linatoka kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama ambaye ni Katibu wa Wabunge wa CCM, anawakumbusha Waheshimiwa Wabunge wa CCM wote uwepo wa kikao cha Kamati ya Wabunge wa CCM mara tu baada ya kuahirisha Bunge jioni hii. Kwa hiyo, Wabunge wote wa CCM, kikao ukumbi wa Msekwa. (*Makofi*)

Naomba kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge umuhimu wa kuhudhuria vikao vya jioni. Naona kama baadhi wanakuwa kidogo vikao vya jioni na hasa wakati tunapopitisha Miswada ya Sheria hii, ni muhimu sana kwa sababu masuala ya *quorum* ni muhimu katika kupitisha maamuzi. Kwa hiyo, nawaomba wanaokuwepo Dodoma, ni vizuri sana kuhudhuria jioni pia kutusaidia katika maamuzi. (*Makofi*)

Tangazo la mwisho, kwa kweli ni kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya mambo ambayo yamekuwa yakitokea kwenye milango yetu ya kuingia Bungeni, naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kuwa tunao utaratibu wa mavazi ya kuvaliwa wakati wa vikao vya Bunge hapa Dodoma yanayoitwa Vazi Rasmi.

Waheshimiwa Wabunge, mavazi haya rasmi kwa taarifa tulizonazo mpaka sasa kwa Waheshimiwa Wabunge wanaume imekuwa hakuna tatizo ambalo limejitokeza, wanafuata utaratibu unavyokwenda na nichukue fursa hii kuwapongeza. (*Makofi*)

Lakini vile vile kwa Wabunge akinamama, kwa asilimia kubwa sana vile vile hakuna tatizo la masuala ya mavazi. Lakini kwa asilimia ile ndogo, nisome kidogo; vazi rasmi kwa Wabunge Wanawake ni vazi lolote la heshima na hii imetoa nafasi pana ambapo ukisoma kwa Wabunge, hakuna neno vazi lolote, mavazi ya wanaume yako *specified* ni mavazi ya aina gani. Kwa hiyo, kwa akinamama ni vazi lolote la heshima, yaani ambalo si la kubana mwili, lisiloonesha maungo ambayo kwa mila na desturi za Kitanzania hayapaswi kuonekana na ni refu kuvuka magoti. (*Makofi*)

Sasa pamekuwa na mavazi ambayo ni ya kubana kwa baadhi yanayoonyesha mwili (*figure*), lakini vile vile mavazi hayo yanayobana, baadhi yake hayavuki magoti kuteremka chini. Kwa hiyo, baadhi yetu tunapata matatizo kidogo kwenye mageti na inashauriwa kwamba wakati mwingine ukirudishwa getini basi usichukulie kwamba kuna tatizo, ni kwa sababu Kanuni hizi tumeziweka sisi wenyewe ili tuweze kuzifuata sisi wenyewe. Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema...

**MBUNGE FULANI:** Vilemba!

**NAIBU SPIKA:** La vilemba halijajitokeza. Lipo humu, vilemba vile virefu kama vya Nigeria vile vya kumkinga mwenzako aliyeko mbele navyo vinazuiliwa, lakini halijajitokeza. Kanuni inasema kilemba kivaliwe cha kadri, au mtandio na kadhalika. Tujikumbushe tu wale ambao tuna muda, tupitiepitie kidogo kuangalia, inasaidia kidogo. (*Makofi*)

Baada ya maelezo hayo, shughuli zote zilizopangwa kwenye *Order Paper* zimekamilika, isipokuwa tutaendelea na Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2011 katika shughuli zetu za mpangilio wa shughuli za kesho. Kwa maelezo hayo basi, naomba sasa kwa vile muda uliobaki ni mdogo sana, hatuwezi kuendelea, basi niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi. (*Makofi*)

*(Saa 1.40 usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano,  
Tarehe 13 Aprili, 2011 saa tatu asubuhi)*